# Hatua Nne za Uamsho

## Kuuandaa Mwili wa Kristo kwa Uamsho Mkubwa Kuliko Siku Zote

**Dk. Dalen Garris**

**Revivalfire Ministries**

# Hatua Nne za Uamsho
## *Kuuandaa Mwili wa Kristo kwa Uamsho Mkubwa Kuliko Siku Zote*

Hakimilki © 2022 Na Dk. Dalen Garris
Revivalfire Ministries.

***Haki Zote Zimehifadhiwa.*** *Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki itakayotolewa, wala kuhifadhiwa kwa mfumo wa kompyuta, au kunakili kwa namna yoyote ile—kielektroniki, kiufundi, kutoa kopi, kurekodi, kuskani, ama vinginevyo—isipokuwa kuchukua nukuu fupi kama rejea muhimu au kuandika makala—bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.*

*Isipokuwa iwe imetajwa, nukuu za Maandiko Matakatifu zimechukuliwa kutoka kwenye Biblia toleo la Union Swahili Version (USV) tafsiri ya Kiswahili cha Kimvuta.*

This book was first published in the United States of America with the title "**Four Steps to Revival.**"
Copyright © 2021 by Dr. Dalen Garris.

Translated in Tanzania where Swahili originates by:
Ev. Kadama M. Kadama
klmkadama@gmail.com or DIMmissionstz@gmail.com.

Copyright © 2021 For English edition with the title "**Four Steps to Revival**":
Dr. Dalen Garris
Revivalfire Ministries
PO Box 822, Waxahachie, TX.
dale@revivalfire.org
www.RevivalFire.org.

Kwa toleo la Kiswahili linaloitwa "**Hatua Nne za Uamsho"** wasiliana na:
Askofu Festo Benjamin
Divine Intervention Ministries (D.I.M.)
Nyakato Gedeli
P.O. Box 1844
MWANZA Tanzania.
+255767999115
DIMTanzania@gmail.com au festobenjamin8@gmail.com

Kimepigwa chapa nchini Marekani/Printed in the United States of America.

# Tunu

Kitabu hiki kimetunukiwa kwa askari wote wa zamani wa Roho Mtakatifu kutoka Mtaa wa Azusa waliokuja kujionea vijana wa harakati ya Jesus Movement wakiwaka moto ule ule waliouona miaka 50 kabla. Walitutia moyo kuzidi kuamini katika huu uamsho mkubwa, wa mwisho, ulioahidiwa katika Kitabu cha Yoeli.

Maombi yangu na matumaini yangu ni kwamba kitabu hiki kikaweze kupeleka ule moto kwenda kwa hiki kizazi kingine cha Gideoni na kuwahuisha watu watakaoupeleka majumbani kwao.

# Yaliyomo

**Tunu** .......... ii

**Dibaji** .......... vii

**Utangulizi** .......... 1

**Sura ya 1** .......... 5

**Kujirudiarudia kwa Ukengeufu na Uamsho** .......... 5

**Sura ya 2** .......... 11

**Uamsho Mkubwa Kuliko Siku Zote** .......... 11

**Sura ya 3** .......... 18

**Kanuni Sita za Uamsho** .......... 18

1. Uamsho Unahusu Kuwaokoa Waliopotea .......... 18
2. Injili Haikuhusu Wewe Uliyeokoka .......... 20
3. Kila Jambo katika Mungu Lina Gharama Yake .......... 21
4. Hakuna Uamsho Utakaokuja Bila Toba .......... 22
5. Kila Uamsho Lazima Uombewe .......... 24
6. Lazima Awepo Mbeba Maono .......... 28

**Sura ya 4** .......... 32

**Hatua ya 1: Kutambua** .......... 32

Madhabahu Zilizokufa .......... 35
Maonyo Kutoka kwa Nabii Yoeli .......... 40
Miujiza Iko Wapi? .......... 52
Wosia wa Mwisho wa Yesu .......... 55
Huruma, Siri ya Uamsho .......... 57
Mwanamke Aliye Tasa .......... 60

Kilio cha Raheli ........................................................ 63
Uvivu na Upinzani Kwenye Mabadiliko .................... 65

**Sura ya 5 ........................................................71**

**Hatua ya 2: Toba ................................................71**

Wito Kwenye Utakatifu wa Mtu Binafsi .................... 71
Toba ya Ushirika ........................................................ 75
Maombi ya Toba ya Danieli ...................................... 77
Nehemia........................................................................ 80
Changamoto ya Eliya ................................................ 82
Kushindwa kwa Kanisa Kuokoa Nafsi ...................... 85

**Sura ya 6 ........................................................88**

**Hatua ya 3: Jinsi ya Kuuwasha Moto Katika Kanisa ........................................................88**

Harusi ya Kana ........................................................ 92
Eliya Juu ya Mlima Karmeli ...................................... 95

**Sura ya 7 ........................................................100**

**Wito wa Vita ........................................................100**

**Sura ya 8 ........................................................108**

**Hatua ya 4: Kuokoa Nafsi, Siri ya Uamsho........108**

Mausia ya Mwisho .................................................. 110
Karamu Kubwa.......................................................... 111
Kilio cha Raheli.......................................................... 113
Tumeokolewa ili Tuzae Watoto .............................. 114
Mzabibu wa Kweli .................................................... 115
Kuitikia Kwenye Wito................................................ 117
Amri Kuu .................................................................. 119

Kanisa la Efeso ........................................................ 121
Huruma au Upendo ..................................................... 123
Isaya 58 – Ahadi ya Mungu ya Baraka .................... 124
Hukumu ya Kondoo na Mbuzi.................................. 133
Mfano wa Talanta ...................................................... 136
Mfano wa Msamaria Mwema................................... 138
Kipofu Bartimayo ....................................................... 141
Habari Moja ya Mwisho ............................................ 144

**Sura ya 9 ....................................................... 147**

**Nenda Kaokoe Nafsi!......................................... 147**

Jinsi ya Kufanya Jambo Hili ..................................... 149
Mpango wa Wokovu................................................ 151

**Sura ya 10 ..................................................... 155**

**Hatua za Utekelezaji........................................ 155**

1. Soma Biblia Kila Siku.......................................... 155
2. Jiwekee Muda wa Kuomba Kila Siku .................. 157
3. Kuosha Miguu na Ushirika Mtakatifu ................. 160
4. Waangalizi ........................................................... 163
5. Weka Wakristo Waliokomaa Kwa Kila Mkristo Mchanga Anayeokoka ............................................ 163
6. Uwe na Maono ...................................................... 164
7. Umezaliwa Mara ya Pili? .................................... 166
Tubu dhambi zako. ..................................... 167
Mkiri Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako ......................................................... 168
Mwombe Yesu akuokoe na kukusafisha ndani ya Damu yake ............................................ 168

Amini........................................................ 168
Mshukuru Mungu ...................................... 168
**Hitimisho .......................................................170**
**Kuhusu Mwandishi.........................................174**

# Dibaji

Niliishi kama "mwanariadha wa jiwe baridi" katika miaka ya sitini ya uasi. Niliona haiwezekani kuamini katika mungu nisiyemwona, nisiyemhisi, wala kumgusa. Hasa hasa niliudharau Ukristo, nikiamini kwamba Ukristo ulikuwa ni jambo la hasara ambalo lilikuwa halijawahi kutokea ulimwenguni. Mwaka 1969, hata hivyo, Mungu akaniletea ufunuo usio wa kawaida ambao, kwa kweli, Mungu alionekana kwamba aliujaza ulimwengu wote. Nikisumbuliwa na maono haya makubwa, nilitoa ufadhili wote katika Chuo Kikuu cha Boston kusaka nchini mwote ili kumtafuta huyu Mungu ambaye alijidhihirisha mwenyewe kwangu.

Mwezi wa pili mwaka 1970, niliokoka katika kanisa dogo mjini Hollywood, California, nchini Marekani, mwanzoni tu mwa huduma ya Jesus Movement. Tulikuwa na rasilimali chache sana—yaani kanisa dogo sana lenye vijana wadogo kadhaa waliokuwa moto—lakini Roho na nguvu za Mungu zilimwagika ndani ya kanisa hilo kila siku. Ilikuwa ni kitu ambacho sikukiona kabla au baadaye. Jambo hili lilinibadilisha na kuniweke8a hatima ya maisha yangu ya baadaye.

Baada ya miaka mingi ya kushangaza katika huduma ya mitaani katika miji ya Marekani, nilifika mjini Dallas, Texas, na nikaanza kuendesha kipindi cha matangazo ya redio ambacho kilikua kutoka muda wa dakika kumi na tano katika soko la ndani hadi kufikia kipindi cha matangazo ya dakika thelathini ambacho

kilienea kimataifa hadi nchi nyingi, tangu Yerusalemu mpaka Asia. Matangazo yangu katika Yerusalemu yalikuwa ni marudio kama *Sauti ya Yerusalemu* kwenye redio ya mtandao wa satelaiti ya Sky Angel katika bara la Amerika ya Kaskazini kwa miaka mingi.

Makala zilizochapishwa kwenye magazeti mbalimbali zilifuata haraka baadaye baada ya matangazo ya redio, na hili likapelekea niwe na tovuti ya makala na kuzituma kwenye orodha ya baruapepe mtandaoni ambazo ziliwafikiwa mamia ya watu waliojisajili kwenye huo mtandao. Uzoefu huo ulinifanya nianze kualikwa nchi za nje.

Mwaka 2004 nilipokea mwaliko wa kuja Kenya kuhubiri kuhusu uamsho. Hii ilipelekea niwe na safari zingine katika nchi za ukanda wa jangwa la Sahara barani Afrika. Baada ya miaka 17, nilikuwa nimeshafanya safari 60 kwenda kwa makumi ya nchi, nilihubiri kwenye makanisa zaidi ya 1,000, na kujionea makumi elfu ya nafsi zikiokoka. Mamia ya miujiza ilitokea kwenye uamsho ambao ulimwagika, na moto uliwashwa kwenye mamia ya makanisa ambayo bado yanauwasha hata leo hii.

Wakati wote wa hiyo miaka ya mwanzoni mwa uamsho, niliombwa kuuweka ujumbe kwenye maandishi ili kwamba waumini wa makanisa ambao watasikia jumbe hizi wabaki nazo hata baada ya mimi kuondoka. Jumbe ambazo zilipatikana na kuongezeka wakati wote wa miaka hiyo zimepelekea kupatikana

kwa kitabu hiki, *Hatua Nne za Uamsho*. Zaidi ya nakala elfu hamsini zimechapishwa na kusambazwa barani Afrika.

Tumaini kuu moja la uvumilivu nililonalo katika miaka yote hii ni kwamba uamsho utakuja Marekani. Siamini kwamba utaanzia hapa Marekani kwa sababu sisi Wamarekani hatuna njaa sana ya kulipa gharama ambayo uamsho wa kweli unataka, bali kama moto wa uamsho utawaka katika Afrika, naamini ndipo utaenea mpaka hapa Marekani.

Marekani na Uingereza waliuinjilisha ulimwengu. Walipeleka hii hii Injili ambayo sasa wanakerwa na ulimwengu wote, ikiwemo Afrika. Hasa hasa Afrika! Na ni Afrika, ambamo kuna watu wenye njaa kwamba hutembea kwa muda wa masaa 12 mpaka 13 wakitafuta kusikia Neno la Mungu linalohubiriwa, naamini hali hii itazaa uamsho wa siku za mwisho ambao Mungu ameuahidi. Na huenda, labda, kwamba moto ule ule utaenea hadi huku kwetu sisi ambao tuliupeleka huko Afrika nyakati za mwanzoni.

Neno la Mungu linatwambia kwa kurudiarudia kwamba rehema/huruma huzaa rehema/huruma. Mungu na atukumbuke kwa rehema, atifue udongo mgumu mioyoni mwetu, na kuturejeshea ukuu wa uwepo wake na kutuletea uamsho.

# Utangulizi

Kitabu hiki kimezaliwa kutokana na jumbe nilizohubiri mfululizo kwa makanisa mengi katika miaka ishirini na moja iliyopita. Nimeuzingatia kama ujumbe wa matumaini na upatanisho unaowabadilisha watu na kuwapa nguvu. Kwa mara nyingine tena kutoka wakati mmoja hadi wakati mwingine, uamsho uliotokea umesababisha makanisa haya kukua mara mbili, mara tatu, na mara nne, mara nyingine ndani ya miezi michache tu. Kadiri makanisa yanavyokua, yameenea na kuanzisha mamia ya makanisa mapya katika Afrika. Naamini hili ni agano kwao wenye njaa ambao hawajashiba kumtafuta Mungu na kwa ajili ya Injili iliyo na uweza wa kweli.

Kwa sababu Roho Mtakatifu ndiye aliyezitia mafuta mengi hizi jumbe, niliombwa kuziandika ili kwamba baada ya mimi kuliacha kanisa, wasikilizaji waweze kubaki na ujumbe kwenye kitabu kwa ajili ya rejea. Nimeambiwa kwa kurudia rudia sana kwamba jambo la kushangaza kuhusu kitabu hiki ni kwamba hatimaye kina mpangilio wa hatua kwa hatua ambao unaleta maana, rahisi kuuelewa, na unatoka kwenye Biblia. Ni kwamba ujumbe huu unatenda kazi. Si mgumu kielimu ya Mungu wala hauko vuguvugu wala kufifiafifia, yaani haupo katikati. Ni rahisi, una nguvu, na halisi. Na unatenda kazi.

Neno *uamsho* linachanganya, kwenye visa vingi, kwa sababu linaelezea kuhusu kuufufua tena mwili uliokufa. Lakini katika historia yote, mtembeo mkubwa wa Mungu umekuwa ni kinyume cha mfumo wa kidini ambao umebaki kuwa baridi na wa kidunia. Mara baada ya mwili kufa, kwa kuuamsha tu hatuwezi kuurudisha tena kuwa hai. Uzima mpya unaobubujika ndani ya mwili mpya unahitajika, sio ufufuo wa mfumo wa zamani uliokengeuka ukafa.

Naamini kwamba ufufuo ni tumaini bora lenye suluhisho kwenye matatizo makubwa ya kiroho yanayoukabili ulimwengu wetu leo. Kama wafanyavyo Wakristo wengi ambao wamekuwa wakitazama unabii wa Biblia ukiifunua habari hii, nina imani kubwa kwamba tunaishi kwenye majira ya siku za Mungu. Wakati wengi wanaamini tuna sababu chache za kutufanya tutahayarike kwa sababu wao hutegemea kuwa watanyakuliwa mbali na majanga yanayokuja juu ya uso wa dunia, naamini kwamba kanisa halitakabiliwa na majanga hayo tu bali pia litayapitia mpaka kurudi kwa Yesu mara ya pili kutakapotokea.

Shakespeare ameandika, “Ulimwengu wote ni hatua.” Hii ni kweli kuliko alivyotegemea yeye mwenyewe. Siasa, biashara, elimu na vipawa vyetu vyote katika maisha yetu ni mambo madogomadogo katika maisha ambayo tunayafanya kwamba hatimaye yaamue mwisho wetu wa milele. Kanisa linapaswa kuwa bango na nyumba inayoangaza kwa kuwaka taa

ambayo inaonyesha njia ya kwenda mbinguni ndani ya jamii ambayo mara nyingi imejisahau kuhusu matukio halisia ya ulimwengu wa asili na kiroho ambamo ndimo tunaishi sote.

Pale kanisa linapopoteza kuchangamka kwake na nuru yake kufifia, hata hivyo, hujiona wenyewe tukishikwa na mambo mengine yanayoamua kuhusu maisha yetu.

Shabaha yetu huhama kutoka hatima yetu ya milele kwenda kwenye ulimwengu wa sasa unaopita, na hofu ya hukumu ya milele huchukua kiti cha nyuma ndani ya mambo mengi ya kihisia yaliyomo katika ulimwengu unaotuzunguka. Kisha huwa tunajikuta tunaipoteza njia yetu, tunasahau kwamba hii hatua tulimo ni jaribio tu, na tunapoteza mwisho wetu wa kile kilicho cha muhimu zaidi. Maisha hubaki kuwa ya kuchanganyikiwa pamoja na miiba na tanzi ambazo huturudisha kwenye presha/shinikizo mbali sana na wokovu wa kweli katika Yesu Kristo.

Suluhisho pekee la hali hii ni Roho Mtakatifu aliyetumwa toka mbinguni, ambaye hupenya anga, anayebeba nguvu kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Uamsho wa kweli ni jambo lisilo la kawaida la mtembeo wa Mungu ambao hulishikilia kanisa na kulieneza katika jamii inayolizunguka pamoja na ushuhuda unaopenya na uwepo wa nguvu zake unaogusa kuhusu dhambi. Uamsho unapokuwepo

utauhisi zaidi kuliko kuufahamu tu, bali pia ni halisi kuliko kitu kingine ulichowahi kuwa na uzoefu nacho.

Shimo kubwa lililopo kati ya Dunia na umilele huondoka na hakuna jambo jingine utakalojishughulisha nalo ila umilele.

Pasipo nuru angavu, inayong'ara kutuonyesha kwenye uelekeo wa kweli wa maisha, tunaweza tu kurukia gizani. Ni uamsho pekee wa kweli wa Roho Mtakatifu ndio unaoweza kuwasha huo moto tena na kuzifanya nyumba zetu zenye taa kumulika kwenye njia isongayo wokovuni. Yesu alisema kwamba kama angenyanyuliwa, angewavuta watu wote kwake. Kwamba, hakuna namna nyingine, hiki ndicho uamsho unamaanisha.

Kuna wakati unakuja kwa ajili ya uamsho mwingine mkubwa. Yesu Kristo atarudi tena ulimwenguni wakati wowote, lakini kabla hajarudi, Biblia inatwambia kutakuwa na uamsho mwingine mmoja mkubwa, uamsho mkubwa zaidi kuliko wowote uliowahi kutokea. Hata hivyo, uamsho hauwezi kutokea bila kulipa gharama, na ni kuhusu hiyo gharama kitabu hiki kinazungumzia.

Mioto yote lazima iwashwe kwa kiberiti. Maombi yangu ni kwamba kitabu hiki kiwe kiberiti cha kukusaidia kulipua uamsho mkubwa ambao utawaka ulimwenguni mwote.

# Sura ya 1

## Kujirudiarudia kwa Ukengeufu na Uamsho

Nyakati za ukengeufu (hali ya kurudi nyuma kiroho) ambapo kanisa hushindwa kuwa na mahusiano ya karibu na Mungu na nyakati za uamsho ambapo tunaungana naye ni matukio yanayojirudia-rudia katika historia, tangu nyuma kabisa katika nyakati za Yoshua kwenye Agano la Kale. Wakati wowote panapokuwa na mtembeo mkubwa wa Mungu, kanisa hutiwa nguvu na kuchangamka na huwa sehemu inayochochea maisha ya watu wake. Furaha na fadhili ni ishara katika nyakati hizo. Mafanikio na kuinuliwa kimaisha huwa haitokei kwa kanisa lenyewe peke yake bali pia kwa jamii nzima inayolizunguka. Hizi huwa ni nyakati za ajabu!

Lakini hata hivyo, baada ya muda mfupi, mg’ao huanza kufifia na baraka za ajabu zitokanazo na watu kutembea katika Roho huanza kutolewa kama msaada na kufanyiwa biashara kama kivutio mbadala cha kile dunia inatoa. Shabaha yetu polepole huanza kuhama kutoka kwenye umilele kwenda kwenye mambo ya muda tu, kutoka kwenye kuthamini nafsi zetu kwenda kwenye tamaa za mwili, kutoka kwenye ahadi za mambo yasiyoonekana kwenda kwenye kuyatukuza mambo yanayoonekana. Wokovu na dini huanza kuzaa neema iliyo rahisi rahisi tu, ambayo haiingilii kati maisha yetu na isiyotaka utakatifu.

Njia maarufu za kidunia huonekana kuwa na maana zaidi kwetu na rahisi kuzifuata. Hatimaye, tunashangazwa, kwa nini tuvumilie mateso wakati Yesu aliteseka badala yetu msalabani?! Dini ndiyo hujengwa, hunawilishwa, na kuingizwa kwenye jamii ambayo haitaweza tena kuhisi kushurutishwa kwa kupewa changamoto. Mateso ambayo hapo kwanza yaliwasha moto wa uamsho ambao ulizaa madhehebu yetu yaliyo mengi sasa yamepuuzwa na hayaonekani tena kuwa muhimu. Tunajiona tumefika mwisho wa safari na tumeridhika.

Gharama isipolipwa, Ukristo wa kweli hautaonekana kuwa na thamani, na ni rahisi kama ilivyo kwa vitu vingine, huwa rahisi kuutupilia mbali. Kadiri moto wa uamsho unavyozimika, bado kanisa hubaki na umbo na muundo wake wa nje, lakini hupoteza moyo wake wa ndani. Sasa kanisa hujali zaidi kuhudhuria ibada za Jumapili badala ya kupanda mahusiano ya karibu na Yesu na kuwaokoa waliopotea.

Uamsho ndio mapigo ya moyo wa Mungu na kuwaokoa waliopotea ni mapigo ya moyo wa uamsho. Yesu hakufa ili tuwe na dini na mafanikio maishani bali ili tukue katika yeye na kuwa nuru ya kuwaokoa waliopotea. Ikiwa tutasahau kuhusu hilo, tutakosa maana nzima ya msalaba. Shabaha yetu itahamia kutoka kwenye kuwafikiria wengine kwenda kujijali sisi wenyewe, na kwa polepole mshumaa wetu utaanza

kufifia kadiri Roho wa Mungu ambaye hapo kwanza aliongoza makanisa yetu anatakavyokuwa akizimika.

Mara nyingi watu hukosea kuhusu nini ni uamsho. Wengi hufikiri kwamba moyo wa uamsho ni ile hisia tunayokuwanayo pale Roho wa Mungu anapotiririka kupitia sisi au msisimko tunaohisi tunapoona miujiza na udhihirisho wa mambo yasiyo ya kawaida ya Roho. Picha ambayo hukaa ndani ya akili zetu ni kuona kuna makanisa makubwa ya watu wengi wakiinua mikono yao, wakiimba na kumsifu Mungu kadiri Roho Mtakatifu anavyomwagika kama asali juu ya kila mmoja wao. Lakini huu ndio moyo mkuu wa kweli wa uamsho: uamsho unahusu kuokoa nafsi zilizopotea. Hili ndilo kusudi lote na moyo wa uamsho.

Tunapovutiwa sana na jinsi gani tutajihisi vizuri katika Roho Mtakatifu ndipo tutapoteza shauku yetu kwa ajili ya nafsi zilizopotea, tutaishia tu na kuizimisha nia ya Roho. Kabla hatujaendelea, huwa hatubaki na kitu bali kanisa na mfano wa utauwa tu. Mara chache huwa tunagundua kupungukiwa na kitu mpaka hali inaposhuka sana kutokana na kuvujisha kadiri tunavyotumika kwenye taasisi badala ya uvuvio. Mshumaa wetu polepole huondoka (Ufunuo 2:5) na hatimaye huwa tunajikuta tunatumikia ulimwengu wa giza mpaka tunakuwa hatuwezi tena kuiona kweli.

Kwenye nyakati hizi, daima Mungu huwatuma manabii wake kutuita kwenye toba. Kazi ya nabii siyo kuwa msomaji wa sahani ya jiwe lililochorwa

akitwambia kuhusu mambo ya baadaye, bali kuwaita watu wa Mungu kwenye toba. Ni kazi ambayo hakuna atakayeikubali, aidha kwa anayeitwa nabii wala kwa wale alioitwa kuwatabiria. Ujumbe wa kweli wa nabii mara chache huambatana na habari zinazoendelea sasa bali pia umebuniwa na Mungu kusababisha mateso na huzuni kwa maana una mzizi wake kwenye msingi wa kukemea matendo yaliyokufa. Matokeo yake, manabii mara nyingi aidha hupuuzwa na kufukuzwa au huteswa na kuuawa.

Moja ya dalili za ukengeufu katika kanisa ni kuwatukuza manabii wa "amani na mafanikio." Kama magugu, huchipuka kutoka kwenye historia iliyozikwa na kuweka mzizi wake kwenye mambo ya kidunia yaliyomo kanisani. Manabii wa uongo hawatuiti kwenye toba; hutuita kwenye kuridhika. Kamwe unabii wao haujawahi kukosolewa; mara nyingi tu hutoa ahadi za amani na mafanikio. Kamwe hawatuelekezi kwenye hofu ya Mungu bali hutuzamisha kwenye injili inayopendwa ambayo hutiririsha uongo wake wa amani na upendo.

Tatizo ni kwamba, ufafanuzi wao kuhusu upendo wa Mungu ni mdogo sana kuliko maonyo, hofu, na "mahusiano" ya raha na Mungu ambaye ni "Baba" yetu. Neno la Mungu, hata hivyo, hufafanua upendo wa Mungu kama kuzitunza amri zake (Yohana 14:15; 15:10; 1 Yohana 5:2-3), ambao hutokana na kumcha Bwana. Lakini wakiwa kama sambusa, manabii hawa wa uongo

hucheza sauti ambayo masikio mengi kanisani hupenda kuisikia, na hutuingizia maono ya tunda lenye sukari, badala ya tunda la toba.

Mara nyingi manabii wa kweli hawakubaliki katika nyakati zao, lakini mbegu wanazopanda huanguka kwenye udongo mzuri kwenye kizazi cha baadaye. Nabii Yoeli alizielezea hizi nafsi zenye njaa kama wanyama ambao wanatafuta malisho lakini hawayapati (Yoeli 1:18). Katika kuitafuta kwao Kweli, kizazi hiki cha baadaye huyatukuza maneno ya hao manabii wa kweli ambao mababa zao waliwakataa. Hayo maneno yao hupiga kelele ya kweli katika nafsi zao na huanza kukua ndani ya mioyo yao kuwatia moyo kufika kwenye matumani kwa ajili ya Mungu anayetiririka, mpya kila siku.

Gideoni alipepeta ngano yake kwa siri kwenye shinikizo—ngano ikiwa kama alama ya Chakula cha Uzima na shinikizo kama alama ya maombi—na hivi ndivyo ilivyo kwa hawa watu wanaomtafuta Mungu. Wanaitafuta kweli ya Mungu nje ya mifumo ya liturujia za kanisa zilizowekwa ambazo zimekomaa isivyo kawaida na zimekengeuka. Kama Gideoni, kizazi cha baadaye huhisi kwanza mifumo ya dini zilizopo kuwa haziwezi tena kujibu mahitaji ya mioyo yao na kitaanza kutafuta kitu kilicho kikubwa kuliko mababa zao walichowaachia.

Hivyo basi, mzunguko wa ukengeufu na uamsho hujirudia, tena na tena. Je huu ni muundo wa Mungu au

kushindwa kwa watu wenye mwili? Mimi sina jibu la swali hili, bali mimi ninachojua ni kwamba kama Yesu alivyokuwa "mzizi katika nchi kavu" (Isaya 53:2) ndipo mavuno mengi yalitokea baada ya nyakati zake za ukame wa kiroho.

Kanisa liko kwenye wakati kama huo na ni sasa. Tuko tayari kwa mvua na wakati unaofuata wa mavuno. Hata hivyo, wakati huu umwagiko wa Roho Mtakatifu wa Mungu utakuwa mkubwa kuliko uamsho wa nyakati zilizopita. Kadiri tunavyopitia hali ya ukame wa kiroho ambao manabii Yoeli na Amosi wote walitabiri kwamba ungekuja kabla ya kurudi kwa Bwana Yesu Kristo, uamsho mkubwa sana kuliko siku zote umepangwa kutokea.

# Sura ya 2

# Uamsho Mkubwa Kuliko Siku Zote

Ahadi ya Mungu ni hii: kama tutautafuta uso wake na kujinyenyekesha, kwa toba ya kweli, yeye atatujibu, atasikia na kuiponya nchi, naye atatuonyesha mambo makubwa, magumu tusiyoyajua ([2 Nyakati 7:14] Yeremia 33:3). Mungu anataka uamsho ufanyike zaidi ya tunavyofanya sasa. Nabii Yoeli ametuonyesha moyo wa Mungu ulivyo kwetu:

> *"Bwana akajibu, akawaambia watu wake; Tazameni, nitawaletea nafaka, na divai, na mafuta, nanyi mtashiba kwa vitu hivyo…*
>
> *Ee nchi, usiogope; furahi na kushangilia; kwa kuwa Bwana ametenda mambo makuu. Usiogope, enyi wanyama wa kondeni; maana malisho ya jangwani yanatoa miche, na huo mti unazaa matunda yake, mtini na mzabibu inatoa nguvu zake. (Yoeli 2:19,21-22)*

Hata hivyo, kwenye sura ya kwanza ya Yoeli, Mungu aliondoa kanisani masuke au ngano (Neno la Mungu), divai (Roho), na mafuta (upako wa Roho Mtakatifu) kama hukumu kwa sababu kanisa liliacha mavuno ya nafsi yapotee. Hukumu zimebuniwa siyo tu kama adhabu ya dhambi bali pia kama wito kwenye haki. Lakini kwenye hii sura ya pili ya Yoeli, Mungu

anaahidi kurudisha ngano, divai, na mafuta ambayo yaliondolewa katika nyumba ya Mungu ikiwa tutatubu na kumwita kwa ajili ya rehema na urejesho.

Ngano inawakilisha Neno la Mungu, yaani Chakula cha Uzima. Neno linapoondoka kwetu, husababisha kutengwa na Mungu na kutufanya tusiijue siri, hazina zilizofichwa katika Neno ambazo Roho tu ndiye huzichunguza na kuzifunua. Fikiria kuhusu huu utajiri tulioupoteza kwa sababu hatujatembea kwa kina katika kuwa na ushirika pamoja na Mungu! Bali sasa fikiria hamasa ya kujionea mto wa hekima ambao utadhihirishwa ikiwa tutaogelea ndani ya Neno la Mungu. "Imani huja kwa kusikia, na kusikia huja kwa Neno la Kristo," lakini kwa sababu masikio yetu yamezibwa na maisha yetu ya kidunia, imani yetu imekuwa haba sana. Sasa, hata hivyo, masikio yetu yatasikia, na imani yetu itapanda juu hadi viwango vingine ambavyo vitadhihirisha mambo yasiyo ya kawaida katika maisha yetu na maisha ya wale tunaowagusa.

Divai ya Mungu ni ule ushirika wa kina wa kiroho pamoja na Roho wa Mungu kupitia maombi. Mababa zetu wa imani waliweza kuzama kwenye maombi kwa machozi kwa masaa mengi, hata kukesha usiku wakiwa pamoja na Mungu. Wengi wa hawa watu waliweza kuomba kwa namna hiyo si kwa sababu walikuwa na uwezo mkubwa wa kuchagua au waliishi kwa nidhamu kubwa. Hapana, inachukua upako na nguvu kutoka

kwa Mungu ili kuomba kwa kiwango hicho kikubwa na kipana. Roho wa Mungu aliwapa uchaguzi na nia ya kusukuma nje vikwazo vya kiakili na mwili ili kuingia kwenye mchuano wa maombi kwa kiwango hicho. Uchaguzi huo kwa kiwango kikubwa umepotea katika kanisa la sasa, lakini Mungu anasema atauleta tena.

Msisimko wa mpenyo hadi kwenye chumba cha kiti cha enzi cha Mungu baada ya maombi ya nguvu ya mchuano kama hayo ni kama hakuna kitu unachoweza kukiona kwa kuwa na "mazungumzo na Yesu." Bali itakupatia ushindi na furaha ambayo itachochea kutembea kwako na Mungu. Sasa utatembea ukiwakanyaga pamoja naye mtawala ili kuangusha kuta zote za adui. Uhakika unaoweza kuwa nao kwenye maombi yaliyojibiwa haushindwi na vikwazo, na hata milima utaing'oa na kuitupa baharini kwa sababu sasa una imani kwa Mungu. Hii ni kwa sababu umekuwa kwenye uwepo wake na mitazamo ya uhalisia wa hii dunia sasa imeshaondolewa kwako. Unaweza hata kulisimamisha jua lisisogee, kuzuia mvua isinyeshe, kushusha moto kutoka juu, na kuita mvua ya baadaye ya uamsho.

Mafuta ya upako ya Roho Mtakatifu ambayo Yoeli aliyasema kwamba Mungu atayarejesha yamekosekana kwa muda mrefu hata hatujui tumepungukiwa na nini. Matokeo yake, tumeridhika na mahubiri makavu, mafundisho ya kimaadili, na kanisa lenye muundo usio na uhai. Badala yake tumejishawishi sisi wenyewe

kwamba jibu liko kwenye kuwa msomi wa elimu ya Mungu na kwamba wale wenye digrii za elimu ndio watatutosheleza. Mwandishi wa vitabu na mwanauamsho wa karne ya ishirini, Leonard Ravenhill alisema kwamba mwanzoni tulikuwa na wahubiri wasio na digrii bali wenye mioyo mingi, lakini sasa tuna wahubiri wenye digrii nyingi zisizo na moto.

Upako ambao umekosekana utaanza tena kumwagika na uzima utaingia tena katika kanisa. Fikiria kuhamasika sana juu ya ujumbe ambao usingeweza kuusubiria kwamba utarejea kwenye ibada za kanisani, ili kwamba ujumbe wa Jumapili tu usitutosheleze. Sasa unapaswa kuwemo kanisani kila siku ili kuusubiria. Utamweleza kila mtu ukutanaye naye kuhusu jinsi ujumbe huo ulivyo mzuri! Nafsi zenye njaa hatimaye zitaokolewa, siyo kwa sababu ya mafundisho yetu wala imani, bali kwa sababu wanaweza kuuona moto kwenye macho yetu. Nabii Isaya alisema "hata Roho atakapomwagwa juu yetu kutoka juu" (Isaya 32:15). Hivi ndivyo ilivyo; uamsho huu ni umwagiko kutoka juu ambao Isaya aliuzungumzia. Huu ni uamsho.

Mti wa mtini na mzabibu itatoa nguvu zake tena, na kama kinywaji kinachotiririka kupitia sisi, tutazaa matunda mengi na kamwe hatutakatwa tena. Mvua ambayo itanyesha italeta tena uzima jangwani. Lakini siyo mvua tu, kwa kuwa Bwana Mungu atanyesha ile mvua ya kwanza *na* mvua ya baadaye kwa pamoja:

> *Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa yeye huwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli kama kwanza. (Yoeli 2:23)*

Yoeli 2:23 ni msitari wa ufunguo ambao unatabiri kuhusu huu uamsho unaokuja kwenye hizi siku za mwisho. Baada ya wito wa Yoeli kwenye sura yake ya pili kwa ajili ya kanisa kutubu, kisha anawaita kufurahi. Mara tu baada ya kanisa kutubu na kulia mbele za Mungu kwa unyenyekevu na upendo kwake, njia hufunguka kwa ajili ya Roho Mtakatifu kumwagika juu yake. Sasa Mungu anaweza kummwaga "Roho juu yetu kutoka juu" kama anavyoahidi kwenye Isaya 32:15.

Yoeli anasema kwamba Mungu amekwishatunyeshea "mvua ya vuli." Hii "mvua ya vuli" ni nini? Hii inaweza kuwa ni ile Pentekoste iliyokwishatokea! Lakini Mungu anakwenda kuleta siyo tu mvua ya kwanza [vuli] kama ilivyokuwa Siku ya Pentekoste, bali ataleta mvua ya kwanza [vuli] na mvua ya baadaye [masika] kwa pamoja. Ndugu, haitakwenda kunyesha pekee; bali itamwagika! Siku ya Pentekoste ya pili inakuja katika kanisa ambayo itakuwa kubwa sana kuliko ile ya kwanza.

Mvua ni alama muhimu ya uamsho. Baada ya moto kushuka juu ya dhabihu iliyokuwa kwenye kilele cha

Mlima Karmeli, Eliya alimwambia Ahabu, "Haya! Inuka, ule, unywe; kwani pana sauti ya mvua tele." (1 Wafalme 18:41). Hiyo sauti ni sauti ya maombi ya watakatifu ikipanda kwenda mbinguni, ikilia Mungu aokoe watu. Unaposikia sauti hiyo, mvua huwa haiko mbali. Uamsho huu unaokuja utachochewa na kutahayarika kwanza kuhusu Mungu kutusamehe, kuturejesha, na kuokoa nafsi tutakazokuwa tumezipuuza. Itakuwa ni sauti yenye nguvu. Na jibu litakuwa ni umwagiko wa mvua ambayo haijawahi kutokea kabla ambayo itashuka kwenye huu uamsho mkubwa wa mwisho.

Sambamba na mvua, Yoeli alisema kwamba, "Na sakafu za kupepetea zitajaa ngano." (Yoeli 2:24).

Sakafu zipi zitajaa ngano? Sakafu za kupepetea za makanisa yetu! Nafsi ni mavuno, kama Yesu alivyosema kwa wanafunzi wake, na mavuno huletwa kwenye sakafu ya kupepetea ambapo ngano hupepetwa na makapi kutenganishwa. Kazi ya kanisa ni kuzalisha nafaka safi isiyo na makapi. Hizi sakafu hazitajazwa nusu wala kukaribia kujaa; zitajazwa kikamilifu na nafsi zinazokuja kumwomba Yesu Kristo ili awe Mwokozi wao kibinafsi. Madhabahu zitazajwa, viti/mabenchi yatajazwa, na mara moja zaidi, kutakuwa na chumba cha kusimama tu kadiri watu watakavyokuja kwa Mungu, wakifa ili waokolewe na kuhuishwa.

*Na mashinikizo yatafurika kwa divai na mafuta. (Yoeli 2:24b)*

Siyo tu divai na mafuta vitakuwa vingi, bali vitafurika! Roho wa Mungu atatuzidi uwezo wetu wa kujiachilia kwenye sifa. Ni watu wachache leo ndio wanaofahamu inafananaje Roho wa Mungu kumwagika juu yako kwa wingi hadi unajiachilia mwenyewe ndani yake. Hautaweza kusimama, hautaweza kuketi, hautaweza kufikiri, na hautaweza kuongea chochote bali kumsifu Mungu tu. Utalewa Roho. Hata ile hewa muhimu itatokea kwenye utukufu wa Mungu.

Panua kufikiria kwako kadiri uwezavyo, lakini mambo ambayo Mungu atatenda bado yatakuwa yenye kushangaza macho yako. Atafanya mambo ambayo kamwe hujawahi kuyaona wala kuyafikiria. Uamsho huu utakuwa wenye thamani isiyo ya kawaida… na wa kushangaza:

*Nanyi mtakula chakula tele, na kushiba, na kulihimidi jina la Bwana, Mungu wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu na watu wangu hawatatahayari kamwe. (Yoel 2:26)*

Atarejesha miaka iliyopotea. Atainua mifupa mikavu bondeni (Ezekieli 37). Atamrejesha bibi-harusi wake wa thamani na kumwita tena amrudie kwenye upendo mkuu kuliko siku zote.

# Sura ya 3

# Kanuni Sita za Uamsho

Kabla hatujaona hatua ambazo kanisa linataka kuzifuata kwa ajili ya umwagiko wa Roho wa Mungu, ningependa kujadili kanuni sita ambazo ni za muhimu katika kuelewa kama kweli tunamtegemea Mungu katika kusonga. Niliziona kanuni hizi hizi kazini kwenye kila uamsho katika historia. Kanuni zinahitaji kuzifanyia kazi ndani ya mtazamo wa waamini na makusudio ya mioyo yao, lazima zipewe nafasi kabla ya uamsho wowote utakaopenya. Pasipo hizi kanuni kutuongoza, hakuna tufanyacho kitakachofanya kazi.

## 1. Uamsho Unahusu Kuwaokoa Waliopotea

Kanuni ya kwanza ya uamsho ni kuelewa kwamba uamsho hauhusiani na jinsi gani unajisikia vizuri, jinsi gani huduma zako zinavutia, wala baraka ngapi za ajabu umepokea. Uamsho unahusu kuwaokoa waliopotea—ndio jambo la kwanza, la kwanza kabisa, na la daima. Sababu kuu Mungu huleta uamsho ni kwamba kanisa liinuke na kuangaza nuru ya wokovu kwa mamilioni ya nafsi zilizopotea zilizoko njiani kuelekea jehanamu.

Ili kanisa liangaze hiyo nuru kwa ufanisi, ujumbe wa Injili lazima ufikishwe kwa nguvu, nguvu ya kweli, kutoka kwa Mungu. Kama hakuna nguvu kwenye

ujumbe wetu, kadhalika hakutakuwa na kutofautisha kanisa na dunia, na kama hatutofautiani na dunia, basi chumvi yetu itakuwa imepoteza ladha yake na nafsi zilizopotea zitatafuta mahali pengine kwa ajili ya kutosheleza mahitaji muhimu zinayoyatafuta kwa ajili yao.

Jambo hili siyo kitu kinachoweza kuja kutoka kwenye hotuba ya elimu ya kimwili. Linapaswa litokane na Roho wa Mungu, vinginevyo halitafanya kazi. Katika kuwaandikia Wakorintho, kwa ujasiri Paulo alihubiri kwamba hakwenda kwao kuhubiri "kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yao isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu." (1 Wakorintho 2:1,4-5)

Kwa kurudiwa rudiwa, kwenye Agano Jipya, tumeambiwa kuhusu nguvu ya Mungu kwenye wokovu. Bila hiyo nguvu, ujumbe wetu wa Injili si kitu bali falsafa nyingine ya maisha, mawazo ya mtu fulani kuhusu Mungu, na utakuwa haubebi chochote isipokuwa "mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu zake." Maonyo kutoka kwa Paulo yanafuata: "hao nao ujiepushe nao." (2 Timotheo 3:5). Mungu huleta uamsho ili kanisa liwashe moto mtakatifu na kuonekana kwa mwangaza na nguvu ya Mungu yenye kutuweka huru kwenye wokovu. Moto huo unapowaka, nafsi huja na kugundua tofauti iliyopo kati ya kile Injili inatoa na kile ulimwengu unatoa, na ndipo waliopotea wanaweza

kupandikiza matumaini yao kwenye Kweli na mambo yasiyoonekana—mambo yatarajiwayo.

## 2. Injili Haikuhusu Wewe Uliyeokoka

Kanuni ya pili ambayo kanisa linatakiwa kuishika ili kuona uamsho ni kwamba Injili ya Yesu Kristo haikuhusu wewe; inawahusu wasioamini. Hata hivyo, jumbe nyingi nisikiazo leo kutoka mimbarini, vitabuni na wainjilisti redioni, huzingatia juu ya nini Mungu anaweza kufanya kwa ajili yako, jinsi gani Mungu anataka kukubariki na kukufanikisha wewe, na jinsi ambavyo ahadi ni zako kuzipokea.

Hata mimi niko tayari kubarikiwa na Mungu kabisa, lakini siyo sababu kuu ambayo Yesu aliifia msalabani, siyo njia ya mateso ya mwili wa Kristo iliyosulubiwa ambayo tumeitwa kuipitia. Anatuita tujikane nafsi zetu wenyewe kama kweli tunataka kumfuata:

> *Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha [atakayeiokoa]. (Luka 9:23-24)*

Yesu hakufa ili kutufanya matajiri. Yesu alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi wasiende jehanamu, na

anatuita tumfuate katika wito huo huo katika kutimiza Agizo Kuu kwa kuhubiri Injili na kufanya wanafunzi. Huu ni ujumbe wa Kalvari. Hivi ndivyo upendo ulivyo. Kama huwezi kushika wazo hili, kamwe hautauelewa msalaba.

Mpaka waamini watakapoacha kujithamini wao wenyewe, ndipo Mungu ataleta uamsho. Mungu anahitaji wachungaji ambao watayatoa maisha yao kwa ajili ya kondoo kabla hajawaletea zile nafsi za thamani.

## 3. Kila Jambo katika Mungu Lina Gharama Yake

Kanuni ya tatu ya kuielewa ni kwamba hakuna jambo katika Mungu lililo bure [isipokuwa neema]. Kila jambo lina gharama. Na gharama ya uamsho ni kubwa, kubwa sana, kwa kweli, ambayo naamini ndio sababu kwa nini uamsho wa Roho wa kweli ni nadra sana. Ni watu wachache walio tayari kulipa gharama hiyo, hasa kwa ajili ya watu ambao hata hawawajui [watu waliopotea]. Mungu anataka kukupa mzigo mkubwa kwa ajili ya waliopotea ili uzae namna ya kujitoa ambayo humtawala mtu hadi kufikia kiwango cha kufunga, kuomba, na kujitoa dhabihu ambayo inahitajika kwa ajili ya uamsho wowote.

Kazi ya kweli ya kiroho inahusisha zaidi ya kuwekeza muda wako, kama ilivyo kwa mtu afanyaye kazi ya kila siku. Inahitaji hali ya kupondeka moyoni ambayo itaendesha shauku yako hadi kiwango cha kuwaka moto ambao utaangusha kila ukuta na kuvunja

kila kikwazo kinachosimama kwenye njia ya maombi yako hadi yafike juu kwenye kiti cha enzi cha Mungu na kutimiza misheni yako. Hali hii siyo suala ya kukutana na Mungu bila kutegemea, bali ni vita ambayo lazima uwe umekwishaipanga dhidi ya mwili na chochote cha kimwili kinachosimama njiani mwa maombi yako. Lazima utafute uamsho kwa moyo wako wote ili kulipa aina hii ya gharama.

Jambo la kushangaza ni kwamba, kama utamwomba Mungu akupe huu mzigo, atakupa. Lakini ni juu yako kuutafuta kutoka kwake. Siyo wa bure. Huwezi kutegemea kwamba ukae tu kanisani bila kufanya jambo, bali mwache Mungu adondoshe uamsho kwenye viganja vyako vinavyosubiri kupokea kitu. Lakini haitatokea bila kufanya jambo. Kwenye hatua fulani, utahitajika kuinuka na <u>kufanya</u> kitu. Huwezi kukaa tu kanisani. Kama methali ya zamani isemavyo, "Kama utaendelea kufanya mambo uliyokwishayafanya, ndivyo utakavyopokea vitu ulivyonavyo tayari. Kama unataka kitu cha tofauti, unapaswa kufanya jambo tofauti. Na kama usipofanya kabisa, hakuna kitakachotokea." "Imani bila matendo imekufa nafsini mwake." Kuna gharama ya kulipa ili kupokea uamsho.

## 4. Hakuna Uamsho Utakaokuja Bila Toba

Kanuni ya nne ya uamsho ni kwamba hakuna uamsho utakaokuja bila toba, aidha katika ushirika au

kibinafsi. Nitaizungumzia hii kanuni kwa kina baadaye, lakini nitaisema hapa kwa ujumla wake, kama makanisa yetu yangekuwa kwenye nafasi yanayotakiwa kuwa, yangekuwa tayari yana Roho wa Mungu akimwagika juu yake na yasingehitaji kuamshwa. Toba hutubadilisha. Wengine wanaweza kusema kwamba kuna nyakati ambapo kanisa linajishusha sana na linaona siyo lazima lihitaji kutubu, lakini mimi sijakubaliana nao. Roho wa Bwana anapotembea, kuna hamasa, na nafsi huokolewa. Lakini Mungu ni mtakatifu na hawezi kutembea kupitia chombo kichafu, aidha kiwe ni kanisa au mtu. Njia pekee ya kusafisha chombo ili Mungu atembee ndani yake ni kupitia toba.

Chochote ambacho kimekuwa kikizuia uamsho ndani ya mtu au kanisa lazima kiondolewe. Kanuni zile zile za Agano la Kale zinazohusiana na ukoma katika nyumba ya kimwili ndizo zinatumika kwenye ukoma wa kiroho katika nyumba ya Mungu. Ikiwa ukoma ulionekana katika nyumba, kila kitu kiliwekwa nje, kuta zilisuguliwa na kusafishwa, na nyumba ikaachwa ipone. Kama baada ya usafi huo ukoma ungeendelea kuenea, ndipo watu wa nyumba nzima wangepigwa kwa mawe na kutupwa nje ya kambi. Toba hulisafisha kanisa kwa njia hiyo hiyo. Kama tutatubu, Mungu atatembea kati yetu. Kama hatutubu, au kama toba yetu isipokamilika, kanisa na kila kitu kilichomo ndani yake vitaendelea kuwa na huo ukoma wa kiroho na hivyo vitatupwa nje ya kambi ya kiroho.

Nini tunahitaji kukitubu? Tunaweza kuanza na ukosefu wetu wa utakatifu, ukosefu wetu wa shauku ya kuutafuta uso wa Mungu, lakini lililo kubwa zaidi, ukosefu wetu wa kubeba mzigo wa kuokoa nafsi kwa ajili ya Kristo. Amosi sura ya 6 inawataja wale waliomo katika kanisa ambao "wanastarehe katika Sayuni." Wanakaa na kufurahia mambo yote maishani, lakini "hawahuzuniki kwa sababu ya mateso ya Yusufu." Kwa maneno mengine, wanajali tu kuhusu wao wenyewe na hawana huzuni kwamba kuna nafsi zinashuka jehanamu kila dakika ya kila siku. Hukumu inayowaangukia ni kwamba watakwenda matekani [uhamishoni] pamoja na wale walio wa kwanza kabisa kwenda matekani. Kwa nini? Kwa sababu hukumu huanza katika nyumba ya Mungu.

Dhambi yetu kubwa ni kwamba "tumeacha mavuno yapotee" na hatujali kuhusu hilo. Bila toba, baadaye hatutahukumiwa tu bali pia itazuia ule uamsho ambao Mungu anapenda kuuleta.

## 5. Kila Uamsho Lazima Uombewe

Hakuna njia nyingine ya kuleta mtembeo wa Mungu. Maombi humtembeza Mungu. Ikiwa unataka Mungu alete uamsho, unatakiwa kuuombea. Ni rahisi namna hiyo. Mambo yote megine ambayo ungefanya katika maisha yako ya Kikristo yatakuathiri wewe au wale wanaokuzunguka, lakini maombi humtembeza Mungu. Chunguza historia na utaona kwamba kabla ya

mtembeo wowote muhimu wa Mungu kutokea, huwa kuna kundi la watu ambao kila kitu kwao kimeshapangwa tayari, wakipambana kwenye maombi. Siku zote hawa ni watu wachache, lakini mara nyingi hufanya mapambano ya kushikamana pamoja na kukataa kupokea jibu la "hapana" kwenye maombi.

Mara moja nilimwuliza rafiki kwa nini ilikuwa ni vigumu sana kwetu kusoma Biblia na kuomba. Alinijibu, "Hilo ni rahisi. Kwa sababu ni muhimu sana." Hivyo ndivyo ilivyo. Kusoma Biblia pamoja na kufunga na kuomba ni dhana zenye ufanisi tulizopewa kufanikisha kazi za Mungu na ni silaha tulizopewa kuzitumia kupigana na nguvu za giza. Haishangazi kwamba Shetani huvamia haya mambo matatu kwa bidii kuliko kitu kingine katika maisha yetu ya Kikristo. Anafahamu nguvu tulizonazo katika mambo hayo na hufikiria kutukatisha tamaa katika kujifunza jinsi yalivyo na nguvu. Kwa kusoma Biblia, kuomba, na kufunga, tunaweza kabisa kuubadilisha ulimwengu.

Uvamizi mkuu wa Shetani ni kuwazuia waamini wasiombe wala kusoma Biblia. Hasa hasa anachotaka ni kutuzuia tusifikie kiwango/ujazo kamili wa mambo hayo. Kama ataweza kutufanya tutosheke na kipande cha mkate, kamwe hatutaingia kwenye karamu [sherehe ya chakula] ya Bwana. Kuwaombea vibaya maadui na maombi ya kulalamika hayatahamisha milima. Kamwe hayatapenya vikwazo vyovyote mpaka mbinguni na kukiona kiti cha enzi cha Mungu. Ndiyo, ni kweli

kwamba Mungu anaweza kusikia hata kilio cha moyo kilicho hafifu, na wengi hutumia hiyo hoja kuzama kwenye wakati wa kutafakari ambao hauwezi kusikilika juu ya dari la chumba kwa sababu huwa hakuna sauti kwenye maombi ya namna hiyo. Siyo kuhusu moja ya kumi unayoifikia kwenye maombi; ni kuhusu kiwango cha shauku na kutahayarika. Yakobo, kwa kumtumia Eliya kama mfano kuhusu ufanisi wa shauku kwenye maombi, aliandika, "…kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii" (Yakobo 5:16). Kwa maneno mengine, kama unataka kuona mvua ya uamsho ikishuka juu yetu, unatakiwa kwenda kuomba kama Eliya.

Kina na kiwango cha maombi kinachohitajika kuombea uamsho viko juu kuliko ambavyo Wakristo wa kawaida wanaweza kuomba katika wakati wowote. Hata hivyo, historia inatuonyesha kwamba, Mungu hutaka miaka ya kutosha kwa watakatifu kumwomba kwa shauku kwa ajili ya uamsho kabla hajaanza kuitikisa dunia. Lakini mioyo ya waamini waliokata tamaa inapoponywa na kuzoeshwa kuamini kupokea siyo kitu kingine bali ushindi, maombi yao yatamfanya Mungu ashuke. Hakuna kitu kingine kitakachofanya hilo litokee. Mfano mkubwa wa namna hiyo ya maombi ni kama kile tulichokiona kwa Peggy na Christine Smith kutoka huduma ya uamsho ya Hebrides Revival. Peggy na Christine walikuwa ni wanawake wazee, wenye umri wa miaka 82 na 84, waliokuwa na njaa ya

kumtembeza Mungu na waliwajibika hata wakafungua mlango wa uamsho mkubwa katika visiwa vya Hebrides. Peggy alikuwa kipofu na dada yake Christine alikuwa na uvimbe uliomsababishia kuwa na kilema. Hawakuweza kuhudhuria mikutano ya hadharani, nyumbani mwao tu ndimo palikuwa hema yao ya kukutana na Mungu ambaye aliwapa ahadi: "Nitamimina maji juu yake aliye na kiu na mafuriko juu ya nchi yenye ukame."

Uvumilivu wao kwenye maombi ulipasua nchi kwa kuleta uamsho mkubwa ambao ulikuwa haujawahi kuonekana. Wanawake wawili wazee, mlemavu na kipofu, waliweza kumfanya Mungu atembee kwa namna iliyotukuka. Hapa kuna nukuu kutoka kwao ambayo inaonyesha walikuwa na roho ya namna gani na aina gani ya vita vikubwa walivyoviweka kwenye chumba cha maombi.

> *"Tulipambana wakati wa masaa ya usiku, tukikataa kupokea jibu la 'Hapana.' Je Mungu hakutuahidi? Na hatatimiza? Mungu wetu ni Mungu anayetunza maagano, na lazima awe mkweli kwenye mpango wa agano lake.*
>
> *Je ameshawahi kushindwa kututendea? La hasha! Kabla ya asubuhi, tulimwona adui akijiondoa mwenyewe, na Mwanakondoo wetu wa ajabu akalitwaa eneo.*

*Tulikuwa na fikira kuhusu Mungu ambazo zilitujengea uhakika katika nafsi zetu ambazo zilikuwa zimekataa kukubali kushindwa."*

Kama wanawake wawili wazee waliweza kuomba namna hiyo na kutendea kazi hiyo nguvu ya Mungu, fikiria kuhusu nini tutafanya pale tutakapombeba Mungu katika Neno lake na kutendea kazi hiyo imani kwa magoti yetu. Inatumia imani kubwa kuomba katika kina cha kiwango hicho, lakini Mungu atakupatia imani hiyo kupitia Neno lake. Neno la Mungu huzalisha imani ndani yetu na hiyo imani ndiyo ambayo hutupatia nguvu ya kuomba. Kama tunahitaji uamsho, tunatakiwa kuegemea kwa Mungu ili kutuleta kwenye vita kama hivyo ambavyo hao wanawake wazee wawili viliwafanya kuzaa matunda.

## 6. Lazima Awepo Mbeba Maono

Kanuni ya sita na ya mwisho ya uamsho ni kwamba mtu mmoja lazima awe na maono ili kuliongoza kanisa kuelekea kwenye uamsho. Mtu mmoja lazima aweze kuona mbele zaidi ya upeo wa nyakati na hali ilivyo, mbele zaidi ya mazingira na uhalisia uliopo, na kuona kile Mungu alichonacho kwenye hazina yake kwa ajili ya wale walio na imani ya kuipokea. Kabla ya uamsho wowote kupenya, mwanamume au mwanamke wa Mungu mwenye maono yanayowaka atahitajika ili kuendesha safari na

kuwaongoza watu wa Mungu kwenye uamsho. Yeye atakuwa ameshauona kabla haujaja, na wote kwa pamoja watashirikishana haya maono, pamoja na imani na nia yenye kuvumilia kwa wale wanaowazunguka na kuwahamasisha kutwaa taa zao na kueneza moto.

Hawa ni wabeba maono kwa ajili ya kizazi chao. Kamwe siyo aina ya watu wa kawaida, bali daima watabaki kuwa tofauti, peke yao, na wenye kiwango kikubwa. Hupumua hewa tofauti, huona nuru tofauti, huyapokea yasiyowezekana, na wako hodari kumwamini Mungu. Wao ndio wanaozibeba taa zinazowaka moto wa uamsho kwa ajili ya kila mtu mwingine kuwafuata.

Mtu mmoja lazima auanzishe mchakato wa uamsho, na hawa wabeba maono ni watu wanaoitikia kwenye wito huo.

Yonathani alikuwa ni mfano wa mbeba maono. Kwenye 1 Samweli 14, tunamwona Yonathani na mbeba silaha wake wakiwa chini ya mlima kuwatazama Wafilisti 20 wenye misuri. Miaka miwili tu kabla ya jambo hili, baba yake na Yonathani, Mfalme Sauli, aliwashinda maadui kwa jeshi la wanaume 330,000 wapigao vita, lakini kampeni hii ilipokamilika, Sauli akawaacha kila mtu kwenda nyumbani kwake isipokuwa wanaume 3,000. Wakati wowote tunapouacha ulinzi wetu uende zake, tunampa adui nafasi ya kutuvamia, na hiki ndicho kilichotokea kwa Sauli. Adui alirudi tena akiwa na jeshi lisilo la kawaida

na kuwatesa Waisraeli. Jeshi dogo la Sauli lilishindwa na akababakiwa na wanaume 600 pekee, wasio na upanga wa vita hata mmoja.

Nini kilitokea kwenye mapanga 330,000 aliyokuwa nayo tu miaka miwili nyuma? Nini kilitokea kwenye jeshi la ushindi lililoshinda vita vikubwa namna hiyo? Tunapoacha kutazama macho yetu kwenye vita, tunapoteza kuyaona maono, na ushindi wetu huanza kuporomoka kupitia vidole vyetu vinavyotupilia mbali silaha tulizonazo.

Lakini Yonathani hakupenda kuwa kama baba yake. Maono ya Yonathani kamwe hayakupata dosari. Hao Wafilisti ishirini hawakuwa kikwazo kwake. "Kwa maana hakuna la kumzuia Bwana asiokoe, kwamba ni kwa wengi au kwamba ni kwa wachache," alisema wakati akikwea kwa mikono na magoti yake kukutana na adui. Hii ni namna sawa na jinsi tunavyotakiwa kuwajibika kwenye vita—kwa kupiga magoti mbele za Mungu—na unapaswa kumwamini kukupatia ushindi.

Haikuwa kuwashinda wanaume ishirini ndio ingeleta uamsho. Ilikuwa ina maana gani basi kuwamaliza wanaume ishirini juu ya mlima katika mamia ya maelfu ya Wafilisti? Hapana, haikuwa nguvu za Yonathani katika kupigana vita ambavyo viliwasha uamsho; ilikuwa ni imani yake kwenye maono aliyobeba ambayo Mungu angeyatumia kushinda vita. Yonathani alikuwa ni mtu wa maono, na hicho ndicho

Mungu alichokiona na jambo hilo ndilo lilileta tetemeko la ardhi ambalo lilishinda vita katika siku hiyo.

Anatakiwa kuwepo angalau mtu mmoja anayeiona njia ya ushindi, ambaye hatishwi na utisho wa adui wala ukubwa wa changamoto iliyopo. Imani yake iwe katika Mungu ambaye ana nguvu zaidi kuliko kikwazo chochote na ambaye ametuahidi kwamba yupo hapohapo kwa ajili yetu kama tutaamini katika yeye. Bila kuwa na mtu wa namna hiyo aliye na maono yaliyo wazi kwa ajili ya kile Mungu anaweza na atakachofanya, hapatakuwa na mtu mwingine yeyote kumfuata. Lazima tuwe na mbeba maono ili kutuongoza katika kazi.

# Sura ya 4

## Hatua ya 1: Kutambua

Hatua ya kwanza ya kuona uamsho ukija, kwanza ni kutambua kwamba bila kujali jinsi gani tunafikiria kanisa letu lilivyo zuri, tunahitaji kutambua kwamba sasa hatuko kwenye uamsho. Lazima tufahamu hatuko tena kwenye nafasi ya baraka ambayo tulipaswa kuwepo. Kuta zetu zimebomolewa, hekalu limeharibiwa, na makanisa yetu yametekwa na kuhamishiwa Babeli ambako pia bado tunajaribu kutunza matendo yetu ya kidini katika ubatili ili kujishawishi sisi wenyewe kwamba tuko sawa kwa Mungu.

Ufalme wa Babeli ulioiteka na kuihusuru Yerusalemu ulikuwa ni mahali pa kifo cha kiroho kwa kanisa na Israeli. Kwa sababu Waisraeli waliacha sheria za Mungu kwa muda wa vizazi vingi, Mungu akawakomesha watoke Yerusalemu, Mji Mtakatifu. Aliwaruhusu jeshi la Wababeli [Wakaldayo] kuwajilia, kuzibomoa kuta zilizowalinda Waisraeli, na kisha kuwachukua mateka mpaka Babeli kwa miaka sabini. Habari ya kurudi kwao Yerusalemu ndio habari kubwa ya uamsho katika Biblia. Tunapofanya mambo kama hayo ambayo Waisraeli waliyafanya, tutapokea matokeo yale yale, vyote kukomeshwa na Babeli ya kiroho na pia urejesho wa kanisa kupitia uamsho.

Kwenye sura ya 2 ya kitabu cha Nehemia, kama Nehemia alivyoviona vifusi vya mji wake wa kujivunia wakati wa usiku uliotulia, lazima alihisi dhiki nyingi na mashutumu ambayo yalikuwa pale kwa muda wa miaka sabini. Kuharibiwa kwa Yerusalemu ilikuwa siyo tukio la kawaida kwenye mwonekano wa hukumu za Mungu kwa watu wake mwenyewe kwa sababu walikataa kumsikiliza. Kabla hatujaianza kazi ya kuzijenga kuta za mji wa Mungu, yatupasa kwanza kutambua dhambi za watu wetu na kuviona vifusi kama Nehemia alivyoona:

> *Nikatoka nje usiku, kwa njia ya lango la bondeni, nikashika njia iendayo kisima cha joka, na lango la jaa, nikazitazama kuta za Yerusalemu, zilizokuwa zimebomoka; na malango yake yameteketezwa kwa moto. Kisha nikaendelea mpaka lango la chemchemi, na ziwa la mfalme; lakini hapakuwa na nafasi ya kupita kwa yule mnyama aliyekuwa chini yangu. Kisha nikapanda usiku kando ya kijito, nikautazama ukuta, kisha nikarudi nyuma, nikaingia kwa lango la bondeni, nikarejea hivyo. (Nehemia 2:13-15)*

Kadiri nisomavyo aya hii, mimi hujisikia kama nimelowana kwa umande wa usiku ushukao kutoka juu angani, kiwango cha ukimya wangu hutoweka tu kwa sababu ya makelele ya farasi. Mji wa kujivunia ambao ulikuwa umepambwa kwa uzuri sasa ulikuwa ni

matuta ya vifusi. Jinsi gani moyo wa Nehemia ulivunjika kadiri alivyotembea njiani kupitia kwenye vifusi! Hivi ndivyo tunavyotakiwa kuhisi tunavyoliona Kanisa. Wakati mwanzoni lilikuwa la kusisimua na hai lenye mguso wa umwagiko wa Roho Mtakatifu, ambapo madhabahu zilikuwa zikijawa na Wakristo wapya wanaozaliwa mara ya pili, ambapo miujiza ilitegemewa kutokea na mambo yasiyo ya kawaida yalikuwa kawaida kuyaona, bali sasa tunaweza tu kusikia mwangwi wa kile kilichokuwepo katika kanisa.

Toba inayoambatana na kufunga na kuomba lazima itangulie kuanza kabla ya urejesho wowote wa kiroho. Kabla ya kumkaribia mfalme, Nehemia alijinyenyekesha mwenyewe mbele za Mungu na kutubu kwa ajili ya dhambi za watu wake. Bila toba, Nehemia asingepata hiyo fursa ya kumwomba mfalme kuondoka kwenda kuzijenga kuta za Yerusalemu.

> *Na lango la samaki wakalijenga wana wa Senaa; wakazitia boriti zake, wakasimamisha milango yake, na vyuma vyake, na makomeo yake. Na baada yao akafanyiza Merenothi, mwana wa Uria, mwana wa Hakosi. Na baada yao akafanyiza Meshulamu, mwana wa Berekia, mwana wa Meshezabeli. Na baada yao akafanyiza Sadoki, mwana wa Baana. Na baada yao wakafanyiza Watekoi, lakini wakuu wao hawakutia shingo zao kazini mwa bwana wao. Na lango la kale wakalifanyiza Yoyada, mwana wa*

*Pasea, na Meshulamu, mwana wa Besodeya; wakazitia boriti zake, wakaisimamisha milango yake, na vyuma vyake, na makomeo yake. (Nehemia 1:3-6)*

Vivo hivyo, kama kanisa lisipotambua kukengeuka kwake na kukusudia kutubu, ndipo Mungu hawezi kulirejesha, kwa sababu litarudi nyuma kwenye hali ambayo imelisababishia kukengeuka kabla.

Wale waamini wanaoendelea kukaa kwenye mchakato unaoendelea pole pole wa kuangukia katika ukengeufu hawawezi kuona hali hiyo kuwa inatambaa kuingia kanisani kwao na mara nyingi huwa wako kwenye kukataliwa, hali ambayo haitawaruhusu kukubali kwamba kanisa lao linakufa. Mchakato wa kuzifuata desturi zetu za kidini hudhihirisha ukweli kwamba tunashindwa pole pole. Hatuwezi kuiona hali hii kwa sababu hatuzingatii, na vinginevyo, haina raha kufikiria kuhusu hilo. Ni rahisi sana kuwasikiliza watu walio mchanganyiko wanaotwambia kwamba bado Mungu anatupenda bila kujali ukweli mwepesi kwamba tumekwishauacha uwepo wa Mungu siku nyingi nyuma na sasa tunakabiliwa na hukumu.

Hatulioni hili kwa sababu hatutaki tulione.

## Madhababu Zilizokufa

Mahali fulani kwenye hii hatua ya kutambua, lazima tufikie kwenye kutambua kwamba, bila kujali

tunalipenda kanisa letu kwa kiasi gani, kama hatuokoi nafsi, hatumo kwenye uamsho. Kadiri ilivyo rahisi na kawaida kama inavyotakiwa kuwa, kufikia huo utambuzi ni kikwazo kikubwa kinachoyafanya makanisa mengi kukaa mbali na mtembeo wa Mungu usio wa kawaida kati yao.

Yesu alisema kwamba, hakuna mtu awezaye kuja kwake isipokuwa yule anayevutwa na Baba (Yohana 6:44). Kwa kutumia hoja hii ya msingi, kama ndiye Roho wa Mungu anayezivuta nafsi kutubu, na nafsi haziji kwenye madhabahu yako kutubu, basi hii inamaanisha kwamba Mungu hawavuti watu mahali hapo. Kanisa, hasa uongozi wake, wanapaswa kujiuliza kwa nini.

Je madhabahu zenu ziko tupu? Je kuna ukosefu wa miujiza isiyo ya kawaida na watu kutotembelea kanisa lenu? Huduma zenu zimekuwa na mafundisho makavu kuhusu Mungu yakiwa na pointi tano tu, wimbo, na utani kidogo? Nguvu ya Roho Mtakatifu haibubujiki tena kupitia huduma zenu kama upepo uvumao kwa kasi? Je mambo hayo yamekwishatokea?

Tunahitaji kuwapa watu chakula wanachokihitaji ili warudi tena na tena. Chumvi njema ni ile inayofanya vyakula viwe na ladha nzuri. Yesu anafundisha kwamba sisi kama waamini ni chumvi ya ulimwengu, lakini tukipoteza ladha yetu, hatutafaa kuwa chumvi njema tena (Mathayo 5:13). Ulimwengu una njaa ya ile kweli, lakini kile tunachotoa hakina ladha nzuri, hawatakitaka.

Labda huu sasa ni wakati wa kuamka tukiwa na ukweli kwamba kitu fulani hakiko sawa katika kanisa. Kitu fulani muhimu kinakosekana katika kutembea kwako na Mungu, na unahitaji kukirejesha. Usipofanya hivyo, badala ya kutembea naye utajikuta unatangatanga bila kuwa na malengo.

Bila shaka, unaweza kutosheka na kanisa lako kwa jinsi lilivyo. Ikiwa hivi ndivyo ilivyo, basi hutapata kile unachokitamani. Mungu hatakusogeza mbele kuliko unapotaka wewe kwenda. Kama atakusogeza, hautakuwa na uwezo wa kumudu gharama kubwa ambayo utaingia ili kufika hapo, na kamwe hautaweza kuwalisha watoto wachanga katika Kristo ambao atakutuma kwao. Aliyatoa maisha yake kwa ajili ya hizo nafsi za thamani, na hataweza kuziweka mikononi mwa watu wasiojali sana kuyatoa maisha yao kwa ajili ya nafsi hizo.

Kanisa lisilookoa nafsi ni kama mti wa mtini ambao umenyauka na hauzai matunda tena. Ni shina lenye matawi yaliyokufa. Hutaweza kupata msamaha ambao utabadilisha hukumu ya Mungu kwa sababu ya kutozaa kwako matunda. Yesu aliulaani mti wa mtini ingawa haikuwa majira yake ya kuzaa matunda (Mathayo 21:19-21). Kamwe haujawahi kutokea wakati ambao kuokoa nafsi siyo majira yake.

Shina lisilozaa matunda lazima likatwe kwa sababu limekuwa ubao uliokufa ambao kamwe hautakuwa hai tena (Yohana 15:6). Chemchemi inapoacha kutiririka

kupitia kanisa lako, litakufa na halitafaa kitu bali kuchomwa motoni. Unapoacha kuona tena nafsi zikiokoka, wagonjwa wakiponywa, miujiza na udhihirisho wa Roho Mtakatifu vikitokea, basi ndio muda wa kujitoa kwenye uamsho kwa maana chemchemi haitiririki na kanisa lenu limekufa. Kwa muda wa miaka kumi na miwili ya mwishoni, nimehubiri kwa mamia ya makanisa katika Afrika, na karibu watu wote ndani ya makanisa hayo hutegemea mwinjilisti mkubwa mzungu wa Marekani atawabariki kwa ujumbe wa kutia moyo. Hata hivyo, mimi huwaambia kwamba, mimi siko hapo ili kwamba wabarikiwe, wapate fedha, wapate mume, au kuongeza mazao yao. Mimi niko pale kuwaonyesha Kweli ya kile Mungu anawataka kufanya wao kama waamini wa Injili ya Yesu Kristo.

Changamoto yangu ya kwanza ninayowapa ni kuwauliza kama wanaamini wana kanisa zuri. Kama watasema wameridhika na kanisa lao na hali yao ya kutembea katika Ukristo, ndipo mimi huwa sina haja ya kuendelea nao mbele. Bora nitafute kundi jingine la kanisa ambalo lina njaa ya kitu kikubwa kuliko kufuata nafasi za kazi tu kanisani. Kama wasemavyo, mimi sitafuti mtu asiye mtafutaji; bali mimi natafuta watu watafutaji. Watafutaji ni wale wanaoitafuta kweli, ambao mioyo yao imepondeka kwa ajili ya watu waliopotea, ambao hawasemi "kanisani kama kawaida"

na hulia kwa huzuni kwa ajili ya kitu kikubwa katika Mungu. Wana njaa, huzuni, na wanamtafuta Mungu.

Mimi huwapa changamoto kwa kuwauliza nafsi ngapi mpya zimeokoka katika kanisa lao juma lililopita. Vipi kuhusu mwezi uliopita? Sawa, vipi kuhusu mwaka jana? Hili ni jaribio la karatasi ya "litmasi" [ya vipimo vya maabara ibadilikayo rangi] kwa ajili ya Ukristo. Haijalishi kanisa lako ni zuri kiasi gani, mchungaji wako ni wa ajabu kiasi gani, au waumini wangapi wanapendana wao kwa wao. Swali ni, Mnajishughulisha na kuokoa nafsi kwa ajili ya Yesu Kristo? Ndiyo au hapana? Je mnajaribu hata kidogo? Kama bado, basi hamtimizi wito ambao Mungu ameuweka katika kanisa. Kila juma waamini wengi hukaa kwenye kiti kile kile kanisani kwao wakiwa wamezungukwa na nyuso za watu wale wale. Wao huambiana mambo yale yale mazuri waliyoambiana juma lililopita. Husema tunataka uamsho, lakini hutegemea utashuka tu kutoka mbinguni mpaka kwenye viganja vyao wakiwa wamekaa kama mti uliokufa kwenye benchi la ubao bila kufanya chochote. Kama ilivyo kwa msemo wa zamani usemao, Kama hutafanya kitu, hakuna kitakachotokea.

Kuna baadhi ya watu hawajali kabisa. Wanalo kanisa wanalolipenda na hupinga mabadiliko. Hawataki chochote chenye kusumbua hali yao ya kustarehe wanayoifurahia sasa. Hawa ni viriba vikuukuu ambavyo haviwezi kubeba divai mpya (Luka

5:36-39), ambayo ni umwagiko wa Roho Mtakatifu atakayetumwa na Mungu kwao. Ili uamsho uje, watu hawa wanaweza aidha kupasuka, kubadilika au kuacha.

Kwa kiwango fulani unalazimika kukubali kwamba kitu fulani kinakosekana na kwamba moto wa madhabahuni penu umeondoka. Roho wa Mungu hayupo tena, nafsi haziokolewi tena, na haionyeshi kama kutakuwa na mvuto kwa wenye dhambi kusogelea madhabahu yenu baada ya muda mfupi ujao. Kwa nini wasisogee? Una nini cha kuwapa kilicho zaidi ya maneno yanayorudiwa rudiwa mara nyingi hata tamaa yao ya asili iweze kuisha na wasiendelee kutokujali watu wengine wasiookoka?

Ni pale tu tunapokubali hali ya kuanguka kwetu ndipo tunaweza kuirudisha mioyo yetu kuitikia kwenye wito wake wa uamsho.

## Maonyo Kutoka kwa Nabii Yoeli

Sura ya kwanza ya kitabu cha Yoeli inaelezea ukengeufu na uamsho ambao utatokea kabla tu ya Kurudi wa Bwana Mara ya Pili. Inaelezea wakati tunaoishi sasa:

> *Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige; na yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare; na yaliyosazwa na parare yameliwa na madumadu. (Yoeli 1:4).*

Kwenye maandiko hapo juu, Yoeli alikuwa akielezea jinsi mashamba ya mavuno, ambayo yanaashiria nafsi zinazotakiwa kuokolewa, yanavyoweza kuharibiwa na janga moja la walaji baada ya jingine mpaka kisibaki chochote. Makanisa yetu yanasimama kama sakafu za kupepetea nafaka na maghala ya kupokelea na kutunza mavuno ya nafsi mpya ndani yake.

Sakafu za kupepetea zinasimama kama mahali ambapo ngano hupepetwa na kutenganishwa na makapi, na maghala ni mahali ambapo ngano iliyosafishwa huhifadhiwa. Kwa namna hiyo hiyo, kanisa ni mahali ambapo ngano ya kiroho hutenganishwa na makapi ya ulimwengu na kuhifadhiwa hemani kwenye usalama ndani ya kanisa. Kama mavuno yameharibiwa kupitia haya majanga, hii inaashiria kwamba nafsi chache tu ndizo zitapatikana kwa kuokolewa. Kama uamsho unahusiana na kuokoa nafsi zilizopotea, basi hii ni ishara ya wazi kwamba kuna kitu fulani kinakosewa sana na makanisa yetu.

Kwenye msitari wa 5, nabii anawaita walevi na wanywaji wa divai, watu ambao wameitwa kutunza mzabibu na mtini wa Mungu na anawaambia kwamba divai mpya imekatiliwa mbali na vinywa vyao katika nyumba ya Bwana. Kama divai mpya inawakilisha umwagiko mpya wa Roho Mtakatifu wa Mungu, basi hii inamaanisha kwamba kanisa la kidesturi linakwenda kukosa huu umwagiko wa Roho Mtakatifu. Badala

yake, Yoeli anawaita watu ambao wana njaa ili kwamba wayaambue magamba ya shina la mzabibu na mtini:

> *Maana taifa limepanda juu ya nchi yangu, Lenye nguvu, tena halina hesabu; Meno yake ni kama meno ya simba, Naye ana magego ya simba mkubwa. Ameuharibu mzabibu wangu; ameuvunja mtini wangu; ameyaambua magamba yake kabisa; ameuangusha chini; matawi yake yamefanywa kuwa meupe. (Yoeli 1:6-7)*

Ndani ya Biblia yote, mzabibu na mtini ni alama za Roho na Neno la Mungu, hivyo hili linaweza kuwa ni kundi la watu ambao wana njaa ya Mungu kuliko kundi lililokuwepo kabla yao. Kundi hili la watu laweza kuwa ni wasomaji walafi wa Neno la Mungu na hupiga radi ya maombi katika madhabahu. Yoeli alirejea baadaye tena kuhusu hilo taifa kwenye nusu ya kwanza ya sura ya 2.

Kwenye msitari wa 8, Yoeli analiita kanisa "kuomboleza kama mwanamwali [bikira] avaaye magunia kwa ajili ya mume wa ujana wake." Ikiwa sisi ni Bibi-Harusi bikira wa Kristo, basi hili ndilo lingekuwa kilio cha maombolezo kwetu kwa sababu kuna kitu kinakwenda vibaya katika mahusiano yetu na Bwana. Kama ilivyo kwa bibi-harusi bikira aliyempoteza mume wake mpenzi, hii inatakiwa

kulifanya kanisa kupaza sauti ya vilio vya kweli. Roho wa Mungu amepotea na tumebaki tupu na peke yetu.

> *Sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji Zimekatiliwa mbali na nyumba ya Bwana; Hao makuhani, wahudumu wa Bwana, wanaomboleza. (Yoeli 1:9)*

Hiki ndicho kilio chetu kinavyotakiwa kuwa. Yatupasa kuomboleza kwa sababu ya kukosekana kwa huduma hizi mbili muhimu za Bwana: Sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji. Zingatia kwamba ni Mungu ndiye aliyezikatilia mbali, siyo sisi. Hebu na tutazame kwenye sadaka hizi mbili muhimu na kile zinaashiria.

Sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji zilikuwa ni sehemu ya Matoleo ya Kila Siku iliyoelezwa katika Kutoka 29 na Hesabu 28. Sadaka hii ilihitajika kutolewa mara mbili kwa siku, kila siku. Ni alama ya kutembea kwetu na Mungu na ibada yetu ya kila siku. Kama tu tulivyoamrishwa kutembea katika haki mbele za Mungu na kuzitunza amri zake, ndivyo alivyo Mwanakondoo asiye na ila aliye dhabihu ya haki yetu juu ya madhabahu zilizomo mioyoni mwetu. Moto wa hizo madhabahu za Agano la Kale kamwe haukutakiwa kuzimika, ndivyo pia tunavyotakiwa kuutunza moto ndani ya mioyo yetu uwake bila kuzimika.

Sadaka ya unga ilikuwa ni unga safi laini uliochanganywa na mafuta, hii ni mfano wa Neno la Mungu, ambalo ni Chakula cha Uzima, kilichotiwa

mafuta na Roho Mtakatifu, mafuta safi ya kutakasa. Paulo aliandika kwenye 2 Wakorintho 3:6 kwamba andiko [barua/sheria] linaua bali Roho huhuisha. Mafuta hayo ni upako unaolifanya Neno la Mungu kuwa hai.

Sadaka ya kinywaji ilikuwa ni divai kali iliyomiminwa mbele za Mungu, ikiwa ni ishara ya kujimimina kwetu katika maombi makali mbele za Mungu.

Vitu hivi viwili lazima viambatane na kujitoa kwako kwenye huduma na kuishi kwa haki ili ukubalike kwa Mungu. Kwa kawaida, kama vitaondoka kwenye nyumba ya Bwana, kuna sababu kubwa ya kuomboleza.

Kwenye mstari unaofuata, Yoeli analia kwamba Bwana ameongeza hukumu yake dhidi ya kanisa:

> *Shamba limeharibika, nchi inaomboleza; maana nafaka imeharibika, divai mpya imekauka, mafuta yamepunguka. (Yoeli 1:10)*

Shamba hili ni shamba la mavuno ya nafsi (Yohana 4:35). Neno la Kiebrania lenye sawa na "limeharibika" ni "*shadad*," likiwa na maana ya "limepotea na kuharibiwa." Kama mashamba yameharibiwa na mavuno kupotea, basi hii inamaanisha kanisa haliokoi nafsi, madhabahu zetu ziko tupu, nchi inaomboleza,

nasi tuko kwenye hali ya kukata tamaa ili kuhitaji uamsho.

Kama matokeo ya madhabahu zilizokufa, Mungu huondoa uwezo wa mwamini katika kufanya mambo matatu: (1) kushika kina cha Neno la Mungu (masuke yenye nafaka) (2) kuzama kwenye maombi makali (divai kali), na (3) kuwa na uzoefu wa upako mkubwa wa Roho Mtakatifu (mafuta safi).

Masuke, au ngano, ni Neno la Mungu. Ngano huzalisha unga unaotengeneza chakula, na Neno la Mungu ni Chakula cha Uzima. Kama ngano itapotea au kuharibiwa, basi hii inamaanisha Mungu amekitia muhuri [amekifunga] kina cha Neno lake kama anavyotwambia katika Isaya:

> *Na maono yote yamekuwa kwenu kama maneno ya chuo kilichotiwa muhuri, ambacho watu humpa mtu aliye na maarifa, wakisema, Tafadhali ukisome hiki; akasema, Siwezi, kwa kuwa kimetiwa muhuri; (Isaya 29:11)*

Ngano ya Chakula cha Uzima [Neno] inapoharibiwa au kutiwa muhuri ndani yetu, tunaweza kuisoma Biblia, lakini hatutaweza kupokea ufahamu wa kina wa Neno ambao huja tu kupitia Roho Mtakatifu. Neno litakuwa limetiwa muhuri. Mtume Paulo anatwambia kwamba Roho Mtakatifu ndiye hulipa uhai Neno la Mungu (2 Wakorintho 3:6). Bila Roho, Biblia

itabaki kuwa kitabu tu na hakitaweza kuleta mabadiliko makubwa ambayo Biblia inaweza kuyaleta pale inapovuviwa na Roho. Kama Neno la Mungu "limeharibiwa," ndivyo na sisi tutakavyokuwa.

Kuna maeneo mengi kwenye Biblia ambapo divai imetumika kama alama ya Roho wa Mungu. Kama tunavyoweza kuona matokeo ya divai kwa wanaoinywa, ndivyo tunavyohisi matokeo ya ushirika wetu na Mungu tunapokunywa Roho Mtakatifu wa Mungu katika maombi. Lakini, Mungu anapoikausha kabisa "divai mpya," maisha yetu ya maombi na ushirika wetu katika Roho kupitia maombi kwa Mungu hukauka pia. Twaomba, lakini huo upako wa kusisimua ambao wakati mwingine hushuka na kuangaza muda wetu wa maombi ni divai mpya ambayo itakuwa inakosekana.

Neno la Kiebrania lenye maana sawa na "kukauka" ni "*yabesh,*" linalomaanisha "kuchakaa / kufadhaika kama mtu anayejuta." Hivyo basi, divai inapochakaa au kukauka, ndivyo maisha yetu ya maombi yatakavyokuwa. Mara nyingi katika Agano la Kale, Mungu alikataa kusikiliza vilio vya Waisraeli kwa sababu waliukataa wito wake mbalimbali wa kutubu dhambi zao. Kama na sisi hatutafanya kile Mungu anatuagiza kufanya, yeye pia hatafanya kile tunachomwomba kutufanyia.

Kama uthibitisho wa huku kukauka kwa maisha yetu ya maombi, nitakazia kwenye utofauti kati ya

maisha ya maombi ya kizazi chetu na maisha ya maombi ya watu wa vizazi vya zamani. Tukirudi hako nyuma, maombi ya mikutano ya mikesha ya usiku yalifanyika mara kwa mara, na waamini waliomba usiku wote kwa muda mrefu. Leo tumekandamizwa sana hata kushindwa kuwa na mikutano ya maombi ya mikesha ya usiku, na ikiwa tutafanya, mikutano hii huwa na watu wachache sana kwa kuwa kila mmoja hapendi kubaki usiku wote akiwa na wengine.

Kizazi hicho cha zamani kiliomba, na waliyachukua maombi kama wakati wa kupiga vita na "wangeomba kikamilifu" mpaka wapokee jibu kutoka kwa Bwana. Leo, makanisa mengi yamepoteza sanaa ya maombi. Machache huchukulia maombi kama wakati wa kumaanisha kwenye mapambano katika Roho na hutumia muda wa saa moja, masaa mawili, au matatu au vyovyote itakavyokuwa ili kupata huo ushindi ambao huupokea pale "mpenyo" unapopatikana hadi kwenye kiti cha enzi / kiti cha neema cha Mungu.

Wakristo wengi ambao mimi huzungumza nao kuhusiana na jambo hili hawajui hata namaanisha nini ninapozungumzia maneno haya. Kwao maombi ni wakati wanaopenda kufanya hivyo, ambao huutumia kwenye maombi matulivu ya kuzungumza na Mungu. Tunao "wakati wa kutafakari" na Mungu, lakini wale wazee wetu wa kike walizitikisa mbingu na kuangusha ufalme wa giza. Kwa nini kuna tofauti ya namna hii? Kwa sababu roho ya kuomba, divai mpya, imekauka

kanisani leo na hatuna nguvu tena za kuomba kama tulivyokuwa tukiomba mwanzo.

Jambo la tatu ambalo nabii Yoeli anatwambia ambalo Mungu amefanya ni kusababisha mafuta "kupunguka." Mafuta haya ni mafuta ya upako wa Roho Mtakatifu. Neno la Kiebrania lenye maana sawa na "kupunguka" ni *amal*, linalomaanisha "kugandisha hadi kuwa hafifu." Mafuta ya upako yanapopunguka, au kuganda na kuwa hafifu, ndipo miujiza huanza kupotea kwa sababu ni nguvu ya Roho Mtakatifu pekee ndiyo hufanya hiyo miujiza isiyo ya kawaida.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba ishara zitaambatana nao waaminio (Marko 16:17-18). Hilo lilikuwa ni moja ya maneno yake ya mwisho aliyoyaacha kwao ili kwamba watiwe moyo wanapoipeleka Injili kwa ulimwengu wote. Marko pia alilihusisha hilo, akijengwa katika hiyo hamasa, "nao wakatoka, wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo." Ndiyo, hapa ndipo tulipo leo. Tunalo agizo lile lile, imani ile ile, na Mungu yule yule. Ziko wapi basi ishara?

Hili ni kama swali alilouliza Gideoni: yako wapi matendo yake ya ajabu? Waisraeli wa kizazi chake walikuwa wamejisalimisha wenyewe kwa adui na walimsahau Mungu. Waamaleki waliichukua nchi yao na waliharibu mavuno, kama tu ilivyo leo kuhusu adui wetu wa mambo ya kidunia amejipenyeza kwenye

makanisa yetu na ameharibu mavuno ya nafsi. Hata hivyo, Gideoni alikuwa tofauti. Alimtafuta Bwana kwa siri, na Bwana akamtuma malaika kwenda kumwambia kuwaokoa Israeli. Lakini alikuwa na hili swali moja linalochoma:

> *Gideoni akamwambia, Ee Bwana wangu, ikiwa Bwana yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Yako wapi matendo yake ya ajabu, waliyotuhadithia baba zetu, wakisema, Je! Siye Bwana, aliyetuleta huku kutoka Misri? Ila sasa ametutupa, naye ametutia katika mikono ya Midiani. (Waamuzi 6:13)*

Kutokuwepo kwa miujiza huashiria kutokuwepo kwa Mungu. Vyovyote utakavyoisoma hali hiyo, inamaanisha kifo kwa kanisa. Kanisa haliko kwenye nafasi ya Mungu ambayo linatakiwa kuwepo, na kwa bahati mbaya linahitaji uamsho.

Kwenye hii sura ya 1 ya Yoeli, Bwana aliwaita watumishi wa Bwana wakeshe wakilia na kuomboleza kwa sababu ya dhiki ya kanisa. Ng'ombe, akiashiria waamini, wanalilia malisho, wanadhurura wakitafuta chakula, lakini hawajaweza kupata chochote. Maghala na hifadhi, ambazo ni makanisa ambamo mavuno ya nafsi yanatakiwa kuletwa, yamevunjwa yote. Hata mito ya maji ya uzima imekaushwa.

Kwenye msitari wa 16, tunaona kwamba, chakula, ambacho ni chakula cha kiroho, kimekatiliwa, hata pia furaha na kicheko, mbali na nyumba ya Mungu. Furaha ya Bwana ni nguvu zetu. Mungu asipofurahi katika nyumba yake, tutakuwa kwenye shida kubwa. Hakuna tafsiri mbadala.

Neno hili limeelekezwa maalumu kwa Kanisa la siku za mwisho. Kuna maeneo sita ndani ya Yoeli ambayo hasa yanarejea kwenye siku za mwisho – Yoeli 1:15, 2:1, 2:10, 2:11, 2:31, na 3:41. Huu sio unabii kwa ajili ya makundi mengine ya watu wa nyakati zingine – Mungu anazungumza nasi wakati wa kizazi hiki! Anasema atamwondoa Roho, kina cha Neno na maombi, miujiza na uponyaji, na hata furaha na kicheko mbali na kanisa katika siku za mwisho. Na unashangaa kwa nini tunaona miujiza michache?

Yeye anatupatia sababu ya hii hali ya kutahayarika kwenye mstari wa 11:

> *Tahayarini, enyi wakulima; Pigeni yowe, enyi watunzaji wa mizabibu; Kwa ajili ya ngano na shayiri, Maana mavuno ya mashamba yamepotea. (Yoeli 1:11)*

Hapa kuna mashutumu ya laana dhidi ya kanisa: mavuno ya nafsi yamepotea na yanashuka jehanamu, na Mungu anatulaumu. Sisi ni watunzaji wa nyumba ambao tunatakiwa kuyaleta mavuno nyumbani mwa

Bwana. Lakini tunalaumiwa? Sana tu. Tuna shughuli nyingi, hatuendi kanisani na hata hatujui hilo.

Amosi anasema "kutakuwa na njaa katika nchi, siyo njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya Bwana." (Amosi 8:11-13) Makanisa yanaweza kuonekana kila mahali nchini Marekani, lakini hatulishwi kwa mambo ya ndani sana kuhusu Mungu. Aha! Biblia zipo kila mahali unapotazama, lakini kama Isaya alivyolia (29:11), kitabu kimetiwa muhuri [kimefungwa] kwa ajili yetu; sote tunasoma Biblia, lakini maarifa yetu yanatambaa chini. Ngano, kina halisi cha Neno la Mungu, kimepotea na hakipatikani kwetu. Tunalia kwa sababu ya njaa yetu, lakini hatujui twende wapi kupata chakula kwa sababu mazingira yote ya kiroho yanayotuzunguka hapa Marekani yameharibiwa na kukataliwa.

Kama ningekuwa kipofu asiye kipofu ambaye hana ufahamu wa ulimwengu unaonizunguka, hii sura katika kitabu cha Yoeli pekee ingetosha kunishuhudia kwamba kanisa la siku za mwisho limeanguka mbali na Mungu. Isingekuwa vigumu kuamini kwamba kuna kiasi kidogo sana, kama ni chochote, kilichobaki kwenye mashamba yenye kuzaa sana mavuno ambayo yana nafsi na bubujiko la Roho wa Mungu. Lakini sisi, kama vile watu ambao Yohana ameandika kuhusu wao, tuna macho lakini hatuoni na masikio lakini hatusikii:

*Amewapofusha macho, Ameifanya mizito mioyo yao; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakafahamu kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya. (Yohana 12:40)*

Sehemu kubwa ya ulimwengu wa makanisa yetu imekufa, bali tunatumikia ukengeufu wetu hata tusiwe na macho ya kuliona hilo wala mioyo ya kuamini hilo hata Maandiko Matakatifu yanashuhudia mbele zetu.

## Miujiza Iko Wapi?

Roho yule yule ambaye huzivuta nafsi zilizopotea kuja kwenye madhabahu ni Roho huyo huyo ambaye huponya wagonjwa, hufufua wafu, na kutenda miujiza. Wakati mnaweza kuona rahisi kuelezea kuhusu madhabahu zenu zilizo tupu kwa kujitetea kidini na kithiolojia, ni vigumu kukataa hali ya kukosekana kwa nguvu za Mungu za kutenda miujiza ambayo Biblia inasema itafuatana nao waaminio. Kama tulivyotangulia kusema, nabii Yoeli alitangaza kwamba Mungu ataondoa mafuta (mafuta ya upako wa Roho Mtakatifu ambaye hutenda miujiza). Kwa maneno mengine, hatuoni miujiza inayotoka kwa Roho Mtakatifu pekee kwa sababu mafuta yamekomeshwa.

Gideoni, katika Waamuzi 6, alikuwa ni mkulima maskini tu, lakini aliweza kuona huzuni iliyokuwa kwa Israeli walipokuwa mikononi mwa maadui zao. Waisraeli walimlilia Mungu awaokoe kutoka kwa

maadui zao ambao walichukua nchi yao, lakini Mungu aliwajibu maombi yao kwamba amewapa sheria yake waitunze lakini badala yake wakachagua dunia. Kwa sababu ya hilo, akawaruhusu maadui kuingia nchini na kuichukua nchi. Hivyo, sasa Gideoni alitaka kupepeta ngano yake kwenye shinikizo kwa siri kwa sababu ya kuwaogopa Waamaleki ambao wangeiiba. Kitendo cha kupepeta ngano ambacho ni ishara ya upatikanaji wa Chakula cha Uzima, na shinikizo la maombi, ambamo tunautafuta uso wa Mungu, ilitakiwa kufanyika kwa siri. Lakini ni katika hilo eneo la siri pamoja na Mungu ndimo maombi yakajibiwa.

Uharibifu wa mashamba ya mavuno kwa sababu ya Waamaleki ni ushuhuda mbaya unaotokea pale kanisa linapojiunganisha na dunia. Tunapoiruhusu dunia kuingia kanisani, dunia itachukua utawala na kuyaharibu mavuno. Nafsi (mavuno) hazitaendelea tena kukusanyika kwenye madhabahu zetu. Tutaishia kuwa dhaifu na wasio na nguvu mbele za maadui zetu, tusioweza kuushinda udhaifu wa mwili, na kuwa wageni kwenye nguvu za Mungu. Na sisi ndio tuliokuwa wa kwanza kuiruhusu dunia iingie!

Gideoni aliitambua huzuni yao ilikuwa ni kwa ajili ya nini wakati wengine waliridhika kuendelea na mambo yalivyokuwa yakiendelea, hata kujenga madhabahu za miungu ya Baali katika jaribio batili la kumfurahisha adui.

Wakati wengine waliridhika na kanisa lililokufa, Gideoni hakuwa hivyo.

Wakati malaika anaonekana kwake na kutangaza kwamba Gideoni alikuwa ni "shujaa," mwitikio wa Gideoni ulikuwa ni kurudisha jibu akiwa amekata tamaa, "Ikiwa Bwana yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Yako wapi matendo yake ya ajabu [miujiza]?" (Waamuzi 6:13) Alitambua kwamba ukosefu wa miujiza iliashiria kutokuwepo kwa Mungu.

Ndiyo. Swali zuri. Iko wapi miujiza? Lini mara yako ya mwisho kuona mgonjwa akiponywa, mfu akifufuliwa, Roho Mtakatifu akimwagika katika huduma zenu, na nafsi zikikusanyika madhabahuni ili kuokoka? Kama makanisa yetu ni mazuri sana, sasa Roho wa Bwana yuko wapi? Iko wapi miujiza?

Uponyaji utokanao na imani ni mchache kwa sababu hatuutegemei kutokea. Wakati ambao tunatakiwa kunyanyua mikono yetu juu ili kuwaombea wagonjwa, ndio tunaoshikilia ahadi [apointimenti] ya kukutana na daktari kwa sababu kwa kweli hatuamini kama Mungu atatuponya. Jambo kama hili huwa tunasema "ni busara kupata ushauri wa daktari," lakini Mungu analiita kutoamini. Na huoni haja ya kumfufua aliyekufa! Tendo hili limechukuliwa kuwa si kitu bora sana, upuuzi mkubwa. Kwa kuitii dhiki yetu ya kiroho, tunatumainia kupata amani ambayo kamwe haitakuja kwa kujiunganisha na dunia. Bali watu wa Mungu,

kama vile Gideoni, huona kile kinachopungua na kuikataa hali ya kuridhika bila kuwa nacho.

Jibu la malaika kwenye kilio cha Gideoni kuhusu kukosekana kwa wokovu wa Mungu na miujiza linasema, "Enenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe Israeli" (Waamuzi 6:14). Huu uwezo ulikuwa ni kitu gani, hizo nguvu? Nguvu za Gideoni zilikuwa ni zile alipotambua hali yao ya kukengeuka (kurudi nyuma) na kumwacha Mungu na yeye hakutaka kuwa hivyo.

Ukosefu wa miujiza katika makanisa yetu inaashiria ukosefu wa Roho Mtakatifu ambaye huitenda. Na bado tumeridhika na kugaagaa kwenye kubweteka badala ya kukabiliana na ukweli kwamba nguvu ya Mungu imeondoka kwetu na kutuachia kanisa tupu ambalo kuta zake za kujihami dhidi ya adui zimebomolewa.

## Wosia wa Mwisho wa Yesu

Mtu tumpendaye anapokaribia kufariki dunia, huwa tunampenda zaidi. Walio karibu na kufa wanapotulia kwenye malango ya kutokea, karibia na kuingia mautini, kisha wakatugeukia kwa kutwambia wosia wa mwisho, wosia huu huwa ni kitu ambacho tunakitunza ndani ya mioyo yetu. Huo wosia wa mwisho ni muhimu. Baba anayekufa anapotoa wosia wa mwisho kwa wanae ndipo hujiona anakufa kwa amani akifahamu kwamba watautekeleza.

Kama vile Yesu alipokaribia kuondoka duniani, jambo la mwisho alilotuagiza kumfanyia lilikuwa ni kuhubiri injili ulimwenguni mwote. Huu wosia wa mwisho wa Yesu unajulikana kama Agizo Kuu. Ndio lilikuwa kusudi lote la kuja kwake na kifo chake msalabani. Yesu alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi kutoka jehanamu, na alituachia jukumu la kumalizia kazi hiyo. Agizo hili halina onyo la kututaka mpaka tuwe watu wasomi, viongozi mashuhuri katika jamii, wala mbwa walio walinzi wa kanisa. Ni rahisi tu: kuokoa nafsi na kufanya wanafunzi [Marko 16:15-16, Mathayo 28:19-20]. Ni mchakato wa kujikana mwenyewe, kuchukua msalaba wako na kumfuata. Kumfuata wapi? Pale Golgotha, mahali ambapo aliyatoa maisha yake kwa ajili ya waliopotea.

Je tumefuata hiyo njia ile ile, au tumechenga kupitia njia za kimaisha zinazoelekea kwingineko? Je tumeshawishika sisi wenyewe kwamba tutatimiza neno lake la mwisho kwa kuhudhuria kanisani? Je ushirika na watakatifu wengine umechukua nafasi ya wajibu wa kwenda kuwaokoa wenye dhambi? Kadiri tuinuavyo mikono yetu katika ibada wakati wa nyimbo, tukiwa salama katika imani kwamba tumeokolewa, je tumeridhika na kuzuia huu upeo wetu wa kumwona Mungu kwenye mpaka zinapoishia kuta za kanisa? Tunaporudisha ndani usikivu wetu na kupoteza kuona vilivyoko nje, tutapoteza uwezo wa kushika kusudi la wokovu wetu wenyewe. Kama kanisa halitaona nje ya

kuta zake (ulimwenguni), litakuwa limekataa sababu yake ya msingi ya kuwepo hapa ulimwenguni.

Hatukuokolewa kwa ajili ya nafsi zetu. Ikiwa kusudi lote la wokovu wetu lilikuwa ni hilo basi ungeenda mbinguni moja kwa moja; basi kwa nini isiwe kuokolewa tu na kupinduka na kufa? Kwa nini usijinyonge? Unapoteza tu hii hewa. Kwa nini ubaki hapa duniani? Nenda. Basi nenda mbinguni na utakuwa umetimiza Agizo Kuu!

Aha, lakini hukufa mwili wako, je ulikufa? Hii inahusiana na kitu kingine zaidi ya wokovu wako binafsi. Tumepokea hii karama ya wokovu ili tuipeleke kwa wengine. Hii ndio kwa nini tunaendelea kuishi hapa duniani!

Madhababahu zetu ziko tupu, bado tunaupuuza wosia mkuu wa mwisho la Mwokozi wetu aliyeyatoa maisha yake kwa ajili ya hizi nafsi ambazo tumezifukuza.

## Huruma, Siri ya Uamsho

Mara nyingi, mimi husikia kwa watu wanaowahi kuthibitisha ukosefu wa nguvu kwenye makanisa yao wakitaja matendo mema yote wanayofanya. Kwamba wanaendesha huduma ya kusindika vyakula kwenye makopo kwa ajili ya maskini, kuongoza huduma za michezo ya watoto siku za Krismasi, na kujitolea kwenye shughuli za kijamii. Yote haya ni matendo mema lakini siyo dalili ya uamsho.

Kuna matendo mema mengi tunayoweza kuyafanya, na yatupasa kuyafanya, sisi kama Kanisa la Yesu Kristo. Wapagani pia hufanya mema hayo hayo, lakini hii haimaanishi wamejawa na Roho wa Mungu. Huruma, huruma ya kweli, ni zaidi ya matendo mema. Huruma ni kuitoa nafsi ya mtu kwa upendo ili kwamba nafsi zingine ziweze kuokolewa. Ni kipengele muhimu cha Ukristo, ni  maana halisi ya Msalaba. Shabaha kuu ya huruma ni kuziokoa nafsi na kuzijenga. Huruma ya kweli inapokuwepo kanisani, waumini huwaleta waliopotea kusikiliza injili. Kama huruma haipo, hakuna hata mmoja atakayepondeka moyo wala kubeba mzigo kwa ajili ya waliopotea, na madhabahu zitaendelea kuwa tupu.

Yesu ametuamuru kuwaalika siyo tu marafiki zetu kwenye karamu/sherehe zetu bali pia maskini, vilema, viwete, vipofu (Luka 14:13). Hata hivyo, wengi wetu tunapoangalia kwenye ushirika wa kanisani kwetu, wote tuwatazamao ni nyuso za zamani zile zile tunazoziona kila juma. Tumefanya karamu zetu na kuwaalika marafiki zetu, lakini hatujafikiria kuhusu vipofu, vilema, viwete na maskini kama ambavyo Yesu ametwambia kufanya. Kama hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa lako, basi kuna ukosefu wa huruma, na hakika hakuna uamsho.

Nabii Amosi alitumia mfano wa picha ya watu wanaostarehe na kwa urahisi kabisa, wanafurahia baraka za kuwa hai, lakini hawana huzuni kwa ajili ya

waliopotea wanaoangamia (Amosi 6:1-7). Hulala juu ya vitanda vyao vya pembe za ndovu lakini hawahuzuniki kwa sababu ya mateso ya watu wao. Kulingana na msitari wa 7, watakuwa wa kwanza kuhukumiwa, kwa sababu hukumu lazima ianze katika nyumba ya Mungu. Hili suala la kutookoa wengine siyo suala la kuchagua bila kupokea matokeo yake. Kama haupelekwi na huruma kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea, kuwasha moto katika kanisa lako na kuanzisha tena bubujiko la chemchemi kutoka kwa Mzabibu wa Kweli, ndipo utakapokabiliana na ghadhabu ya Mungu kwa sababu hukujali kuhusu nafsi ambazo Bwana aliwafilia ili awaokoe.

Huruma inahusiana na kuwaokoa waliopotea. Yesu alikuwa ni Huruma katika mwili na alikuja kuwaokoa wenye dhambi. Hicho ndicho alichokifia msalabani. Huruma, kwa hiyo, ni zaidi ya hisia na mawazo; inahusiana na vitendo. Paulo aliwaambia Wakorintho kwamba naweza kuwa na karama zote za Roho—unabii, hekima, maarifa na imani—lakini kama sina upendo, mimi si kitu (1 Wakorintho 13:2). Umuhimu wa huruma [upendo] umefichwa ndani ya kwenda kuziokoa nafsi.

Itakugharimu nini kufikia kwenye kutambua kwamba jambo fulani limepungua kanisani kwenu? Makanisa katika nchi ya Marekani yamekuwepo kwa miaka mingi bila kuwa na uamsho wa kweli ambao tumeupuuza unaoashiriwa na ishara mbaya za kifo

chetu na kujitetea bure kunakotupima pamoja na makanisa mengine yaliyokufa ili kujishawishi wenyewe kwamba tuko sawa.

Kama unataka kuwa kama dunia inavyosema "kawaida" na kuanza safari rahisi ya kubweteka katika Ukristo, basi kamwe hautaziona nguvu za Mungu maishani mwako. Bali kama unataka kuziona nguvu za Mungu kwa kiwango cha kushangaza na cha juu sana, lazima kwanza kuutambua ukweli kwamba kanisa halina uamsho.

Ni kwa huo tu ndipo utaziona nguvu zisizo za kawaida zikitokea ambazo zitakuwa zikiongelewa katika umilele wote.

## Mwanamke Aliye Tasa

Ndani ya Biblia yote, kuanzishwa kwa ndoa kumeelezwa kama mfano wa mahusiano kati ya mwamini na Mungu. Yesu Kristo ni Bwana-Harusi; kanisa lake ni Bibi-Harusi. Kila jambo tangu uchumba mpaka kuzaa watoto lina alama yake katika mahusiano yetu na Mungu. Ni kama vile Mungu ametupatia mfano katika namna ya kuishi, jambo ambalo ni la muhimu sana katika mahusiano yetu hapa duniani, kama kikumbushi chetu cha kudumu na cha lazima kuhusu maisha yanamaanisha nini. Ndoa haihusiani na kufanya tendo la ndoa tu. Wala siyo tu kuhudumiana, kutunza nyumba katika usafi na kutandika vizuri kitanda, kupika chakula, au kumwaga nje uchafu. Mambo hayo

yote yana mfano katika kutembea kwetu na Mungu, bali kusudi kuu la ndoa ni kuzaa watoto na kuongezeka na kuijaza nchi. Mungu alitoa agizo hili kwa watu wengi wa Agano la Kale, akianza na Adamu, kisha wengine kama vile Nuhu, Ibrahimu na Yakobo.

Kama ilivyotaja katika Mwanzo sura ya 2, mke alipokuwa tasa katika Agano la Kale ilichukuliwa kuwa ni aibu kwake. Leo, tukiwa na wanawake wengi wasomi, kujenga familia hakufanyiki kwa kuzingatia umuhimu wa ndoa kama ilivyokuwa mwanzo. Lakini pamoja na kwamba haifanyiki hivo leo, mfano huo bado unabaki pale pale ukieleweka: mke alikuwa na wajibu wa kuzaa watoto na kuwalea mpaka wakue ikiwa ni kipaumbele kwake. Wajibu huo huo umewekwa katika kanisa, ambalo ni Bibi-Harusi wa Kristo, kwenye ulimwengu wa roho—kumzalia Kristo watoto wa kiroho na kuwalea.

Nimeweza kuwasikiliza Wakristo kadhaa wakijitetea wenyewe kuhusiana na kuokoa nafsi kwa kusema kwamba tunda tunalotakiwa kuzaa ni tunda la Roho tu (Wagalatia 5:22). Mimi nakataa. Hilo tunda ni matokeo ya Roho Mtakatifu anapofanya kazi ndani ya waamini, siyo wajibu wetu wa kutimiza. Agizo Kuu halitudai kuwa na tabia njema, bali kwenda na kuziokoa nafsi. Urahisi wa Injili umegeuzwa kuwa mgumu kwa kujitetea kusiko na majibu pale tunapokataa kusalimisha njia zetu za starehe za maisha na kupiga hatua ya kuutii wito wa Mungu.

Mifano miwili ya ajabu ya kutaka utauwa ili kuleta matunda inaweza kuonekana kwa wanawake wawili wa Agano la Kale. Hana na Raheli wote walikuwa ni wanawake tasa waliomwomba Mungu ili kukwepa aibu ya ndoa isiyozaa. Aibu ilikuwa wazi kwao, ingawa wote walikuwa ni wake waliopata kibali kwa waume zao. Kwao kusudi lao maishani halikuwa kupewa upendo na wenzi wao bali kuwa na watoto. Suala la kukosa watoto halikuwa kuashiria thamani ya utu wao bali kuathiri heshima ya waume wao. Hivyo, yatupasa kumpa heshima Kristo kwa kuokoa nafsi [kuzaa] na kuzilea katika yeye.

Leo kanisa limekuwa mwanamke tasa. Haijalishi jinsi gani liko vizuri, jinsi gani ni tajiri, au jinsi gani lina ujuzi kiasi gani linaloumudu. Ikiwa kanisa haliokoi nafsi, limekuwa mwanamke tasa. Tunaonekana kuwa na uwezo wa kuinua majengo makubwa ya kuvutia kuonyesha mafanikio na maisha ya kanisa letu, lakini tunatumia muda mchache sana kutafuta nafsi ili kuyajaza. Ni rahisi sana kujenga vituo vya kufanyia mazoezi (jimu) na maduka ya Kikristo ya kuuza kahawa kuliko ilivyo katika kuwashuhudia uso kwa uso watu wasiookoka. Imekuwa ni njia ya sisi kukwepa maswali. Tunatumaini bado tunaweza kuwa mashahidi bila kujiingiza sisi wenyewe kwenye hii shida binafsi.

Je hilo si kweli? Huoni yanayoendelea karibu nawe? Lini ilikuwa mara ya mwisho kwako au kanisa lenu kwenda mitaani kushuhudia kwa wengine na

kuwaambia kuhusu wokovu? Na bado amri ya Yesu iko wazi, toka nje uende kwenye njia kuu na vichochoro na kuwashurutisha kuingia ndani ya nyumba ya Baba ili nyumba ya karamu/sherehe ya chakula cha harusi ya Mwanakondoo ijae (Luka 14:23). Nini ambacho kinakuzuia usiitii hii amri? Kama ni kuwaogopa wanadamu, basi haumwogopi Mungu. Kama unaona itakuwa shida, basi utakuwa hauna upendo mkuu sana kwa waliopotea. Kama unajitolea mno kwenye masuala ya kijamii, basi umefungamana sana na hii dunia. Kama unafikiri una wazo jema sana juu ya jinsi ya kuokoa nafsi, basi unahitaji kujifunza kwamba huwezi kuitengeneza mwenyewe njia yako ya kwenda mbinguni. Ni jambo rahisi tu la kiimani na utii. Kumbuka, utii ni bora kuliko dhabihu, bali uasi ni kama dhambi ya uchawi (1 Samweli 15:23). Naamini jambo kubwa linaloturudisha nyuma kutoka kuwa mashahidi halisi ni ukosefu wa shauku. Hatumiliki huo moto wa hamasa ambao utatutawala bila kujali changamoto ya kuwaambia wengine kuhusu mambo mazuri ambayo Mungu anafanya kanisani kwetu na nini anaweza kuwafanyia pia.

## Kilio cha Raheli

Ni jambo mojawapo kutambua kwamba hamna uamsho unaowaka moto katika kanisa lenu, lakini ni jambo tofauti kabisa kuhusu kuuhitaji. Inaweza

kuonekana kwamba mambo haya mawili yanakwenda pamoja, lakini sivyo.

Akitaka kuzaa watoto, Raheli aliomba:

*Nipe wana, kama sivyo nitakufa mimi. (Mwanzo 30:1)*

Raheli alikuwa haombi baraka kwa ajili ya nafsi yake; alikuwa na huzuni kwa ajili ya nafsi zingine. Jambo hili wengi wetu wamelikosa. Kusudi letu kubwa maishani siyo kuhusu sisi; ni kuhusu wengine. Hili siyo kuhusu uamsho unaokusudiwa kutafuta uamsho wala Mungu kututembelea ili tujisikie vizuri sisi wenyewe. Ni ushawishi wa ndani kabisa mioyoni mwetu tunapoona kwamba nafsi zinakwenda kukaa jehanamu ikiwa hatutafanya jambo ili kuzuia hilo lisitokee.

Je una huzuni kwa ajili ya uamsho? Kama Raheli, unataka kufa kwa ajili ya uamsho, kuyatoa maisha yako ili kuziona nafsi zikiokoka? Chochote kilicho pungufu ya hicho ni kama shaba iliayo au malimba ivumayo bila maana: makelele mengi lakini hakuna kitu. Au kama Petro anavyoelezea kuhusu hili, kwamba, ni kama visima visivyo na maji na mawingu yasiyo na mvua (2 Petro 2:17). Tunasema tunahitaji uamsho katika makanisa yetu kwa sababu tunafahamu tunapaswa kuwa nao, lakini ni kwa jinsi gani kweli tunautaka? Gharama ya uamsho wa kweli iko juu sana kuliko mwili wa kibinadamu unavyotaka kuomba. Inahitaji Roho wa

Mungu kutuleta kwenye hiyo nafasi ya kuacha matamanio binafsi, ambayo itatufanya tuweke pembeni mambo yetu mazuri ili kubeba juu yetu mateso ya mwili wa Kristo ambayo Neno la Mungu linatuita kuyashiriki.

Jambo hili siyo mateso ya akili isiyotafuta mateso bali ni kujitoa wenyewe, vyote kiroho na kimwili, ili kuona sababu kuu ya Kristo kutawala kwa ushindi. Kwenye kitabu cha Ufunuo, Mungu hatukemei kwamba wale wanaojaribu ndio watakaokula katika Mti wa Uzima bali ni wale washindao. Kikwazo kikubwa kinachotukabili ni tamaa zetu za mwili. Tunahitaji kuvuka mambo ya kawaida na starehe na kuingia kwenye kutembea na Mungu ambaye amezisulubisha hizo tamaa za mwili ili tuweze kutembea katika Roho wa Mungu. Hii ni changamoto Mungu ametupatia ili kujaribu hatima yetu. Hii hutenganisha kondoo na mbuzi na kuinua wanaume na wanawake halisi wa Mungu kutoka madaraja ya watu wa kawaida.

## Uvivu na Upinzani Kwenye Mabadiliko

Watu wengi kwa kawaida hawapendi mabadiliko. Mara tu wanapopanga mambo kwa namna wanayofikiri, ndivyo walivyo, huyatetea kwa ukali. Makundi mengi ya watu hupenda hisia ya kujifungia kwenye kuta zinazowabana ili wajisikie salama. Uvunjaji wowote wa usalama huo unapojitokeza huathiri namna ambayo wamepanga mambo yao

kwenye akili zao. Wana shida nyingi za kutembea bila kuwa na msingi imara chini yao, hivyo huona kuwa ni rahisi kushika desturi za liturujia ambazo wanazitumia kuliko kuzivunja kwa ajili ya jambo ambalo linaonekana halijajaribiwa na lenye kuleta mapinduzi. Hubakia katika "kanisa kama kawaida," na hubakia kuwa viriba (chupa) vikuukuu vya divai ambavyo haviwezi kutatuka/kupasuliwa na divai mpya.

Tatizo ni, misingi waliyokwishaijenga ina msingi wake kwenye wazo lisilo sahihi. Dini ni mfano wa kimwili unaowakilisha kutembea kwetu na Mungu, lakini kama tutatunza mambo ya mwilini ili kulinda mambo ya rohoni, tutajikuta tunabakia mikono mitupu. Imani ni hakika ya mambo *yasiyoonekana*, na ni bayana ya mambo *yatarajiwayo* (Waebrania 11:1). Kama matarajio yako yameshikilia kwenye mambo unayoweza kuyaona kwa sababu huwezi kushika yale usiyoyaona, basi itakuwa ngumu kwako kuhamasisha mabadiliko yasiyo ya kawaida katika kanisa.

Na tuone habari ya Lazaro (Yohana 11:1-46) na jinsi inavyohusiana na kifungo cha desturi za kidini. Lazaro alikuwa amekufa, lakini Yesu alipofika, alimwita Lazaro atoke kwenye kaburi lililokuwa limefunikwa kwa jiwe kubwa, atoke kwenye kifungo cha sanda katika mikono na miguu cha desturi ya kidini. Uso wake pia ulifungwa kwa sanda hivyo hakuweza kuona. Yesu aliagiza jiwe liondolewe na akamwita Lazaro atoke nje ya kaburi akatoka, lakini pia aliwaamuru wanafunzi wake

wamfungue hilo vazi lake la kaburi (sanda) na kumwacha huru. Inahitaji mkono wa Mungu kuliondoa hilo jiwe la kidini na kuliita kanisa lije kwenye nuru, lakini ni wajibu wa wanafunzi wake aliowaamuru kulifungulia kanisa kutoka kwenye desturi zinazooza zinazolifunga. Tunahitaji kuwabeba hawa watu kwenye maombi, kwa sababu ni Mungu pekee ndiye mwenye kuwahakikishia kuyaacha mavazi magumu ya desturi za zamani. Kuna waamini walio wavivu sana kuhitaji uamsho. Mjinga yeyote hufahamu kwamba kutafuta uamsho inatamkwa kama K-A-Z-I, lakini baadhi ya watu hawajali hata kama ni kwenda mbali kwa kiwango hicho. Hawajali kama kuna mtu mwingine anafanya hiyo kazi au la, lakini usiwaulize kuusulubisha mwili wao, hasa kwa yule ambaye hujawahi onana naye. Hawajali hata kama ni kuomba, lakini si kukesha usiku wote, hasa pale inapofanyika si kwa ajili yao. Hawajali ushuhudiaji hasa kwa mtu aliyekwishaokoka na hukubaliana nao, lakini usiwaambie kutoka kwenda kwenye njia kuu na vichochoro kuwashuhudia waliopotea. Wanashikilia wokovu wa kuwakilishwa ambao huchukulia wanaweza kushikilia kwenye mkoti wa mchungaji ili awakokote mpaka mbinguni. Lakini ikiwa unajificha kwenye kiti cha nyuma ya kanisa, kamwe hutaweza kujificha mbele ya fimbo ya hukumu ya Mungu.

Nilipokuwa mtoto mchanga katika Bwana, nilimwuliza kwa nini baadhi ya watu wanaokolewa na

wengine hawaokolewi; kwa nini baadhi ya watu hubakia kwenye wokovu, na kwa nini wengine wanashindwa. Aliongea nami moja kwa moja: *Baadhi ya watu hujali, na wengine hawajali. Ni rahisi namna hiyo.*

Hilo lilikuwa ni moja ya mambo ambayo nilikuwa sijayasikia. Ni kweli kwamba maji hutafuta kina na kimo chake. Mtu yeyote anaweza kuutambua uhitaji, lakini kama kweli hatujali, daima tutabakia nyuma tu kwenye kiwango ambacho tunajisikia kuwa vizuri. Hata hivyo, kama tunahitaji uamsho, tunapaswa kujali sana kwenda zaidi ya tamaa zetu za mwilini. Kama tunajaribu kuinuka juu kuliko kimo chetu cha matamanio bila Roho wa Mungu kuwaka ndani ya mioyo yetu, haitatuchukua muda mrefu kabla hatujarudi tena nyuma na kushuka chini hadi kwenye hicho kimo ambacho tunajisikia vizuri. Ni Mungu pekee ndiye anaweza kutupatia uwezo huo, na ni juu yake kwamba tutafute nia ya kuvunja hali yetu ya kubweteka.

Lakini yatupasa kumwomba Mungu kwa ajili ya jambo hilo.

Imeandikwa kwamba kama mtoto atamwomba baba yake mkate, atampa jiwe? Baba yenu wa mbinguni hatawapa Roho Mtakatifu wale wamwombao? (Luka 11:11). Kwa hiyo, dhambi zetu zitakuwa ni zile ambazo hatukujali sana kuomba, na kuomba sana kwa bidii. Kama tuliomba, hakika Mungu angetupatia nia na nguvu za kubeba mzigo aliotuagiza kuubeba. Kama

ilivyokuwa kwa baba mwenye mtoto aliye na roho chafu alivyomwomba Yesu kumsaidia kutokuamini kwake (Marko 9:24), ndivyo itupasavyo kumsihi Mungu kutuingizia nia isiyokwisha mioyoni mwetu kwa ajili ya uamsho. Tunaweza tu kuwa miili, lakini Mungu anaweza kuweka huo mzingo mkubwa mioyoni mwetu kwa ajili ya uamsho, utakatifu, na kwa ajili ya nafsi zilizopotea, hali ambayo itatufanya tusiwe hivi tulivyo. Kama hatuombei mzigo huo, haitatuchukua muda kabla hatujaanguka tena mpaka kwenye kimo chetu cha chini.

Wakati hatua ya kwanza kwenye uamsho ni suala la kuutambua ukweli, naamini kwamba kumtafuta Mungu kwa ajili ya hitaji la uamsho ni jaribio la kwanza ambalo lazima tushinde. Unatakiwa kuhitaji uamsho sana hata kuwa na huzuni kwa ajili yake. Hakuna mbadala kwako, na hakuna mlango wa nyuma wa kujitetea uamsho usipokuja. Nafsi yako inapaswa kujikokota kutoka kwenye uzembe na kuwa na shauku ya moto ambao hautazimika mpaka uamsho umekuja. Ni Mungu pekee ndiye atakayekupatia jambo hilo. Haliji lenyewe; ni kwa neema ya Mungu tu. Kwa hiyo, yatupasa kuutafuta uso wa Mungu kwa ajili ya hilo.

Tunauanza mchakato wote kwa kumwomba Mungu kutusaidia katika udhaifu wetu na kuiweka mioyo yetu tayari kwa kuupokea na kuuwasha moto. Kama kweli tunamaanisha, tutaendelea katika maombi mpaka tuupate uamsho. Tukikata tamaa kabla ya kujibiwa, basi tutaupoteza huu wito aliouweka juu yetu,

na tutakuwa tumechagua kushindwa siyo tu Mungu pekee yake bali pia sisi wenyewe na zile nafsi nyingi za wengine zisizohesabika ambazo zingekuja kwenye wokovu kupitia sisi.

Mungu hatazileta nafsi za thamani kwenye kanisa lisilojali sana kufunga na kuomba kwa ajili ya watu waliopotea. Kama atafanya hivyo, watakufa mapema, kwa sababu hakuna atakayechukua mzigo wa kuzimwagilia, kuzitunza, na kuzisaidia nafsi zao kukaa na moto unaoendelea kuwaka. Lakini kama watu wa kanisa wana nia inayowaka moto na kuvunjika katika roho zao, kufa nafsini mwao, na kuutafuta uso wa Mungu kwa ajili ya nafsi za wengine, basi Mungu atakapozileta hizo nafsi, watazithamini kama zawadi ya thamani waliyoitaabikia.

Tunapoushinda uvivu wetu na hali ya kufifia kwa maono yetu ili kupanua maono yetu zaidi ya upeo wetu, tutamwona Mungu ambaye amekuwa akitusubiria kumwamini katika mambo makubwa yasiyo ya kawaida. Hizi ni nafsi zenye imani ambazo Mungu anaweza kuzitumia baadaye kuleta uamsho. Wanaozimia, wasioamini, na waoga kamwe hawataweza kukwea sana hadi juu ya kilele cha Mlima Pisiga kuitazama nchi ya ahadi ya uamsho.

Tunainuka kwenye changamoto ya Mungu tu kwa neema yake ili kwamba kila kitu kitakapokwisha kunenwa na kufanyika, Mungu pekee ndiye apewe utukufu wote.

# Sura ya 5

# Hatua ya 2: Toba

*"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." (2 Nyakati 7:14)*

Andiko hili limenukuliwa kwa umuhimu, huhubiriwa ili kutumiwa kama tangazo la kilio kwa ajili ya uamsho, lakini ili kuiweka nchi yetu kwenye hatua hii, watu fulani wanapaswa kusugua magoti yao. Inapaswa ianzie mahali fulani. Hakuna uamsho utakaokuja bila toba.

## Wito Kwenye Utakatifu wa Mtu Binafsi

Kila uamsho katika historia ulitanguliwa na wakati wa toba ya kujitoa kutoka ndani ya moyo ambayo hupelekea kuwepo na utakatifu katika kanisa lote. Kabla ya mtembeo wa Mungu kuanza kufanya kazi katika kanisa, lazima Mungu akute kuna msingi safi na mtakatifu ili asimame mahali hapo. Kama tunatafuta mtembeo usio wa kawaida wa Mungu, hekalu letu lazima lisafishwe mbali na dhambi ili kuupokea uwepo wake. Mungu hatashirikiana na dhambi.

Toba ya namna hii haiwezi kuwa bandia. Huwezi kutamka maneno kwa sababu unafikiri hivyo ndivyo unavyotakiwa kufanya au hata kutaka kufanya. Inatakiwa kufanyika kwa upendo, toba inayofurika sana ambayo inatoka ndani ya nafsi yako. Hii siyo kupayuka payuka mbele za Mungu kwa ajili ya kuweka sawa jambo kwa kutia kiraka kitu cha kijinga tulichokifanya. Hii ni kama vile kwamba hakuna kilio kingine cha kuomba kusamehewa ambacho tumeshawahi kulia, na lazima kiwe kweli kama kweli tunataka kuyafikia masikio ya Mungu aliye mtakatifu.

Paulo ametuonya kuhusu kumaanisha juu ya dhambi:

> *Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. (Waebrania 10:26-27).*

Hatuwezi kupumzika kwenye uzoefu wa wokovu wetu wa kwanza. Maisha yetu lazima yaonyeshe kutembea daima katika utakatifu mbele za Mungu, na kushindwa kwetu lazima kuonekane tofauti na huo utakatifu. Huu udhaifu katika maisha yetu lazima uletwe kwenye nuru ya hukumu na rehema ya Mungu ili kusafishwa kikamilifu na kusamehewa ili mifereji yetu iwe "imfaayo Bwana" (2 Timotheo 2:21).

Toba ya kweli kama hiyo inayolihusu kanisa lote, dhambi zisizo na madhara zitakuwa ni uovu zinaposimama kinyume na utakatifu wa Bwana Mungu Mwenyezi. Kadiri uwepo wa Mungu unavyotusogelea, ndivyo hizo dhambi zitakavyoonekana kuwa nyeusi mpaka nuru ya utukufu wa Mungu inayopofusha itakapofichua kila pembe yenye giza ndani ya mioyo yetu. Baadaye kidogo tutauhisi uzito wa dhambi zetu jinsi ulivyo mzito ambao hatutaweza kusugua magoti yetu sakafuni kwenye maombi kwa ajili ya msamaha kama vile mzigo huo haukujulikana kabla.

Nimewaona Wakristo kwenye huduma za uamsho pale ushawishi wa Roho Mtakatifu ulipochukua nafasi, ukiwinda bila kupingwa na mambo ambayo hapo kabla yalionekana kuwa ya kawaida kama sehemu ya maisha. Nuru ya utukufu wa Mungu hupofusha, na hata giza dogo sana huonekana kutofautishwa na nuru. Toba inapofanyika kamwe watu hawataendelea kusimama wamejitenga na Mungu kwamba dhambi ibaki kuwasababisha hivyo. Hatia hugeuka kuwa mzigo mzito kwamba wanatakiwa kutubu wakitembea kwa hatua ndefu ndefu za vilio kutoka moyoni, wakiungama kwa sauti kwenye ushirika mambo ambayo kamwe hawakuwahi hata kuyafikiria kabla, kwamba ni makosa.

Kuna jambo kuhusiana na huku kuungama kutoka ndani kunakotusafisha, huwajaza watu na furaha ya kuwekwa tena huru ambayo hung'ara kutoka kwenye nyuso zao. Kuzifunua hizo siri za dhambi zao huleta

uhuru ambao watu walio wengi hawakuwahi kuuona kabla, na mzigo wao hudondoka chini yao ambao hawakuwahi kuuona kama waliubeba kwa muda mrefu sana. Toba hii huweka watu huru. Kamwe hawataendelea kusubiri kumwambia kila mtu, na kamwe hawatajali kile mtu yeyote atawaambia kilicho kinyume. Wako huru!

Bila huo uhuru wa kujitakasa, Mungu hawezi kututembelea. Kama hatuko watakatifu, mtembeo wa Mungu utakwama kwenye tabaka la matope ambalo hufunika nafsi zetu zinapokuwa na dhambi. Chini ya sheria ya Walawi, madhabahu kwanza ilitakiwa kutakaswa kwa damu kabla haijawa takatifu kufaa kupokea dhabihu kwa ajili ya Bwana. Mara baada ya dhambi zote kufagiwa katika kanisa na hewa chafu ya kubweteka kutolewa nje ya madirisha, madhabahu sasa inaweza kutakaswa, na hema kusafishwa. Sasa, na ni sasa hivi, Mungu aweza kukaa ndani ya kanisa lililo katika utakatifu mkamilifu na linaloandaa sadaka zisizozuiwa za nafsi zetu kwake katika ibada.

Huo uhuru wa kuondoka kwenye kila kivuli cha dhambi hutupatia ujasiri na nguvu mpya ya imani kwetu sisi waamini. Kwa sababu wenye haki ni wajasiri kama samba (Mithali 28:1), utakatifu huu wa hali ya juu sasa huinua imani iliyosafishwa kama dhahabu kwa wanaume na wanawake walio na ujasiri wa kutembea ndani ya chumba cha enzi, wakiunguruma katika imani ya askari kuomba haki zao kwenye kiti cha enzi cha

Mungu. Hawa siyo kondoo waoga wanaomwogopa na kumwonea haya Bwana wao bali ni askari wa Mungu wanaosimama katika haki ili kushikilia pembe za madhabahu na kudai ahadi za Mungu na hawataziacha ziende mpaka Mungu amewatembelea.

Ni kwa imani ya namna hiyo ndipo Mungu hupendezwa na amejifunga kwa Neno lake mwenyewe ili kuitikia kwenye wito wa namna hii wa uamsho. Yeye yampasa ajibu kwa sababu ni haki ya waamini, na wanaume na wanawake ambao wamefikia kiwango hiki cha imani wanaifahamu na hawatakataliwa.

Toba huleta haki, na haki huiweka huru imani, na imani huhamisha milima. Sasa tunaweza kusimama mbele za Mungu na kudai ukamilifu wa ahadi zake kwetu na kutambua kwamba kwa sababu tuna haki mbele zake, yampasa atujibu. Uamsho unakuja. Tunaufahamu. Tunaudai. Sasa tunayo imani ya kumwamini Mungu kwa ajili ya uamsho. Uamsho utakuja.

Haki huvutia ahadi za Mungu.

## Toba ya Ushirika

Toba binafsi hujenga msingi wa toba ya ushirikiano. Kwa uwazi toba huletwa na mahusiano mapya binafsi na Mungu, ni rahisi kuona umbali tulikofika katika kuanguka kwetu. Sasa ndipo tutafahamu ni kiasi gani siyo tu sisi bali taifa zima, makanisa yetu, na watu wetu walivyojitenga na Mungu.

Mambo ambayo yalionekana kuwa ya kawaida au ya kupita hapo kabla, sasa yatatiwa rangi ya vivuli vya giza ambavyo vinaweza tu kuonekana kwenye mg'ao wa nuru ya Mungu. Tutashangaa kwamba hutukuyaona haya kabla, lakini ni kwa sababu tulitumikia kwa muda mrefu utusiutusi/zama za kale zisizobadilika zilizokuwa zikitambaa kuingia katika makanisa yetu.

Kama tunataka uamsho ambao utafika hadi nje ya milango ya makanisa yetu, yatupasa kumtafuta Mungu ili alete huo msamaha kwenye nchi yetu. Kivuli cha ukengeufu kinaning'inia juu ya taifa letu kama wingu jeusi, na lazima tuombe kwa ajili ya Mungu kutusamehe sote. Hapa ufunguo ni kutambua kwamba tuliishi kama watu ambao sasa tunajiona hatuangaziwi. Wengi wa majirani zetu, wananchi, na wapendwa wa makanisa yetu wanahudhuria kama tuonavyo sasa kwenye kumbi za dini za gizani. Wao pia wanahitaji kujionea huu uzoefu wa toba ambao tutakuwa tumeupata. Mzigo wetu kwa ajili ya nafsi zilizopotea huanzia hapa kwenye toba. Mioyo yetu inapaswa kupondeka kwa ajili ya wale wanaoteseka chini ya blanketi za ukengeufu ambazo sisi tumetoka.

Yesu alimuita Lazaro kutoka kaburini, lakini aliwaita wanafunzi wake kumfungulia atoke kwenye mavazi ya kaburi ya desturi za zamani za kidini (Yohana 11:43). Hivyo sisi pia tumeitwa kuliombea kanisa. Kutazama zaidi ya utofauti wa kidhehebu,

tumeitwa kuombeana sisi kwa sisi. Uamsho unapokuja, huwa hauna ushirika na wengine wasiohusika katika kanisa.

Hukumu itaanza katika nyumba ya Mungu, na hivyo maombi yetu na yawe kwa ajili ya kuomba rehema kwanza.

## Maombi ya Toba ya Danieli

Habari ya urejesho wa Yerusalemu ni moja ya kumbukumbu kubwa zenye maelezo marefu kuhusu uamsho katika Biblia. Nafasi ya kitabu hiki haitoshi kuelezea mengi kuhusu anguko la Israeli, vilio vya manabii, na hukumu za Mungu, lakini inatosha kusema, kwenye kila hukumu ya Mungu daima kuna mbegu za uamsho utakaofuata. Danieli alikuwa ni mmoja wa hizo mbegu.

> *Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake, mimi Danieli, kwa kuvisoma vitabu, nalifahamu hesabu ya miaka, ambayo neno la Bwana lilimjia Yeremia nabii, ya kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu, yaani, miaka sabini. Nikamwelekezea Bwana Mungu uso wangu, ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu. (Danieli 9:2-3)*

Isaya, ambaye alianzisha mchakato wa Koreshi kutoa tamko, pia alikuwa ni mbegu ya uamsho. Esta alikuwa ni mbegu nyingine tena ambaye alimtia moyo Artashasta kuthibitisha tamko la kuurejesha Yerusalemu, pamoja na Nehemia, Ezra, na wengine. Unabii uliandikwa, mchakato ukaanzishwa, mbegu zikapandwa, lakini alikuwa ni Danieli ambaye aliuombea uamsho.

Usomapo neno kutoka kwa Mungu katika Maandiko Matakatifu, utatambua kwamba ni kweli. Maneno Imeandikwa; Asema Bwana Mungu; lazima yatatimia. Danieli alisoma kwenye kitabu cha Yeremia kwamba uhamisho katika Babeli ungekoma baada ya miaka sabini ndipo Mungu angewarejesha Israeli katika Yerusalemu. Wana wa Israeli walikuwa wamekaa mbali na haki ya Mungu na walikuwa watumwa katika nchi ya Babeli kama matokeo ya uasi wao, lakini hapa katika Yeremia kuna ufunuo wa rehema kubwa kutoka kwa Mungu! Miaka yote sabini ilikuwa inakwisha, na Danieli alitambua urejesho ulikuwa umefika. Uamsho ulikuwa unakuja kwa sababu Mungu alisema hivyo miaka sabini nyuma! Ingawa ilikuwa imeandikwa katika Neno la Mungu na wakati wa huu uamsho ulikuwa juu yao, je Danieli angewaita marafiki zake kuja kuimba na kufurahi? Je wangesherehekea tumaini hili jipya la urejesho? Hapana, Danieli alikuwa ni mmoja wa watu wenye hekima waliowahi kuishi, na

alitambua kwamba ingawa ilikuwa imetabiriwa katika Neno la Mungu, bila toba kusingekuwa na uamsho.

Ili kuchukua huu wito wa ajabu wa kurudi kwenye neema ya Mungu, toba ilitakiwa kutafutwa, siyo na mtu mmoja kibinafsi, bali katika ushirika, kwa ajili ya watu wote wa Mungu.

Watu fulani walipaswa kusugua magoti yao, na Danieli alikuwa mtu. Maombi yake ya msamaha kwa ajili ya watu wake ni moja ya maombi marefu katika Agano la Kale (Danieli 9).

E.M. Bounds, mwandishi wa vitabu kuhusu maombi anayeheshimika sana, aliandika kwamba Mungu hatafanya kitu chochote bila maombi ambacho anaweza kukifanya kupitia maombi. Jinsi gani ni kweli. Mungu anaweza kufanya, lakini hatafanya. Anatumia mwili. Sisi ni mwili wake, mikono na miguu yake katika kupeleka Injili hapa duniani. Ni imani yetu ndiyo inayohamisha milima na maombi yetu ndiyo yanayomfanya Mungu atutembelee. Mpango wa Mungu ni kwa ajili yetu kuwa vyombo vya rehema yake na kufuata kielelezo cha Mwanae, Yesu Kristo.

Kadiri tunapoutafuta uso wa Mungu kwenye toba kwa ajili ya watu wetu, ndivyo tunavyoondoa laana na kufungulia mlango ili kuruhusu urejesho kuanza. Maombi hukunjua mikono ya Mungu.

## Nehemia

Nehemia pia alitambua umuhimu wa toba katika kuzaliwa kwa uamsho. Alilia aliposikia jinsi Yerusalemu unavyokaa katika hali ya kubomolewa. Huu ulikuwa ni mji wa Mungu. Ulitakiwa kuwa mzuri na kujengwa kama makumbusho ya utukufu wa Mungu, lakini ulikuwa umeharibiwa kwa sababu ya dhambi za watu wake, watu wa Mungu. Moyo wa Nehemia ulipondeka.

Nehemia alikuwa ni mnyweshaji wa mfalme, ambaye kazi yake ilikuwa ni kuonja na kuhakikisha divai, ambayo ilichukuliwa kuwa na umuhimu mkubwa katika jamii hiyo, haikuwa tu salama bali yenye ladha nzuri. Mnyweshaji wa kifalme ilikuwa ni kazi yenye jukumu kubwa, mamlaka, na heshima na ilihitaji mtu anayeaminika vizuri. Akiwa kama mnyweshaji wa mfalme, alikuwa na uwezo wa kuonana na mtu ambaye angetoa amri ya kuujenga mji, lakini hata hivyo, pia alitambua kwamba bila toba kwa Mungu kwa ajili ya dhambi za watu ambazo zilisababisha huu uharibifu wa mji, ombi lake kwa mfalme lingekuwa batili. Usiku na mchana, Nehemia alifunga na kuomba kwa Mungu kuwasamehe watu wake na kumpatia kibali alipopeleka hitaji lake mbele za mfalme.

Hayo ni maombi ya kumaanisha—mchana na usiku, kufunga siku nzima, kuhuzunika kwa ajili ya kutafuta majibu kutoka kwa Mungu. Kuna nyakati

ambazo wewe huwezi kukubali jibu la "labda" kutoka kwa Mungu. Inapokuwa lazima upokee jibu bayana kutoka kwa Mungu, basi utauweka mwili na vitu vingine pembeni ambavyo vinasimama njiani ili kujiweka mwenyewe mbele za Mungu pekee ambaye anaweza kukukomboa. Kisha utabakia hapo mpaka jibu lipatikane. Nehemia alitambua hilo kwa ajili ya watu wake waliokuwa wanaangamia katika utumwa, alitakiwa kupata jibu. Hapakuwa na mbadala mwingine.

Sisi, tulioitwa na Yesu Kristo, ni wanyweshaji wa Mfalme Mkuu kwa sababu tunabeba kikombe cha divai ya Roho Mtakatifu wa Mungu ndani ya mamlaka yetu ili kumtumikia Mfalme wetu. Kama Nehemia, tunakaa katika hali ya utumwa wa kiroho katika nchi ya kipagani wakati kanisa limeanguka kwa kuharibiwa kiroho. Kuta za wokovu zimebomolewa na kanisa liko katika kubomoka, na kubakia halina ulinzi dhidi ya adui. Kama Nehemia na Danieli, lazima tukubali chanzo cha hali yetu ya sasa na kulia mbele za Mungu kupata msamaha kwa ajili ya taifa letu na makanisa yetu.

Kama hatulitambui jambo hili la dhambi zetu na kutubu, Mungu anawezaje kubadili hukumu zake? Kama tusipolikubali hili kwa moyo wa upendo uliopondeka, tunawezaje kumtegemea Mungu hata kumsikia toka mbinguni na kutusamehe? Watu wetu

watarudia namna zile zile za kimwili za kidini walizokuwa nazo kabla.

Hili ni jaribio la moyo wa Mkristo. Ni kweli tumekosea kwa dhambi zetu? Tunaomboleza na kulia kwa ajili ya Mungu kuturudia hadi kiwango ambacho tutakuwa tayari kuomba na kufunga mchana na usiku? Tunakubali kuteseka kwa maumivu ya dhambi na kuanguka kwa watu wetu na kumlilia Mungu kwa mioyo yetu yote kwa ajili yake kuwarehemu watu wake? Wakati hukumu ya Mungu ni hakika, pia kuna rehema ikiwa mioyo yetu itajutia makosa, na tunaweza kuigeuza hasira ya Mungu kwa maombi ya toba ambayo yatapenya mbingu na kukifikia kiti chake cha enzi.

Maombi ya moyo ulio nusu nusu hayatafanya kitu. Lazima tupondeke kikamilifu mbele za Mungu kabla hajatuletea urejesho. Hawezi kukijaza chombo ambacho hapo kwanza hakikuwekwa tupu na kusafishwa kupitia toba.

## Changamoto ya Eliya

Kwenye 1 Wafalme 18 tunasoma habari ya changamoto ya Eliya katika Mlima Karmeli. Eliya alishusha moto katikati ya wana wa Israeli waliokuwa wamegeukia kuabudu miungu ya Baali, lakini wakati moto uliposhuka, ulileta uamsho? La hasha. Wana wa Israeli wakasema, "Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu" (msitari wa 39), lakini kukubaliana tu na hali

ilivyo au Mungu alivyo haina maana ya kutubu. Walikuwa tayari kusubiri wakati makuhani wao wanachinjwa katika kitendo cha Eliya kusafisha taifa katika kijito cha Kishoni (mstari wa 40), lakini hawakuwa tayari kuanguka kwa magoti yao kwa moyo uliopondeka katika huzuni ya dhambi yao. Walijali sana kuhusu maisha yao kuliko maisha ya kanisa. Hapakuwa na toba ya ushirikiano ili kutifua udongo mgumu katika taifa.

Eliya hakufanya uamsho wala urejesho kwenye nyumba ya Mungu, na hata mrithi wake Elisha hakufanya. Inahusisha toba ya ushirika ya kuuamsha ushirika, na hiyo haikuja mpaka miaka mingi baadaye. Ingawa nabii alikuwa mtu wa Mungu, udongo mgumu wa moyo wa Israeli ulikuwa haujavunjwa vunjwa ili kupokea mbegu ya Neno la Mungu, na hivyo hakuna mavuno ambayo yaliweza kuzaliwa kwenye huo udongo mgumu, mkavu. Toba kutoka kwenye moyo uliovunjika ndio kitu pekee ambacho kinaweza kuvunja vunja udongo mgumu, ukimwagiliwa kwa machozi yetu, ili kwamba mbegu ya Neno la Mungu iweze kupata udongo utakaoleta mavuno ya uamsho.

Kwa nini tumekuwa vipofu namna hii kwenye ukweli wa kiroho? Kwa nini ni vigumu sana kuvunjika mioyo yetu ili kufikia kwenye hiyo toba ambayo Mungu anaitaka? Nia iliyojumlishwa na taabu na dhiki itatufanya tu tuombe msamaha. Mchanganyiko wowote katika hivyo vitatu lazima utakuwa ni njaa ya haki,

ambayo ni maombi kwa ajili ya kitu kingine tofauti na kile dunia hii inaweza kutoa katika raha na mafanikio. Kwa uaminifu naamini kwamba watu waliokuwa juu ya Mlima Karmeli walikuwa na nia kubwa ya kurudi kwenye maisha ya mafanikio kuliko kwenye maisha matakatifu. Mioyo yao ilikuwa bado haijapondeka kwa ajili ya dhambi yao; walichofanya ni kugundua kosa lao tu.

Kuna ulimwengu wa aina mbili unaotuzunguka: ulimwengu wa mwili tunaouona na ulimwengu wa roho ambao ni wa milele. Kadiri tukaavyo ndani ya ulimwengu mmojawapo, ndivyo tunavyokaa nje ya ulimwengu mwingine. Mpaka njaa ya kuwa watakatifu itakapochipuka ndani ya mioyo yetu, ndipo starehe za ulimwengu huu hazitaendelea kutupofusha ili tuone zaidi ya maisha yetu ya kila siku. Mfalme Sulemani aliandika: "Pasipo maono, watu huacha kujizuia" (Mithali 29:18). Tunatakiwa kuwa na uwezo wa kuona mbali ya Mlima Karmeli na kuona Nchi Mpya ambayo iko mbali sana kwenye umilele na kuitamani sana kama nyumbani mwetu pekee. Ni pale tu tunapoacha ubatili wa hii dunia ili kushikilia mambo yatarajiwayo, ndipo tunaweza kuacha mambo ya ulimwengu wa mwili na kutafuta mahali pa kweli pa toba.

Kutamani haki hutuweka tuhitaji toba, siyo tu kwa ajili yetu bali taifa na makanisa yetu pia. Jambo hili linapotokea, tutakuwa tayari kuuvunja udongo mgumu wa mioyo yetu ili kupanda mbegu za uamsho.

Inachukua muda na moyo ambao hautulii kwenye mambo madogo madogo, bila kujali itachukua muda gani. Hakuna mbadala, bila kujali kanisa lako ni zuri kiasi gani. Ni uamsho pekee tu ndio utakaokidhi maombi ambayo Mungu ameyaweka ndani ya mioyo ya watumishi wake.

Hii ni kwa sababu Nehemia aliomba kwa bidii ili kuona kanisa linarejeshwa. Alipaswa kuona uhalisia wa hali ilivyokuwa. Ndio maana Eliya alikaa kwenye msitari, Danieli alisugua magoti yake, na wale walioguswa na kilio cha Raheli cha "nipe wana, kama sivyo nitakufa mimi," walipambana kwenye kufunga na kuomba mpaka Mungu akajibu.

Mpaka hiyo rehema ipatikane, vinginevyo hakuna uamsho.

## Kushindwa kwa Kanisa Kuokoa Nafsi

Kabla hatujaanguka kwenye magoti yetu katika toba, yatupasa kufahamu nini tunatubia. Toba ambayo nabii Yoeli aliiitisha ni ile ambayo inahitaji kurarua "mioyo yenu, wala si mavazi" (Yoeli 2:13). Toba ya kweli inatakiwa kutoka ndani ya moyo uliororaruliwa au vinginevyo itakuwa ni unafiki. Lakini ili kufikia kwenye moyo mkunjufu wa toba ambayo inahitajika, yatupasa kufahamu kitu gani ndio makosa. Ni kile ambacho hatujawa na "kanisa" zuri la kuridhisha? Au hatujaimba kwa sauti ya juu sana? Au hatujawa wazuri vya

kutosha? Nini ni moyo wa tatizo? Nini tunapaswa kutubu?

Dhambi yetu kubwa, ambayo imesababisha kifo cha kiroho ambacho Yoeli alikitabiri kwamba kitakuja juu ya kanisa katika siku hizi za mwisho, ni kushindwa kupeleka Injili kwa waliopotea. Tumeacha mavuno ya nafsi kupotea (Yoeli 1:11).

Kuokoa nafsi siyo kazi nyingine ya kanisa, wala si jambo tunalofanya tunapokuwa na muda wa ziada au jambo fulani ambalo limekabidhiwa kwenye uongozi wa kanisa kulifanya. Hili siyo jambo lenye kiwango sawa kama kumiliki duka la chakula cha makopo, kukusanya zawadi za kutoa kwa maskini wakati wa Krismasi, au kuandaa stoo ya damu. Kuokoa nafsi ni jambo muhimu la wito wa Kristo; ni mapigo ya moyo hasa wa Mungu. Ndilo uliloitiwa kufanya ulipookoka. Ni moja ya kazi kuu mbili za kanisa. Yesu alisema kwamba tukazae matunda mengi, na matunda yetu yapate kukaa (Yohana 15:16). Lakini kabla matunda yako hayajakaa ndani ya Yesu, lazima kwanza uende nje na kuwaokoa waliopotea kwa ajili ya Bwana.

Ninaona kwenye makanisa mengi kwamba watu wana tabia ya kuamini kwamba kama watalisaidia kanisa lao, itamaanisha kwamba watu wapya watakuja kuokolewa. Waumini wamewaachia wachungaji mzigo na hofu ya kuokoa nafsi. Zaidi ya yote, si ni kwa ajili ya kazi ya kuokoa nafsi ndio maana wachungaji wanalipwa? Jibu langu ni kwamba wachungaji hawazai

kondoo; kondoo ndio huzaa kondoo. Mungu ameweka jukumu la kushuhudia kwa waliopotea chini ya miguu yetu sote. Na ameweka wazi kwamba kuokoa nafsi si jambo ambalo tutalifanya tu katika wakati utufaao. Nafasi yetu ndani ya Mungu hasa iko kwenye jambo hilo. Hili siyo kitu cha kufanya; ni jambo la kufanya.

Ikiwa sababu kuu ya Mungu kuleta uamsho ni kuokoa nafsi, basi kwa hilo tunatakiwa kurudisha usikivu wetu kwake. Wachache wetu ndio wanaotambua jinsi ilivyo muhimu kwa Mungu kuokoa nafsi. Huu ni moyo wa tatizo. Yatupasa kuacha kuweka shabaha juu yetu wenyewe bali tuielekeze kwa wengine.

Mungu anatuhesabu kuwa sisi tu mashahidi wake duniani, na amesema, "Nimetangaza habari, nimeokoa, nimeonyesha, na hapakuwa mungu wa kigeni kati yenu; kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, nami ni Mungu" (Isaya 43:12). Jambo hili ndilo linalovunjwa katika kanisa. Ili kuliweka sawa, lazima tuanze na toba yetu ya ndani mbele ya kiti cha Mungu.

# Sura ya 6

# Hatua ya 3: Jinsi ya Kuuwasha Moto Katika Kanisa

Ni rahisi kububujika sauti ya maneno ya ushawishi yenye kutangaza malengo yanayovutia, lakini bila uelewa wa kutosha kuhusu jinsi gani tutafikia hayo malengo, tutaachwa tukitangatanga bila uelekeo. Kabla ya kwenda mbali, tukiwa kama tuliochokozwa, yatupasa kutulia kwanza kwenye hali duni tuliyonayo. Tutahitaji tuuwashe moto katika kanisa ili kutufanya sote tuwake.

Kabla hatujauwasha moto ulimwenguni, panatakiwa kuwepo na moto katika kanisa letu kwanza. Kama kanisani hakuna moto, wasiookoka wanapokuja hugeuka na kuirudia dunia. Kwa nini wabaki? Una nini cha kuwapa tofauti na falsafa yako kuhusu Mungu? Tunatakiwa kuwa na kitu cha kuwapa wanachokitaka.

Moto unapowaka katika kanisa, hutupatia motisha ya kuwashirikisha wengine hamasa tuliyonayo. Bila huo moto, tutafanya tu kile tunachodhani tunatakiwa kufanya. Tunahitaji moto unaochoma sana ndio utakaotuchochea. Hivi ndivyo uamsho hufanyika. Uamsho hutupatia moto ili tuliletee kanisa huo moto na kanisa liupeleke ulimwenguni.

Tunahitaji kujenga hamasa ambayo itatusukuma kuwa na shauku na kuendelea kukua na kueneza Injili

katika jamii yetu. Wapi tutapata msukumo, nia, shauku, na hamasa ya kwenda zaidi ya miili yetu ili kutimiza mambo haya? Tutauwashaje moto katika kanisa ambalo litaenea katika jamii yetu yote na kujenga hamasa inayoleta uamsho?

Yesu alisema sisi ni chumvi ya ulimwengu (Mathayo 5:13); yaani sisi ni ladha ya chakula cha uzima tukipelekacho ulimwenguni. Chumvi yetu inatakiwa kukifanya chakula hicho kiwe na ladha nzuri kwa wasiookoka ili wakihitaji zaidi tena na tena. Lakini kama chumvi iliyomo ndani yetu itapoteza ladha yake, haitafaa kitu tena. Kama tutawaleta wasiookoka katika kanisa lisilo na moto unaowaka ndani yake, na kama chumvi iliyomo humo haina ladha, watageuka na kurudi nje. Kama huna zaidi cha kuwapa kuliko ambavyo wangepata kutoka kwa ulimwengu, basi kwa nini wajisalimishe maisha yao kwenye dini yako iliyokufa?

Injili ya Yesu Kristo siyo falsafa iliyokufa kuhusu Mungu wala wazo la ushawishi lenye mtazamo mpya wa maisha na umilele. Ni uweza wa Mungu uuletao wokovu (Warumi 1:16). Kama huna kitu cha kutoa zaidi ya dini iliyokufa yenye injili isiyo na uweza, basi utakuwa huna kitu cha kuzipatia nafsi zisizookoka ambazo zina njaa ya kuifahamu kweli. Tunahitaji uweza [nguvu] kwenye ujumbe wetu na moto katika makanisa yetu. Maarifa yote ya elimu ya Mungu ya ulimwengu huu hayatafanya kitu chochote kizuri bila ujumbe

wenye nguvu na moto. Hata hivyo, pakiwa na moto unaowaka kanisani, kila kitu chema hutokea chenyewe. Hamasa huongezeka kwa kila muumini wa kundi mpaka wanapojiona wao wenyewe kuwa katika kupiga mbio kuingia kwenye jamii yao ili kuwaambia watu wengine kile kinachoendelea katika kanisa lao. Majirani zao wanaweza kujionea hilo kwa macho yao na kulisikia katika sauti zao, na hamasa huanza kuenea. Kama ilivyo kwa moto uwakao katika pori la nyasi, mara tu baada ya moto kushika, moto hauwezi kuzimwa bali kuambukizana katika nyasi zilizo jirani.

Jambo pekee linaloweza kuanzisha moto ni moto mwingine. Uelewa wa hilo hufanya iwe rahisi kuona kwamba kuuwasha moto katika kanisa tunahitaji kwanza kuwasha moto kwa mtu mmoja mmoja *ndani* ya kanisa. Joto linalotoka kwenye moto wowote huunguza, siyo kidogo. Moto unaotoka katika mimbari utaleta ushawishi. Moto mkubwa unahitaji kuanza kwenye mabenchi, na kuanzia hapo utaenea miongoni mwa kundi, kisha utaifanya sehemu ya kanisa iliyobaki kushika moto. Tunafanyaje jambo hili? Jibu rahisi ninaloweza kutoa ni kwamba kila jambo linalohusiana na kumtumikia Bwana daima huja kutoka juu kwenye mambo yale yale mawili: Neno la Mungu na maombi. Lakini huanza na Neno kwa sababu Neno la Mungu ni chanzo cha nguvu zote. Ni Neno la Mungu ndilo lililoumba ulimwengu, na ni Neno la Mungu ndilo

litakaloumba uamsho ili kwamba, mwishoni, awe ni Mungu mwenye kupewa utukufu, siyo mwanadamu.

Ili kuuwasha moto, unahitaji vyote kwa pamoja mafuta na cheche/kiberiti. Neno la Mungu ni kuni, na maombi ni cheche. Kimojawapo peke yake hakiwezi kuwaka, bali ukiviweka vyote pamoja, ndipo utawasha moto. Lakini, kila kitu huanza na Neno la Mungu.

Neno hutupatia mambo mengi. Hutupatia ufahamu na maarifa. Hutupatia hekima katika kumcha Bwana na kupambanua mambo ya rohoni (Mithali 1). Hutuosha uchafu na kutupatia nguvu ya kushinda dhambi (Zaburi 119:0). Hutupatia nuru ya kuona (Zaburi 119:105) na masikio ya kusikilizia, lakini cha muhimu sana, hutupatia nguvu ya kuomba.

Unapokwenda kuomba, unapaswa kuamini kwamba Mungu atakusikia; vinginevyo, maombi hayatafanya kitu kwako, kwa sababu bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu (Webrania 11:6). Na utapata wapi imani? Imani huja kwa kusikia Neno la Kristo (Warumi 10:17). Hivyo, ni Neno la Mungu ambalo hutupatia imani ya kuweza kuomba.

Unapokuwa na imani uliyoipata, kupitia kusoma Neno la Mungu, kwenye kiti cha enzi cha Mungu katika maombi, Roho wa Mungu atashuka utakapoomba. Ukimchukua huyo Roho uliyempokea kwenye maombi tena ndani ya Neno, utakwenda ndani zaidi, kwa sababu Roho na Neno hupatana kwa habari moja (1 Yohana 5:7). Unapozama zaidi, masikio yako

yatafunguka hata zaidi, na utaongeza imani yako. Ukiichukua tena ndani ya maombi hiyo imani iliyoongezeka utakwenda juu zaidi. Unapokwenda juu, utapokea Roho zaidi. Ukikichukua tena hicho kiwango kipya cha Roho ndani ya Neno, utazama ndani zaidi. Na kisha utapandisha kiwango hadi juu, na kisha utazama ndani sana, na kupanda juu tena, na kuzama kwa kina kirefu tena, na kuwasha na kuwasha hatimaye moto utaanza kuwaka ndani ya moyo wako na kukuweka kwenye hali ya kukuchoma moyoni! Hivi ndivyo inavyofanyika! Hakuna njia nyingine.

Mara baada ya wewe kuwaka moto, wafanye na wengine kuwaka moto, nao watawafanya na wengine zaidi kuwaka moto, na moto utaenea kama moto unaowaka porini katika kanisa lenu. Mara baada ya kanisa lenu kuwaka moto, litaueneza moto huo kwa jamii nzima. Na mara baada ya jamii kuwaka moto, jamii itaendelea kuwaka mpaka uamsho utakaposhuka kutoka mbinguni. Na hatimaye hapatakuwa na kitu cha kuuzima.

Lakini kila kitu huanza na kusoma Neno la Mungu.

## Harusi ya Kana

Kwenye habari ya harusi ya Kana (Yohana 2), Mungu ametuachia maagizo maalumu kuhusu jinsi ya kumfanya Roho Mtakatifu atembee katika kanisa. Yesu na wanafunzi wake walialikwa kwenye sherehe ya harusi ambapo mwenyeji aliishiwa na divai. Harusi ni

mfano wa kanisa, na divai ni alama ya Roho, hivyo sherehe ya harusi bila divai ni kama kanisa bila Roho wa Mungu ndani yake.

Mariamu, akimfahamu vema mwanae, aliwaambia wahudumu kwa sauti maalumu, ya kimamlaka, "Lolote atakalowaambia, <u>fanyeni</u>!" (msitari wa 5, msisitizo wangu). Unataka uamsho? Basi lolote Yesu akwambialo kufanya, lifanye.

Yesu aliwaambia wafanye nini? Alisema, "Jazeni mabalasi maji" (msitari wa 7).

Maji ni alama ya Neno la Mungu. Tunaliona hili kwenye aya inayozungumzia kusafishwa kwa kanisa kwa maji katika Neno (Waefeso 5:26). Tunaliona kwenye mwamba uliotoa maji (Kumbukumbu 8:15). Yesu ambaye ni Neno la Mungu ni Mwamba ambao Musa aliupiga kama Yesu alivyopigiliwa juu ya Msalaba akatoa damu na maji.

Pia tunaona Neno kwenye birika la shaba ndani ya hema ya kukutania (Kutoka 30:18). Makuhani walioga kwenye birika la shaba kabla hawajaenda kwenye huduma ya Bwana. Kama hawakuoga, wangekufa. Shaba kwenye hilo birika ilikuwa ni ya vioo vya wanawake wenye kutumika (kioo cha kujitazama), waliokuwa wakitumika mlangoni mwa hema ya kukutania (Kutoka 38:8). Kwa nini ilikuwa hivyo? Kwa sababu walipolitazama birika la shaba wangeona taswira ya hali mbaya ya mioyo yao na kisha kuiosha

kwa maji ya Neno la Mungu kabla hawajaenda kwenye utumishi wa Bwana.

Pia, cha kuzingatia ni kwamba kwenye harusi kulikuwa na mabalasi sita ya mawe au udongo (Yohana 2:6). Sita ni tarakimu ya kibiblia inayohusiana na mwanadamu (Ufunuo 13:18 ni mfano mmojawapo). Pia, kama vile Mungu alivyo Mfinyanzi na sisi tu udongo, ndivyo haya mabalasi sita yanavyowawakilisha watu katika kanisa.

Kwenye habari hii, Yesu aliwaambia wahudumu kujaza maji mabalasi. Waliyajaza, siyo nusu wala kukaribia kujaa, bali waliyajaza hata juu mdomoni (msitari wa 7)! Mara tu maji hayo yalipochotwa na kumiminwa kwa mkuu wa meza ya harusi, maji yalikuwa yamebadilika kuwa divai.

Hivyo, Yesu alikuwa akimaanisha tufanye nini? Tuwajaze watu kanisani kwa Neno la Mungu, siyo nusu wala karibu na kujaa, bali hata kufurika! Mabalasi yalipojazwa hata juu mdomoni, Roho na Neno walipatana (1 Yohana 5:7-8), na maji ya Neno la Mungu yatabadilika kuwa divai ya Roho Mtakatifu!

Je kuna maagizo mengine zaidi hapa yaliyo maalumu? Hatujui ya kwamba nguvu zote zinatoka kwenye Neno la Mungu na si mahali penginepo? Hiyo nguvu ya Neno inapoelekezwa kupitia maombi, itauwasha moto. Nguvu hiyo haitokani na vitabu, semina, video, kuimba au kucheza bali Neno na maombi. Kamwe haitokani na kuwa na wazo zuri wala

jambo lolote la kiushawishi la kibinadamu wala kitu mbadala wa hayo. Moto unatokana tu na Neno la Mungu ambao uliuangazia ulimwengu, uliumba ulimwengu, ulifanya uhai kuwepo, na kisha Neno akafanyika mwili na kwenda msalabani kumwaga damu yake kwa ajili ya ukombozi na utakaso wetu. Huwezi kuwasha moto kwa namna nyingine, kwa sababu hakuna nguvu nyingine inayoweza kuleta uamsho katika kanisa lenu. Yesu alisema kwamba bila yeye, sisi hatuwezi kufanya neno lolote (Yohana 15:5), na yeye *ndiye* Neno la Mungu.

Unataka moto uwake kanisani kwenu? Soma Neno la Mungu. Soma na kusoma na kusoma mpaka ujazwe hata juu kwa nguvu za Neno la Mungu, na kisha nenda kamimine divai kwa Mkuu wa Meza ya sherehe kwa kuomba.

Hakuna kujitetea hapa. Hakuna mbadala hapa. Hakuna njia nyingine.

## Eliya Juu ya Mlima Karmeli

Eliya aliitwa na Mungu kama nabii wakati wa majira ya utele. Mashamba yalikuwa ya kijani na mito iliyotiririsha maji ilimzunguka, alisimama mbele ya Ahabu, Mfalme wa Israeli, na kutangaza kukoma kwa mvua. Kila mmoja alimcheka, lakini baada ya miaka mitatu baadaye, hakuna aliyekuwa akicheka. Kiwango cha ukame kiliashiria dhiki ya kiroho kwa taifa, lakini kila mmoja alifikiri ilikuwa ni tatizo la nabii mwenyewe,

siyo la kwao. Ni vigumu kiasi gani kwetu sisi kukubaliana na hali yetu ya kurudi nyuma (kukengeuka)! Na ni jinsi gani ilivyo rahisi kuwalaumu wale ambao Bwana amewainua kuleta ujumbe wa toba!

Baada ya miaka mitatu na nusu ya ukame na dhiki, Eliya aliitisha amri ya kutwa nzima juu ya Mlima Karmeli kwa ajili ya kufanya maonyesho ya mwisho akiwa pamoja na viongozi wa dini: "Kwa hiyo na wakatutolee ng'ombe wawili; wao na wajichagulie ng'ombe mmoja, wamkate-kate na kumweka juu ya kuni, wasitie moto chini; nami nitamtengeneza huyo ng'ombe wa pili; na kumweka juu ya kuni, wala sitatia moto chini. Nanyi ombeni kwa jina la mungu wenu, nami nitaomba kwa jina la Bwana; Mungu yule ajibuye kwa moto, na awe ndiye Mungu."

Eliya alikuwa peke yake. Manabii wengine wote wa Mungu walikuwa wameuawa, isipokuwa mabaki waliokuwa wamejificha. Wakuu wa dini walikuwa 850, miongoni mwao manabii na makuhani wa Baali (manabii wa Ashera), dhidi ya nabii wa kweli wa Mungu (1 Wafalme 18:19).

Israeli, kwa wakati huo, ilikuwa ni ndogo, nchi ya vijijini, kwa hiyo idadi kubwa hivyo ya makuhani wa Baali ilimaanisha kwamba hao walikuwa ni viongozi wa kanisa la kijiji kutoka kila mji mdogo katika Israeli. Hawa walikuwa ni wanaume ambao walifungisha harusi za ndoa za mabinti na wana wao, kuwabariki watoto, na kuongoza makanisa yao. Waliwatambua kwa

majina. Walikuwa ni viongozi wa jamii mbalimbali. Lakini walipenda sana dini ya uongo ya wakati huo. Hawakuwa na wazo kwamba hawakuwa sawa na Mungu. Kiuhalisia walifikiri Baali angewasikia na kushusha moto ili kumwonyesha huyu nabii mzee wa Yehova, mtabishaji, aliyewahukumu, kwamba wao walikuwa ni watu wa kweli waliokuwa sawa na Mungu.

Wako wapi Maeliya wa wakati huu watiao moyo? Tumekamatwa sana na mifumo ya kidini ambayo inatawala makanisa yetu kwamba yeyote asimamaye kuitangaza mifumo hiyo kama ukengeufu atakataliwa kama mtabishaji wa dini, ahukumuye, na aliyepitiliza kiasi. Kama ilivyokuwa kwa Eliya, ujumbe wa kumcha Mungu mara nyingi huchukuliwa kama kusababisha mgawanyiko katika makanisa ya sasa, wakati ujumbe wa mapatano ya kupendana kusiko haki huchukuliwa kama upole na utauwa. Tumechagua kustarehe, na manabii wa Mungu wanakimbia kwa ajili ya uhai wao.

Eliya alifahamu kwamba muda ulikuwa umefika wa Mungu kuonyesha haki yake.

Makuhani wa Baali walianza kwanza maonyesho yao. Walicheza kuzunguka madhabahu yao, walimwita Baali kushusha moto, lakini hakuna kilichotokea. Kutwa nzima hata alasiri walilia, hata wakajikatakata ili kumfanya Baali asikie kwa sababu ya damu zao, lakini hapakuwa na jibu kutoka kwa Baali. Hakuna kilichotokea.

Baada ya makuhani wa Baali kushindwa, Eliya akawaonyesha; akaijenga upya madhabahu ya Mungu. Madhabahu ya Mungu ilitakiwa kujengwa kwa mawe asili yasiyokatwa/yasiyochongwa kwa mikono ya mwanadamu, kwa sababu madhabahu ya kweli ya Mungu isingeweza kujengwa kwa kufuata dini za wanadamu bali juu ya msingi uliojengwa na Mungu.

Kisha Eliya akaletewa maji mapipa manne yaliyojaa.

Kumbuka sasa, hii ilikuwa ni wakati wa ukame mkubwa. Mvua ilikuwa haijanyesha kwa miaka mitatu na nusu. Mito ilikauka, mazao yalikuwa yamekufa, na wanyama walikuwa wanakufa. Kwa nyongeza, dhabihu hii ilikuwa ikitolewa juu ya kilele cha mlima! Walikwenda wapi kutafuta maji kwa ajili ya Eliya? Vema, walitakiwa kushuka chini ya mlima mpaka baharini kuchota maji na kisha kupandisha mpaka juu ya kilele cha Mlima Karmeli.

Basi Eliya akamimina juu ya dhabihu maji yaliyoletwa na kisha akaagiza mapipa mengine manne yaliyojazwa maji. Tena akaagiza mapipa manne yaliyojaa maji. Mapipa kumi na mawili yaliyojaa maji yalitakiwa kumwagwa juu ya madhabahu! Popote walipopata hayo maji, juhudi za kuyapata lazima zilikuwa ngumu sana.

Mungu alikuwa akisema nini? Maji, kama nilivyotaja, ni alama ya Neno la Mungu. Je ni vigumu kwako kusoma Biblia/Neno la Mungu kila siku?

Haijalishi ni vigumu kiasi gani, ni jambo muhimu sana, kwa sababu moto wa Mungu hautashuka juu ya dhabihu yako mpaka madhabahu izamishwe ndani ya maji.

Hapatakuwa na nguvu, wala ujasiri, wala hekima, wala imani ili kuendelea kumtembeza Mungu bila moto kushuka kutoka juu. Tunapotegemea ratiba na mpangilio wetu katika kumtembeza Mungu tutakuwa kama hao makuhani wa Baali. Nina uhakika walimaanisha vizuri. Nina uhakika walifikiri walikuwa ni watu waliokuwa karibu sana na Mungu. Lakini hawakutoa dhabihu ya kweli wala kwa Mungu wa kweli, kulingana na ukweli wa Neno la Mungu, hiyo iliwafanya kuwa waabuduo sanamu. Ni pale tu tunapoikaribia huduma ya Bwana kulingana na Neno lake ndipo atatuhusu kuendelea ili kwamba Mungu pekee, siyo mwanadamu, ndiye apewe utukufu.

# Sura ya 7

## Wito wa Vita

Katika Agano la Kale, tarumbeta mbili za madini ya fedha zilipigwa ili kuuita mkutano kukusanyika pamoja:

> *Tena hapo mtakapokwenda kupiga vita katika nchi yenu, kupigana na adui awaoneaye ninyi, ndipo mtakapopiga sauti ya kugutusha kwa tarumbeta; nanyi mtakumbukwa mbele za Bwana, Mungu wenu, nanyi mtaokolewa na adui zenu. (Hesabu 10:9)*

> Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Pigeni na kelele katika mlima wangu mtakatifu; Wenyeji wote wa nchi na watetemeke; Kwa maana siku ya Bwana inakuja. Kwa sababu inakaribia; *(Yoeli 2:1)*

Tarumbeta/baragumu zilipigwa kuwaita watu pamoja kwa makusudi mbalimbali; huduma za kidini, amri mpya au matangazo mapya, na mwanzo wa sikukuu au sherehe. Hata hivyo, zilipopigwa kutoa sauti ya tahadhali, ilikuwa ni kuwakusanya watu wa Mungu kwenda vitani. Mungu anapotuita sisi katika kitabu cha Yoeli kwa sauti ya tahadhali katika mlima wake mtakatifu, anatuita kwenye vita. Silaha ambazo

Mungu huzitoa kwa Wakristo zina uweza katika Mungu hata kuangusha ngome na kila kitu kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu. Paulo anaelezea Neno la Mungu kama upanga wetu, haki kama dirii yetu (buletiprufu), wokovu kama chapeo yetu (helmeti), na imani kama ngao yetu (Waefeso 6:10-14). Tumeitwa kama askari ili tuvipige vile vita vizuri vya imani. Mgogoro wa nuru na giza ni maudhui ya Biblia inayotawala tangu kitabu cha Mwanzo mpaka Ufunuo na hii inafafanua wito wetu kama majeshi ya Bwana wa majeshi. Tuko vitani, na hatutaiepuka mpaka tunakufa.

Hatuwezi kuwa askari wa kweli kama hatuna vita vya kupigana. Mioyo yetu haitakuwamo, suluhu yetu haitakamilika, na ujasiri na mwelekeo wetu utashindwa kama hatuko tayari kuhatarisha kila kitu chetu ili kuutafuta ufalme wa Mungu. Huo hauwezi kuja katika kanisa ambalo halijapitia hatua ya kutambua, kisha kuhitaji, kisha toba. Ni pale tu tunapokuwa tumepitia kwa dhiki hatua hizo ndipo tutakapokuwa tayari kupigana vita hata kufa kwa ajili ya kweli ya Mungu.

Wito kutoka kwa Mungu unaendelea:

> *Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni watoto, Na hao wanyonyao maziwa; Bwana arusi na atoke chumbani mwake, Na bibi arusi katika hema yake. Hao makuhani, wahudumu wa Bwana,*

*na walie Kati ya patakatifu na madhabahu, Na waseme, Uwaachilie watu wako, Ee Bwana, Wala usiutoe urithi wako upate aibu, Hata mataifa watawale juu yao; Kwani waseme kati ya watu, Yuko wapi Mungu wao? (Yoeli 2:15-17)*

Huu ni wito wa maombi makali ya kumaanisha. Haya siyo maombi ya kupona mguu wenye kidonda, kupata kazi mpya, wala kupata fedha zaidi. Huu ni wito wa kupiga radi hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu kwa ajili ya uamsho katika nchi yetu yote. Yanayopita ni fikira za kawaida za hii dunia na kuridhika na "kanisani kama kawaida." Huu ni wito wa vita.

Majeshi ambayo Yoeli anayaelezea katika sura ya 2 ni wakatili, fidhuli, wako haraka, wasiojadiliana, na hawana kingine kama tunachokiona kwenye mabenchi yetu leo. Hawajali kitu katika kile dunia inatoa, na hawaangalii nani anatuhumiwa makosa kupitia ujumbe wao mkali wa toba. Moto wao unawaka kutokea kwenye madhabahu ya Mungu na hawatatoka mpaka Bwana amerudi. Hakuna kitakachosimama kwenye njia yao. Bwana amewaagiza na ananena sauti yake mbele zao. Wataomba katika kurudi kwa Bwana kwa nguvu na uweza wake.

Aina hii ya uwezo inaweza kuwa na maana kama tusikiavyo kutoka mimbarini au kwenye televisheni leo? Hii siyo Injili ya upole na unyenyekevu [mbele za wanadamu waliomkataa Mungu], ambayo wachungaji

wetu walitulisha sisi. Huu ni wivu unaotula na shauku inayowachapa mijeledi wauza fedha hekaluni. Haitakaa kirahisi katika makanisa yetu yaliyobweteka, kwa maana haitapata udongo mzuri mahali hapo. Ni moto uliowekwa tayari kuteketeza makapi na kuusafisha uwanda.

Aina hii ya vita vya moto huzaliwa na aina ile ile ya maombi. Nyakati rahisi za kutafakari hazitakuwa na joto kubwa sana lenye kuwasha huu moto. Kuwa na mazungumzo mafupi na Yesu hayatavunja mlango wa kuingia chumba cha enzi ya Mungu ili kuunda jeshi kama hili. Hii inachukua maombi makali ya mpambano ya askari ambao watahuzunika kwa machozi na kulia ili kuitikisa misingi ya mbinguni kwa ajili ya kumfanya Mungu atutembelee. Hii ni aina ya imani inayotangaza, "Sitatikisika; sitakataliwa; sitakata tamaa. Nitazishikilia imara pembe za madhabahu na kudai ahadi za Mungu mpaka mbingu zitetemeke na nchi itikisike na Mungu atumwagie roho ya uamsho!"

Kabla hatujakwenda kama majeshi kutembeatembea katika mitaa na kupiga gia kamilifu ya vita, lazima tuelewe kwamba hatutashinda vita katika mitaa mpaka tushinde vita hiyo kwenye chumba cha maombi kwanza. Na siyo tu maombi, bali maombi ya mapambano mpaka tumepokea majibu. Uwezo katika Mungu huja kwa ushindi uliopatikana kwa shida katika chumba cha maombi, na bila hayo maombi, yote tutakayodhihirisha kwa watu waliopotea ni haki ya

macho ya kimwili isiyo na Roho wa Mungu. Kama tunataka Mungu atembee, basi tunahitaji kumtembeza. Mwili hauna faida. Watu wengi walio walumbi (watu wenye lugha ya kushawishi) duniani wanaweza kuishawishi akili, bali Roho wa Mungu anaweza kuugusa moyo.

Unaweza kuwa na ndoana bora ya kuvulia samaki na chambo chake bora sana duniani, bali kama samaki hawana njaa, hawatakula chambo. Maombi yanahitajika kumfanya Roho wa Mungu atembee ili kuwatikisa wenye njaa mioyoni mwao kwa ajili ya kuitafuta kweli kabla hatujaenda kuzitafuta nafsi zao zilizo tayari kwa wokovu. Kama tutajaribu kupiga mbio za shauku yetu kabla hatujautetea ushindi katika chumba cha maombi, tutatimiza machache tu.

Hao wanamaombi askari wa zamani walizungumzia kuhusu jinsi "walivyoomba mpaka mwisho" – kwa namna yoyote mpaka mwisho – hadi walipopokea majibu kutoka kwa Mungu. Mahali fulani kwenye njia zetu hizi za sasa za kufanya mambo, tumepoteza huo uwezo wa kupasua anga hadi kuingia kwenye malango ya mbinguni. Tunasema tunayo imani, lakini imani siyo kuamini tu kwamba Mungu anaweza kufanya chochote. Mjinga yeyote pia anaweza kuamini hivyo. Imani ya kweli ni kuamini kwamba Mungu *atatutembelea* na kukataa kukatisha maombi mpaka amefanya hivyo! Chochote pungufu ya hicho siyo imani bali ni imani ya kuangalia mazingira yalivyo.

Lakini tunaiona imani ya kweli leo? Tumekwishazungumzia maombi ya mikutano ya mikesha ambayo yalikuwa yakifanywa usiku mzima hadi mapambazuko kwa ajili ya nafsi kuokolewa.

Huzuni ya kilio cha Raheli ilikuwa machozi. Na hadi tufikie hicho kiwango cha kujitoa kabisa bila majadiliano, la sivyo hatutakuwa na msukumo utakaotupeleka mpaka kuupata ushindi kwa namna yoyote.

Tumeruhusu sisi wenyewe hii hali ya kubweteka inayotufunika tusijali nafsi za wengine, na matokeo yake imeua nafsi ya kanisa. Hatuombi tena kwa kiwango cha askari tulichoitiwa. Mungu anatuita kama askari, na yatupasa kuomba kwa kiwango cha askari ili kuangusha kila upinzani wa kipepo, kubomoa kila vikwazo vya kiroho, na kupigana kiroho kwa ajili ya huu uamsho tunaotamani uanze. Bwana anasema:

> *Lakini hata sasa, asema Bwana, nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya. N'nani ajuaye kwamba hatarudi na kugeuka, na kutuachia baraka nyuma yake, naam, sadaka ya unga, na sadaka ya*

*kinywaji, kwa Bwana, Mungu wenu? (Yoeli 2:12-14)*

Yoeli analiita kanisa kujitakasa kikamilifu na kujitoa kikamilifu kwenye maombi ya kumaanisha yasiyo ya sheria za kidini. Hii pekee inaweza kutoka kwa wale walio na huzuni ya kutaka kumwona Mungu akitutembelea. Hawawezi kuridhishwa na chochote isipokuwa uamsho kwa ajili ya nchi yote. Hii ni moja ya hatua ambayo Mungu aliwaleta kuifikia na kuifanya duniani. Kazi yao katika kuomba haififii fifii kama taa yenye swichi mbovu bali wamepitishwa katika mchakato wote wa moto ambao umeteketeza hali zote za tamaa na kubweteka katika mambo mengine. Hakuna jambo jingine litakalowafaa. Kama ilivyo kwa kilio cha Raheli lazima nasi tuseme, “Bwana nipe hizo nafsi (wana), kama sivyo, nitakufa mimi!”

Ni katika hatua hii kwamba Mungu atasikia kilio chetu na kutujibu. Kwa wana wa Israeli wakiwa Misri, iliwachukua miaka mamia kufikia kwenye hatua hiyo ya huzuni kabla hawajamlilia Mungu. Lakini walipomlilia, Mungu alisikia maombi yao na kumtuma mkombozi. Je itachukua muda gani kwa kanisa la sasa kufikia kwenye hatua hiyo ya kuhuzunika? Mungu atamtuma farao muovu kuwaua watoto wetu ili kutufanya tupige magoti yetu chini kumwomba Mungu?

Lakini kama tutafikia hiyo hatua ya maombi, yeye atatusikia.

# Sura ya 8

## Hatua ya 4: Kuokoa Nafsi, Siri ya Uamsho

Kizazi cha sasa kinaonekana kupenda sana baraka, miujiza, na upako lakini haya yote hupatikana kupitia utakatifu, kumcha Bwana, na mateso ya msalaba. Daima hupatikana kwa njia hiyo, lakini sikumbuki kama nilisikia kuhusu wakati ambao lengo kuu la Wakristo wengi lilikuwa ni kuzama sana katika "baraka za rohoni." Kadiri tamaa ya kuwa mtu wa kiroho inapogeuka kuwa ya muhimu zaidi kuliko kutunza amri za Mungu, ndipo huwa tunajikuta tumeshindwa na jaribu lile lile ambalo Hawa alilifanya alipolikaribia hilo tunda bustanini.

Uamsho hauhusiani na kutafuta miujiza, mafanikio, uzoefu mzuri, wala kuwa na wakati mzuri; uamsho unahusiana na kutafuta kuwaokoa waliopotea. Nukta. Baraka zote za ajabu za Roho—miujiza, uponyaji, kujazwa, na upako—ni matokeo ya uamsho, siyo sababu ya uamsho. Tunapoyafumba macho yetu tusiokoe nafsi na kuanza kujiachilia sisi wenyewe kwenye baraka zisizoambatana na kuokoa nafsi, tutakuwa tunazungusha koki nyuma kuziba mrija wa Roho wa Mungu. Baraka zinapotamkwa na kutekelezwa huwa tunaachwa hatuna chochote bali kanisa, desturi, na rundo la kumbukumbu zinazofifia za jinsi ambavyo ingekuwa kama Roho wa Mungu

angeachwa kutiririka kwenye kanisa letu la sasa lililokufa.

Tunapogeuka na kutambua kile moyo wa Mungu unakitamani sana, na tukaelekeza shabaha yetu kwenye kuokoa nafsi zilizopotea, ndipo hatutaendelea kuisha sisi wenyewe, ndipo lengo kuu la maisha yetu sasa litaambatana na Amri Kuu mbili: mpende Mungu na okoa nafsi za wengine. Halafu, tutaanza kuuona uamsho wa Roho Mtakatifu ambao utazifungua mbingu na kuubadilisha ulimwengu.

Hii ni siri ya uamsho.

Kuokoa nafsi ndio moyo wa Mungu hasa. Ndio nia yake ya ndani kabisa. Nabii Malaki anatwambia kwamba Mungu anatuona kama vyombo vyake (Malaki 3:17). Sisi ni wa thamani mbele ya macho ya Bwana, zaidi ya vile ambavyo tungeelewa kikamilifu. Kama Mfalme wa utukufu, Yesu aliacha mbingu ili apitie majaribu yetu yote, majaribio na mateso ya mwili, ili ateseke kwa kuteswa pekee na kupata aibu ya msalaba. Na kisha, hata kwa kiwango kikubwa zaidi, alitakiwa kuzibeba dhambi zote za ulimwengu na kuachwa na Baba yake kama ambavyo alipaza sauti ya kilio, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona waniacha?" (Marko 15:34). Haya yote yalifanyika ili tuwe pamoja naye milele. Kama ambavyo Daudi alisema, "Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie?" (Zaburi 8:4).

## Mausia ya Mwisho

Kuokoa nafsi ilikuwa ni jambo muhimu sana kwa Yesu kwamba, alipokaribia kupaa juu mbinguni, aliwaachia wanafunzi wake mausia yake ya mwisho. Alikuwa anaondoka na asingerudi kwa muda wa maelfu ya miaka, hivyo alitoa mausia yake ya mwisho. Wakati wowote mtu aliye karibu na sisi anapotuacha kwa mara ya mwisho hutuomba atupatie wosia wa mwisho, daima huwa ni kitu chenye uzito kwetu. Wengi wetu huhakikisha wanafanya kila kitu ili watimize hayo mausia ya mwisho. Yesu alituachia Agizo Kuu: "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15).

Cha kusikitisha, wengi wetu hawajakwenda hata kwa majirani zao, kamwe hawaujali ulimwengu. Lakini wamefanya kila kitu kingine wanachofikiria ambacho Mkristo anapaswa kufanya. Kila kitu, yaani, isipokuwa kile Bwana ametuagiza kufanya. Angalau, sote tumesikia kuhusu hili andiko na tumelipuuza. Namna hizi zifuatazo za kujitetea tetea zinaonekana kufanana:

- *"Labda ilinenwa tu kwa ajili ya wanafunzi waliokuwa wakisimama mahali pale."*
- *"Kuna kazi zingine tunaweza kufanya badala ya ushuhudiaji kwa waliopotea."*
- *"Hiyo ni kazi ya mtu mwingine. Mimi si mtu mzuri katika jambo hilo."*

- *Nina uhakika Bwana ananiona na kuniacha nuru yangu iangaze kwenye pembe."*

Yesu aliupenda ulimwengu upeo hata akayatoa maisha yake kwa ajili ulimwengu. Jambo gani kubwa zaidi ambalo angefanya? Na sasa kazi iko upande wetu. Bwana hasa hasa ametuagiza kwenda – siyo kukaa chini, siyo kusubiri, siyo kufikiri sana, na hakika siyo kujitetea tetea kwa vijisababu.

> *Kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema! (Warumi 10:13-15)*

Kama kuokoa nafsi ni siri ya uamsho, na ikiwa Yesu ametuagiza kushuhudia kwa hizi nafsi na kwamba hazitaokoka isipokuwa tumefanya hivyo, na ikiwa ametuambia atamwondoa Roho wake katika kanisa mpaka tutakapofanya, basi tunangoja nini?

## Karamu Kubwa

Luka anatwambia kwamba Yesu alikuwa akila chakula nyumbani mwa mkuu wa Mafarisayo. Baada ya kuwaonya kwa sababu hawakuwaalika maskini, vilema,

viwete, na vipofu, mmoja wa watu wa kidini aliyekuwa hapo akatoa maoni, “Heri yule atakayekula mkate katika ufalme wa Mungu” (Luka 14:15) Hii inasikika kama maoni maalumu kwa ajili ya yule Farisayo, au hata waumini wa madhehebu mengi ya wakati ule na sasa, wanaojaribu kufaa katika mazungumzo lakini wakibakia na deni la ukweli kwamba wanafanya kinyume kabisa na kile Yesu alikizungumzia. Ni vipofu hata hawaelewi anasema nini.

Yesu alijibu kwa kuwaeleza mfano wa karamu kubwa, ambapo miongoni mwa watu walioalikwa walikuwepo wanaume watatu, lakini wote wakajitetea tetea kwa nini hawatakuja kwenye karamu. Walikuwa na shughuli nyingi. Basi mtumwa akatumwa tena kwenda mitaani kuwaalika maskini, viwete, vilema na vipofu – watu wale wale ambaoYesu alimwagiza Farisayo kuwaalika – na kuwaleta kwenye karamu kubwa. Kukiwa bado kuna nafasi, Bwana akamwamuru mtumwa kwenda tena mitaani na “kuwashurutisha kuingia ndani” (Luka 14:23) ili nyumba ya Bwana apate kujaa. Lakini nini kilitokea kwa watu walioalikwa kwanza lakini wakawa tu na shughuli nyingi? Hata kuionja tu ladha ya chakula hawakuionja.

Yesu anaongelea watu gani kwenye mfano huu? Hakika siyo kwa mtumwa wake anayezunguka zunguka akijaribu kuweka mambo yote sawa. Ujumbe unalihusu kanisa. Je tumekuwa na shughuli nyingi hata tunavutiwa sana na maisha yetu badala ya kushiriki

katika kutimiza Agizo Kuu kwa kwenda ulimwenguni kuwaalika waliopotea kuja kuingia kwenye karamu ya wokovu? Ni nia ya Mungu kuzijaza nafasi katika nyumba yake ya karamu. Na kama hatuendi, atatafuta mtu mwingine kuchukua nafasi yetu.

## Kilio cha Raheli

Tukiwa kama kanisa, Bibi-Harusi wa Kristo, tunatakiwa kuwa na shauku na huzuni ya kuona nafsi zinaokolewa kama tunavyoona kwenye kilio cha Raheli, ambaye alipotambua kwamba hamzalii mumewe watoto alilia, "Nipe wana, kama sivyo, nitakufa mimi!" (Mwanzo 30:1). Yatupasa pia kujisikia aibu hiyo hiyo ya kutozaa kwetu matunda kwa ajili ya mume wetu, Yesu Kristo, na hii itatupatia msukumo wa kupiga magoti yetu kwa huzuni tukilia, "Bwana, nipe hizo nafsi, kama sivyo, nitakufa mimi!"

Katika Agano la Kale, kusudi kuu la mwanamke lilikuwa ni kumzalia mumewe watoto. Hawakuoana ili mke atandike kitanda, afue sokisi zake, wala kuandaa kifungua kinywa; walioana ili kulea familia. Kwa hiyo, ilikuwa ni aibu kwa mwanamke kuwa tasa. Hata sasa wakati wa jamii hii ya kisasa, kuwa na watoto ni moja ya matamanio makubwa ya mwanamke. Wanawake wameumbwa na hiyo tamaa ndani yao.

Kama vile Raheli, tunahitaji kutaka kuwa na watoto wa kiroho hata kufa. Kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya hizo nafsi ili ziweze kuokoka. Hivi ndivyo Yesu

alivyohisi. Alizipenda nafsi upeo hata akayatoa maisha yake kwa ajili yao. Anategemea kuona sisi tunafanya hivyo pia.

Kuokoa nafsi ni zaidi ya nia ya Mungu. Kuna kusudi la tofauti kwenye mpango wake. Pale kanisa linapoacha kuokoa nafsi, tutakuwa kama mwanamke tasa kwa Mungu. Kusudi letu la kumtumikia Mungu ni kuzaa matunda. Kama tuliokoka kwa ajili ya nafsi zetu tu, basi kwa nini tuendelee kuishi? Kwa nini tusiokolewe kisha tufe? Kwa nini tupoteze hii hewa? Basi na twende moja kwa moja mbinguni. Inatosha. Aha, lakini bado tunaishi, si sisi? Yawezekana kuna sababu kwa nini tunaendelea kuishi. Ni kwa sababu tunatakiwa kutimiza hii misheni ya Bibi-Harusi wa Kristo na kuzaa matunda mengi.

## Tumeokolewa ili Tuzae Watoto

Katika kuandika kuhusu Adamu na Hawa, Mtume Paulo anatwambia,

> *Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi.* (1 Timotheo 2:15).

Je anasema kwa habari ya wanawake wote wasiozaa kuwa watakwenda jehanamu? La hasha. Anazungumzia kuhusu kanisa! Kama vile Hawa alivyokuwa bibi-harusi kwa Adamu wa kwanza, ndivyo

na kanisa lilivyo Bibi-Harusi kwa Kristo, Adamu wa pili. Na kwa jinsi hiyo, kanisa limeagizwa kuzaa matunda mengi. Kamwe usikosoe jambo hili kwa kuweka maoni hafifu ambayo Paulo anayatupilia mbali. Hii ni Amri muhimu sana kuhusu umuhimu wa kuokoa nafsi.

## Mzabibu wa Kweli

Yesu ameandikwa katika sehemu nne kwenye Injili akisema kwamba kila mti usiozaa matunda mema lazima utakatwa na kutupwa motoni (Mathayo 3:10, 7:19; Luka 3:9; Yohana 15:2). Kwenye mfano wa mzabibu wa kweli, Yesu anatwambia tena kwamba kama tutakaa ndani yake, tutazaa matunda mengi, lakini tusipokaa ndani yake, tutakatwa na kutupwa motoni (Yohana 15). Ndiyo! Motoni? Je huu ni mgongano? Sidhani. Kanuni iko wazi. Kusudi letu kuu ni kuokoa nafsi. Kama hatufanyi hivyo, basi tumekuwa tawi lililokufa, tusio na uhai bila chemchemi ya Roho Mtakatifu ibubujikayo ndani yetu na hatutafaa kitu bali kukataliwa na kutupwa motoni [jehanamu]. Na kama tukiwa kama matawi yaliyokufa, bila Kristo ndani yetu, tutatupwa motoni, wapi unafikiri utakwenda kuishi milele?

Jambo hili halipambi ili kufanya mwonekano wa kuvutia. Hata hivyo, liko wazi kwa kile Mungu anataka. Yesu alisema alituchagua kwa kusudi moja: twende tukazae matunda na kwamba matunda yetu yakae

(Yohana 15:16). Hii hapa haituhusu sisi. Inamhusu Mungu.

> *Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. (Yohana 15:8).*

Sisi na uumbaji wote tuliumbwa ili kumtukuza Mungu, na hivi ndivyo anavyotukuzwa – pale tunapookoa nafsi! Kuimba nyimbo na kuinua mikono katika sifa ni mambo makubwa, lakini kama nafsi zinashuka kuzimu wakati tunaendelea kuimba nyimbo zetu, basi hii inampaje Mungu utukufu? Kwa hiyo, kusudi la kuokoa nafsi siyo tu kurejesha ubinadamu, bali tufanye hivyo tukimtukuza Mungu, siyo tu kwa rehema na upendo wake wa huruma, bali pia kwa ajili ya haki na hukumu.

Mungu alikuwa na mpango, na ulikuwa ni wa muhimu kwake hata ikamgharimu kila kitu. Hii ilikuwa ni muhimu kwa Mungu hata Yesu "asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu; ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye" (2 Wakorintho 5:21). Aliufungua moyo wake na kuruhusu kupondeka, kupigwa na kuuawa ili tuokolewe kutoka mautini na kuishi katika uzima wa milele pamoja naye, ili kwamba mwisho wa yote utukufu wote umwendee Mungu.

Ni gharama ya namna gani tuilipe; bali pia ni utukufu wa namna gani tutaurithi!

Lakini Yesu alikwenda hatua moja ndani zaidi: "Nanyi mtakuwa wanafunzi wangu kwelikweli."

Na ni nini hutokea tusipozaa matunda mengi? Tutaendelea kuwa wanafunzi wake? Aha, umeona hoja yangu? Ni kutembea kwetu na Mungu, hata kusudi letu kuu la kuishi limefungashwa kwenye kuokoa nafsi.

## Kuitikia Kwenye Wito

Kuokoa nafsi kwa ajili ya Kristo siyo tu ni kazi nyingine ya kanisa; ni amri kwa kanisa. Mungu alimwambua Adamu, Nuhu, Ibrahimu, na Yakobo kuzaa na kuongezeka [na kuijaza nchi]. Amri hiyo ni kwa ajili yetu pia.

Nimewasikia wachungaji kadhaa wakisema kwamba kanisa lao halifanyi uinjilisti kwa sababu wanaamini wana wito mkubwa wa kulihudumia kundi lao kuliko kwenda nje ulimwenguni kuwaalika waliopotea. Wachungaji wengine hawana ujasiri wa kusema kitu kama hicho cha kijinga, bali ukosefu wao wa jitihada za kuwafikia watu wasiookoka na ukosefu wa huduma za kuwafikia waliopotea hudhihirisha kuwa wao pia wana tatizo hilo hilo. Wengine wana huduma za nje ambazo huwapeleka kwenye maeneo rahisi tu ambayo hayana upinzani wala hakunako dhambi na hatia nyingi ili kujiepusha na matatizo. Hawajali kabisa, hujenga jengo mahali fulani, hupaka rangi kanisa, au hufanya maonyesho ya zawadi. Hawajali kuhusu kutembelea katika jamii ili kuipa

changamoto na kuwaalika wenye dhambi kuuijia wokovu? Hapana, kwa kweli wanaamini hawapaswi kwenda ulimwenguni kuokoa nafsi; wanachoamini ni kwamba, wanaweza kuziokoa kupitia njia zingine zisizo za moja kwa moja.

Kwa nini tunaogopa hivi kuwaambia watu ukweli wa Injili? Kwa nini tumesinyaa kuwaambia kuhusu hukumu ijayo na kutumaini kwamba ikiwa tutawaambia kuhusu upendo watatubu? Hii ni kwa sababu tunaiogopa hukumu yetu sisi wenyewe [ya kutookoa nafsi]? Je kukosa kwetu haki na hali ya kumwogopa Mungu kunatushawishi na kutuweka mbali na hali ya kusimama imara ili kuihubiri kweli?

Mungu ameweka kigezo, kwetu sisi kama walinzi, cha kuwaonya watenda dhambi kuhusu hukumu inayokuja kama hawatatubu. Hii imewekwa wazi kwenye aya kuhusu walinzi walioko juu ya ukuta (Isaya 62:6). Matokeo kwetu yatakuwa mabaya kama hatutatekeleza:

> *Nimwambiapo mtu mbaya, Hakika utakufa; wewe usimpe maonyo, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya, kusudi aache njia yake mbaya na kujiokoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. (Ezekieli 3:18)*

Ni maneno yanayokereketa. Na bado, hili si tendo la kwenda nje kuwaokoa wenye dhambi wasiende jehanamu ya milele, yaani kuonyesha upendo wa Mungu kupitia sisi? Wewe je! Usingependa mtu akuonye kama ulikuwa unaelekea jehanamu? Yesu alisema,

> *Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii. (Mathayo 7:12).*

Sheria yote na manabii wamejumlishwa katika hii kauli! Neno lote la Mungu linalenga kuokoa nafsi, na amri za Mungu kwetu ni sisi kuwa vyombo anavyovitumia kuzionyesha nafsi rehema yake.

## Amri Kuu

Sheria yote na manabii wote wamefungwa kwenye Amri Kuu mbili:

> *Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika*

*amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. (Mathayo 22:36-40).*

Kila jambo linaloamua hatima yetu ya milele na mahusiano yetu yasiyokwisha ya kuishi pamoja na Mungu Mwenyezi linaweza kuchujwa kwenye hizi amri mbili: Mpende Mungu kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote; na mpende jirani yako kama nafsi yako. Kama usipotimiza hizi amri mbili, haitajalisha ni kiasi gani amri zingine unazitimiza.

Tunapobadilisha mtazamo wetu kutoka kujithamini sisi wenyewe tu kwenda kujishughulisha na wengine ni mzani uliotulia sawa sawa katika maisha yetu ya Kikristo. Hii ni kanuni ya 2 ya uamsho: injili haituhusu sisi tuliookoka; inawahusu wengine. Mara ngapi tumeonywa katika Agano Jipya kuwapenda ndugu zetu? Unaweza kuona kwamba mtazamo wetu juu ya Mungu unaaksi ndani yetu kwenye kuwatazama wengine?

Naamini kinyume chake ni kweli pia. Kama kweli tunampenda Mungu kwa moyo wetu wote, ndipo tutakwenda kwa waliopotea, kwa sababu tunatambua kwamba kusaidia katika kumwokoa aliyepotea atoke kwenye ufalme wa giza ina thamani kubwa kwa Mungu hata alimtoa mwanae ili waokolewe. Mungu anatuagiza sisi kufanya jambo hilo pia. Hili siyo ombi bali ni amri inayotoka moja kwa moja kwenye kinywa cha Mungu:

Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili… mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…

## Kanisa la Efeso

Leo kanisa linashiriki kwenye miradi yote, kutoa misaada, programu za huduma, zitaje, lakini limesinyaa kwenye kupiga vita kwa sababu limepoteza kumcha Mungu, shauku yake ya Mungu alicholiitia, na mguso wake wa kuishinda dhambi na mauti.

Uko na shughuli nyingi na "mambo ya kanisa" yanayokufanya usiwe mwokoa nafsi wa kweli? Unafikiri kuwa na shughuli nyingi kwenye ratiba zote na matukio yote ya kanisa lako ni mbadala mzuri wa kuwa shahidi? Hii ni imani ya wengi katika ulimwengu wa kanisa. Tuko bize, bize, bize na shughuli za kanisa kwa sababu ni rahisi kufuata ratiba iliyokwishaandaliwa kuliko amri ya Yesu ya kwenda mitaani. Lakini kubadilishana kazi za kimwili na amri ya kwanza ya Mungu kwamwe haitamridhisha Mungu. Ni kosa hilo hilo ambalo Kaini alilifanya alipomletea Mungu dhabihu za mbogamboga badala ya damu ya mnyama juu ya madhabahu ya Mungu.

Nina hakika Kaini alifanya kazi kwa bidii. Lazima alikuwa na uchungu mkubwa kuliko Habili ambaye hakufanya mengi zaidi tu ya kutembeatembea akitazama kondoo kutwa nzima alipofanya kazi yake nyingine ya kuzalisha mbogamboga kadhaa. Lakini siyo hicho Mungu alikitaka. Malipo ya dhambi ni damu, na

matendo yote mema (au mbogamboga) hayawezi kutimiza vigezo vya ukombozi hapa duniani. Na hayataweza kusababisha juhudi, miradi, na programu kubwa, vitabu, filamu, na juhudi zingine za kimwili ambazo zitachukua nafasi sawa ya mambo rahisi Mungu anayataka: kusoma Biblia, kuomba, na kushuhudia.

Kanisa la Efeso pia lilifikiri litaweka matendo mema kuwa sawa na kwenda kuokoa nafsi. Katika Ufunuo 2, Yesu anawarudi Waefeso kwa kuwaambia kwamba anayajua matendo yao, na taabu yao, na subira yao, na ya kuwa hawawezi kuchukuliana na watu wabaya. Oho, walikuwa ni matajiri katika kila "jambo la kanisa," lakini walipoteza upendo wao wa kwanza.

Upendo huo wa kwanza ni ule ambao wewe mwenyewe ulijisikia pale ulipookolewa kwa mara ya kwanza. Unakumbuka ulivyojisikia pale huo mzigo wa dhambi ulipoondolewa kwako, pale ulipojisikia kuwa huru kwa mara ya kwanza maishani mwako, na pale ulipojisikia umevuka kutoka mautini [hukumuni] kuingia uzimani? Ulihamasika sana hata ukataka kumwambia kila mtu kile Yesu Kristo amekutendea.

Lakini waamini wengi wamepoteza hiyo hali yenye hamasa mbichi na wamekalia tu kukaa "kanisani kama kawaida." Msisimko na hamasa waliyojisikia mwanzoni kama watoto wachanga katika Kristo imeshakwisha siku nyingi na hawawaki tena huo moto mtakatifu. Tumepoteza upendo wetu wa kwanza.

Hivyo Mungu anasema nini kwao waliopoteza upendo wao wa kwanza? Tubu, ukayafanye matendo ya kwanza, usipofanya hivyo Bwana anakuja haraka—hakuna utani hapa—na atakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu. Bila kinara cha taa, tutakuwa hatuko nuruni bali gizani, tutatangatanga kwa kupotea.

Kushiriki kwenye mambo ya kanisa kama vile kuhudhuria ibada, kuimba, kutoa misaada ya chakula kwa maskini na zawadi kwa watoto wakati wa msimu wa Krismasi, ni mambo makubwa kuyafanya, lakini hayataondoa hukumu ya Mungu.

## Huruma au Upendo

Kwenye Wakorintho wa kwanza sura ya 13, Paulo anafafanua umuhimu mkubwa kuhusu upendo dhidi ya matendo ya kimwili. Unaweza kufanya mambo yote ya kidini—kunena kwa lugha, kufanya unabii, kupambanua roho, na kuwa na imani ya kuhamisha milima—lakini kama huna upendo, wewe si kitu. Kuna haja gani ya kuwa mtu mwema aliye mkuu sana duniani kwa ajili ya Mungu lakini ukawa hujali kuhusu waliopotea? Makusudi yote ya wewe kuitwa yamefungashwa ndani ya wito wa kuzaa matunda mengi. Mungu hana haja na wajionao kuwa wema sana; ana haja na watumikao.

Na vipi kuhusu matendo mema tuyafanyayo? Kama utawapa maskini vitu vyako vyote ulivyonavyo — vitu *vyote* — itakufaa nini kama hutawaambia Injili ili

wakaishi mbinguni katika uzima wa milele? Kama utautoa mwili wako kuchomwa moto ili kwamba ujitoe kafara iliyo bora, hii itasaidia nini katika kumwokoa mwenye dhambi asiende jehanamu? Hii haihusu matendo mema katika kutafuta kutendewa mema. Kamwe huwezi kumpendeza Mungu kwa juhudi zako binafsi, kutumia akili nyingi, wala kuwa na elimu ya Mungu ya hapa duniani, wala kujitoa kwa kiwango cha kafara kama mambo haya hayatafanyika sambamba na kuokoa nafsi.

Huruma ni kujitoa mwenyewe kwenye upendo ili nafsi zipate kuokolewa. Timiza hilo kwanza ndipo utatimiza Amri Kuu mbili, kwa ujumla wake, Torati na manabii.

## Isaya 58 – Ahadi ya Mungu ya Baraka

Je unapenda kufahamu jinsi ya kupata kibali cha Mungu ili asikujibu maombi tu bali pia azimwage baraka zake kwako ambazo usingeweza kuwa nazo? Jibu ni kuwaonea huruma waliopotea. Jambo hili ni muhimu sana kwa Mungu.

Isaya 58 inaanza na kilio ambacho kanisa lisilo na uamsho linapaswa kujitambua: Mbona tumefunga lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu lakini huangalii? Tumezitunza amri; tunamkaribia Mungu kwa nia; lakini hakuna kinachotokea. Kwa nini, Mungu? Tatizo ni nini?

Niliwahi kuendesha huduma za uamsho nchini Nigeria miaka mingi iliyopita pale mtumishi wa Mungu aliponiomba kufika kwenye kongamano la wachungaji alilokuwa ameliandaa jijini Abuja. Alisema walijaribu kila kitu walichodhani kingemfanya Roho Mtakatifu atembee, lakini bado hapakuwa na uamsho. “Kuna makosa fulani,” alisema, “na tunahitaji kufahamu ni yapi hayo.” Haikuwa suala la kile walichofanya; ilikuwa ni suala la kile ambacho hawakuwa wamefanya.

Tunafunga na kuomba, lakini tunaombea nini? Je tunazitesa nafsi zetu kwa ajili ya wengine, au kwa ajili ya maslahi yetu binafsi? Shabaha yetu ni ipi, sisi wenyewe au wengine?

Na tutazame kile nabii Isaya alisema:

> *Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? (Isaya 58:6).*

Lengo la saumu (kufunga) na kuomba kwako ni kufungua hivyo vifungo walivyofungwa wenye dhambi, kuwaweka huru mbali na nira ya mzigo mzito wa dhambi, yaani kuitua chini na kuwaacha huru. Siku zote watu hawachagui kwenda jehanamu. Wanajaribiwa na tamaa mbaya na tamaa za mwili na kuangukia katika kifungo cha utumwa. Mara tu wanapoingia kwenye kifungo, wanahitaji mtu

atakayekuja kuwasaidia kukwepa hicho kifungo na jehanamu. Isaya anaendelea kwa kusema hivi:

> *Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? (Isaya 58:7)*

Ni aina gani ya chakula nabii anaongelea? Ni Chakula cha Uzima. Ni aina gani ya nyumbani mwetu ambamo tunatakiwa kuwakaribisha maskini? Nyumba ya Mungu. Ni aina gani ya nguo tunayotakiwa kuwavika? Mavazi ya haki. Je tunawasaidia wenye njaa, maskini, na walio uchi katika Roho ili kuwafanya waanze kutembea na Mungu na kuwafanya wakue kiroho kama wanavyohitaji?

Mungu ametuahidi kwamba kama tutageukia matendo ya rehema, nuru yetu itawaka ghafla kama asubuhi, kama mwangaza wa jua baada ya muda mrefu wa kukaa gizani:

> *Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. (Isaya 58:8)*

Unapitia mapito magumu na kutangatanga? Kwa nini upitie hali ngumu namna hiyo? Je unapenda kuona nuru ikiwaka na kuangaza katika maisha yako ya kila siku? Inawezekana Mungu anakusubiri hadi utakapopanda mbegu ya rehema kwa wengine ili naye apande mbegu ya rehema kwa ajili yako.

Isaya anaendelea kusema katika msitari wa 8 kwamba kama tutalenga kuleta ustawi wa wengine, ndipo afya yetu itarejea haraka. Inawezekana wengi wetu wanateseka bila kutaka kwa sababu tu hawana rehema kwa waliopotea? Maandiko yanatwambia kwamba tutavuna tulichopanda. Kama hatutawaletea afya wanaotuzunguka, unawezaje kutegemea Mungu kukuletea afya? Hii inaweza kuwachukiza baadhi ya watu, lakini ninafahamu kwamba Mungu hutumia mateso kama dhana bora ya kutuondolea mateso maishani mwetu. Lakini kama tutafanya mambo haya ambayo Mungu ametuamuru, ndipo utukufu wa Bwana utatufuata utulinde.

Unapotembelea dukani, watu huhisi kwamba kuna kitu cha tofauti kwako? Wanaweza kuhisi joto la mg’ao wa utukufu wa Mungu unaokuzunguka? Huhisi harufu ya mafuta ya upako wa Mungu ulionao? Unahitaji uishi kwenye uwepo wa Mungu namna hiyo? Kama unahitaji, basi badili mtazamo wako kuhusu watu wanaokuzunguka ambao wako njiani kuelekea jehanamu na wanahitaji mtu wa kuwasaidia, na

kuwahudumia ili Mungu aweze kukubariki na wewe pia.

> *Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. (Isaya 58:8)*

Rafiki yangu mmoja aliwahi kusema kwamba heshima ya kweli siyo wakati mtu unapokuwa na nafasi ya juu wala ya chini bali ni pale Mungu anapokuwa anasikia maombi yako… na kuyajibu. Oho, ili kumlilia Mungu na kufahamu kwamba siyo tu amesikia kilio cha mtumishi wake bali pia amekuitikia, "Niko hapa," ni pale anapojibu ombi lako! Je kuna heshima nyingine kubwa kuliko hiyo?

> *Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; (Isaya 58:9)*

"Lisha wanakondoo wangu," Yesu alimwambia Petro kama kweli alimpenda. "Lisha kondoo zangu." Wito rahisi wa Mchungaji wetu Yesu ni kuwaonyesha wengine rehema ile ile aliyotuonyesha sisi. Kama tutafanya hivyo, Mungu ametuahidi baraka hizi nzuri na kutuongoza katika Roho wake na kutulinda.

Atakuinua kama nuru gizani ili wengine waweze kuuona utukufu wake ndani yako. Hatakuacha katika giza fulani kwenye pembe ambapo hautajulikana. Akiwa kama mfanya biashara bora anayethamini rasilimali zake zote na kuzitumia kupata faida, atakutumia kwa namna uliyokuwa hutegemei kwa sababu ulipanda mbegu ya rehema. Wakati wengine watateseka kwa sababu ya ukame na njaa ya kiroho, Mungu atalikumbuka agano lake pamoja nasi kwa sababu tulifikisha rehema kwa wengine.

> *Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui. (Isaya 58:10-11)*

Ni katika nguvu za kupanda rehema ndipo tutaikunjua mikono ya Mungu maishani mwetu. Hawezi kulipinga Neno lake mwenyewe. Tunavuna tulichopanda. Tunapopanda rehema, ndipo tunafungua mlango wa Bwana kututumia. Kama hatuna rehema kwa wengine, basi maisha yetu ya Kikristo yatakwama kwa sababu hapatakuwa na nguvu ya Mungu

inayoyaendesha ndani yake. Baraka ambazo zinapatikana kwenye ahadi za Mungu zinaweza tu kutumika ikiwa tutatimiza masharti ya Neno lake. Kama unamtaka Mungu abariki huduma yako na kukutumia kwa namna isiyo ya kawaida, panda rehema na nuru yako itakujilia mara.

Na nihitimishe mada hii na ahadi moja zaidi kutoka kwenye Neno la Mungu:

> *Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. (Isaya 58:12)*

Hii ni ahadi ya mwisho kwenye hii sura ya Isaya ambayo inatupatia siri ya uamsho. Kama tutaitikia kwenye wito wa kwenda tuiangaza nuru ya Mungu gizani, tutajenga misingi ya kanisa ambayo ilishavunjika tangu miaka mingi ya ukengeufu na kumwacha Mungu. Tutakuwa kama Nehemia, aliyeujenga ukuta wa ulinzi kuzunguka Hekalu na kurejesha njia ya uamsho. Ndipo tutaudai utukufu wa Mungu urudi katika kanisa.

Ni wito wa namna gani ulivyo! Ni urithi wa namna gani ulivyo! Katika umilele, wengine watatujilia na kutwambia, "Oho, tunajua ninyi ni akina nani. Ninyi ni watu waliojenga upya yaliyobomoka na kuleta uamsho mkubwa katika siku za mwisho."

Hii ni ahadi ya Mungu. Ahadi zake ni hakika. Kama utaitikia kwenye wito wake, atalitimiza Neno lake kwako. Masharti yake ni rahisi: watendee wengine kama unavyotaka wewe watu wakutendee. Panda mbegu ya rehema, pumua huruma, mwaga maisha yako kwa wengine. Beba msalaba wako na kumfuata Yesu, naye atakuongoza kwenye utukufu wake.

Kwa upendo ninaamini kwamba kama tutakataa kuwa na rehema kwa waliopotea tutasimama mbele za Mungu katika hukumu na kutoa hesabu kwa nini tulikataa kutii hii amri. Baada ya yote yaliyoandikwa katika Neno lake, kuikataa hii amri moja tutaonekana kama waasi halisi. Kama vile Yakobo alivyosema, “Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi” (Yakobo 4:17).

Huwezi kusema kwamba hukujua. Biblia imejaa maagizo mengi yanayohusu kushuhudia kwa waliopotea na kufanya wanafunzi.

Sulemani mwenye hekima aliandika:

> *Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe. Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye? Je! Hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake? (Mithali 24:11-12).*

Kuhusu suala hili, mahali hapa kuna mada kuhusu rehema. Sote tunaihitaji – na hasa tutaihitaji zaidi katika Siku ya Hukumu – lakini rehema haiji bila gharama. Watu wengi wa kanisa hudhani, wakiwa na vijisababu kadhaa, kwamba kwa sababu tu wanakwenda kanisani basi watastahili rehema za Mungu, lakini hii siyo sababu. Unatakiwa kupanda mbegu ya rehema ili upate rehema. Na kulingana na Yakobo 2:13, kama hukuonyesha huruma [rehema], haitakuwepo rehema yoyote kwako katika Siku ya Hukumu.

Mchungaji wangu alipenda kutwambia kwamba kama hutapanda mbegu za rehema katika bustani yako, kamwe hapatakuwepo na tunda la rehema mahali hapo pindi utakapohitaji kuvuna rehema. Mithali inatwambia kwamba,

> *Azibaye masikio yake asisikie kilio cha maskini, Yeye naye atalia, lakini hatasikiwa. (Mithali 21:13).*

Fikiria, itakuwaje kama vitu vyako vyote unavyovitegemea kukupa usalama katika maisha yako vitachukuliwa vyote kisha uachwe kwenye milango ya bahari. Utamtegemea Mungu akuokoe, lakini utakapomlilia, hutapata majibu. Badala yake, utapokea huo ukimya uliokufa unaotoka kwenye mlango unaofungwa. Utaita kwa ajili ya rehema, lakini hakutakuwa na chochote kwa sababu hukupanda mbegu ya rehema kwa maskini, yatima, wala

waliopotea. Uliishi tu kwa ajili yako mwenyewe. Na sasa, unapolihitaji hilo tunda la rehema, hakutakuwa na chochote juu ya mti.

Unaona jinsi ilivyo mbaya? Fikiri kile Mungu anasema kwenye Mithali 1:24-32 kwa ajili ya wale waliokataa kumsikiliza Mungu alipoita na waliyakataa marudia yake: Atawacheka na kuwadhihaki siku ya msiba wao na hofu yao ifikapo.

Kama hatutasikiliza wito wa Mungu wa kwenda na kupanda rehema, nasi pia tutakapomwita, tutapokea mwitikio ule ule ambao tulimwitikia yeye.

## Hukumu ya Kondoo na Mbuzi

Hii ni moja ya aya zinazochoma zinazohusiana na somo hili linalokabiliana nasi kwenye mfano wa Yesu kuhusu hukumu ya kondoo na mbuzi (Mathayo 25:31-46). Alisema Mfalme atawabagua waendao mbinguni na waendao jehanamu, siyo kwa matendo ya kibinadamu wala kutimiza sheria za kidini wala kwa kujihesabia haki, bali kwa jinsi walivyokuwa na wasivyokuwa na huruma kwa waliopotea na wahitaji.

Ataanza na kondoo kwanza na kuwachukua mbinguni na kuwasifia wakiwa mbinguni. Kwa nini? Kwa sababu Bwana alipokuwa na njaa, kiu, uchi, mgonjwa, gerezani, au mgeni, walimhudumia. Kisha atawageukia mbuzi na kuwahukumu katika jehanamu kwa sababu wao hawakumhudumia.

Nini kitafanya tofauti kati ya kondoo na mbuzi, na hii utaitumiaje maishani mwako? Unapowaona watu wakiwa katika kifungo cha dhambi, huwa unawatembelea kwa kuwashuhudia injili? Unapowaona watu walio na njaa ya Kweli, huwa unawalisha kwa Chakula cha Uzima? Unapowaona wana kiu, huwa unawapa Maji Yaliyo Hai? Huwa unawavika kwa vazi la haki? Je umewahi kuwaalika kuja kanisani? Au umewahi kuketi kanisani na kufikiria kuhusu hilo, kwamba wanahitajika kuingia kanisani ili nao waokolewe? Umewahi kugundua kwamba kutojali maisha ya wengine na ukosefu wako wa huruma ya kweli inawezekana ndio jambo ambalo liliwazuia wengine wasiokoke?

Mbuzi watajibu, "Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie?" Lakini jibu kutoka kwa Yesu litakuwa hivi, "Amin, nawaambia, kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi" (Mathayo 25:45).

Ni maneno yanayochoma. Je hujawahi kuwaona hao walio wadogo wakiwa karibu nawe kwenye safari ya kuelekea uzimani? Au unafikiri kwamba wajibu wako pekee ni kumhudumia Bwana pekee? Kwa bahati mbaya, ibada nyingi za Jumapili hujazwa na watu wanaojidhania wao kuwa ni Wakristo ambao hufikiri kwa kujionyesha kwao kanisani ni kwamba watakuwa wamemtumikia Mungu. Hawashawishiki wala

kulazimika kupeleka ujumbe wa Injili mbali zaidi ya mlango wa mbele wa kanisa lao. Hawa ni mbuzi.

Maoni ya mwisho ya Yesu kwao ni haya: "Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele" (Mathayo 25:46).

Bwana anachukulia ukosefu wetu wa huruma kwa nafsi zilizopotea kuwa ni uovu, lakini pia anachukulia huruma yetu kwa wengine kuwa ni haki. Tunawezaje kutegemea Mungu kuleta uamsho kama hatutubu dhambi yetu ya ukosefu wa huruma, kukataa kuwapatia wenye dhambi maneno ya uzima ambayo tumepewa? Huruma husababisha uamsho. Bila hiyo, siyo tu tutakuwa tumejitenga na uwepo wa Mungu, bali pia tutajiweka wenyewe katika hali ya kukataliwa.

Sasa tena, Neno la Mungu linatwambia nini cha lazima tunachopaswa kukifanya:

- *Kwa mtu mwenye fadhili [huruma] utakuwa mwenye fadhili [huruma]. (2 Samweli 22:26)*
- *Upendano [rehema] husitiri wingi wa dhambi. (1 Petro 4:8)*
- *Maana hukumu haina huruma [rehema] kwake yeye asiyeona huruma [rehema]. Huruma hujitukuza juu ya hukumu. (Yakobo 2:13)*
- *Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi. (Yakobo 4:17)*

Haya maneno yanatosha kutufanya tukae tena chini na kujitathimini tena katika kutembea kwetu kama Wakristo. Tumekwishawatembelea wagonjwa na walio karibu na kufa na kuhakikisha hatutofautiani nao? Tumekuwa na vijisababu gani vya kujiteteatetea ili kuwapuuza wale wanaoelekea jehanamu kutoka katika watu wanaotuzunguka?

## Mfano wa Talanta

Miwili kati ya mifano Yesu aliyowashirikisha wanafunzi wake—mfano wa talanta (Mathayo 25) na mfano wa fedha (Luka 19)—kimsingi hutusimulia kuhusu somo moja. Somo hilo ni kwamba Mungu ametupatia sisi sote karama na vitu fulani vya thamani ambavyo tunatakiwa kuvipeleka ulimwenguni na kuvitumia kuutangaza ufalme wa Mungu. Watumwa wawili katika mifano yote hawakufanya hivyo. Mmoja aliificha talanta yake iliyo moja tu chini ya ardhi, mwingine aliificha fedha yake katika leso.

Wote walijua kwamba Mungu alikuwa ni "mtu mgumu." Basi, kwa nini hawakufanya kile Mungu alikuwa amewapa kufanya? Walijua kile Mungu alitegemea wafanye. Hiki hakikuwa kisa cha ujinga wala upumbavu. Walikataa. Hawakutaka hata kuiweka kwa watozao riba ili Bwana apate faida ya hicho kitu. Kwa maneno mengine, hawakutoa hata zaka ili angalau mtu fulani mwingine akitumie [hawakuwakabidhi

wanafunzi wapya waaminifu ambao wangewakabidhi na wengine]!

Na Mungu alifanya nini kwao kwa sababu ya dhambi yao hiyo? Kwenye mfano mmoja, alimwita mtumwa "mwovu" na kwenye mwingine alimtupa mtumwa kwenye "giza la nje." Mahali hapo sio mwonekano wa mbinguni. Hapa ni mahali palipoandaliwa kwa ajili ya wenye dhambi [jehanamu].

Je hii mifano ina tofauti na mfano wa karamu kubwa? (Luka 14) Kwenye mfano wa karamu kubwa, kila mmoja aliyealikwa alitoa vijisababu vya kwa nini hakutaka kumtumikia Bwana, na matokeo yake, Bwana akakasirika. Amri yake bado ni sawa leo:

> *Yule mtumwa akaenda, akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa. (Luka 14:21,23)*

Nini kitatokea kwa watu waliotoa udhuru? Miongoni mwa wale walioalikwa lakini hawakuitikia wito, hakuna hata mmoja atakayeionja karamu yake. Kwa nini? Kwa sababu walilenga juu ya ubinafsi wao

wenyewe badala ya kumtumikia Bwana, na waliikosa karamu ya Mwanakondoo.

## Mfano wa Msamaria Mwema

Katika Luka, mwanasheria, akitafuta kujihesabia haki mwenyewe na kumshitaki Yesu, alimwuliza Yesu swali muhimu sana maishani: "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" (Luka 10:25). Hili ni swali nambari moja la siku zote. Nawezaje kuikwepa kuzimu au jehanamu? Huyu mwanasheria alidhani angemkamata Yesu kwa kutumia kanuni na sheria ambazo zingemwepusha na ujumbe rahisi wa Yesu. Lakini Yesu alimjibu kwa kutumia mfano wa Msamaria Mwema (Luka 10:30-37).

Mfano unaanza na mtu aliyesafiri kutoka Yerusalemu kutelemka Yeriko. Yerusalemu ni mji ulioko ukanda wa juu katika Israeli, mji wa Mungu, wakati Yeriko, ulioko karibu na Bahari ya Chumvi, ni mji ulioko chini katika Israeli na unachukuliwa kuwa ni mji wa dhambi, mji ambao Yoshua aliulaani. Kwa hiyo huyu mtu alikuwa katika njia ya uzima akirudi nyuma katika dhambi. Akiwa njiani, ibilisi alimvamia na kumwacha karibu na kufa katika hali ya uchafu, katika dhambi zake pembezoni mwa njia.

Kuhani akapita njia ile—mtumishi, mchungaji, askofu, au aina nyingine ya mtumishi wa kanisani—mtu wa Mungu ambaye tunategemea atakuwa wa kwanza kuwanyoshea mkono wa huruma wale waliopotea na

walio karibu na kufa katika dhambi. Lakini kuhani alifanya nini? Alipita upande mwingine wa njia na kumwepuka kabisa mtu aliyekuwa anakaribia kufa! Alichofikiria ni kama kusema, "Hapana, huyu mwenye dhambi angekuwa amekuja kanisani kunisikiliza ninachohubiri, basi angeokolewa. Lakini hakuja, sasa na afe katika dhambi zake mwenyewe. Sawa, huu ndio uchaguzi alioufanya, sasa na akome kabisa." Na hivyo basi, mchungaji alipita njia ile na kumwacha ameanguka na kuchafuka!

Baadaye alipita Mlawi. Walawi walikuwa ni watumishi wa hema ya kukutania kama tu tulivyo sisi watumishi wa kanisa. Hivyo basi, alikuwa kama walivyo Wakristo wa leo waendao kanisani tu. Kwa kweli alipaswa kumsaidia huyu mtu. Alikuwa njiani kuelekea kanisani, msafi na aliyevaa mavazi ya ibada ya Jumapili. Lakini kama angesimama kumchukua mwenye dhambi, usafi wake, nguo zake mpya zingechafuka zote kwa uchafu na damu, na kisha angechafuka mno hata asiweze tena kwenda kanisani kwenye ibada.

Huyu Mlawi, mtu mtanashati muumini wa kanisani, alifanya nini? Alifanya kitu kile kile kama alivyofanya kuhani! Alimpita pembeni na kumwacha katika hali ya uchafu ili afe. Na hasa hasa, Mlawi alionelea kwamba huyu mwenye dhambi alikuwa ni mlevi, malaya, au mwenye tabia nyingine ya watendao dhambi aliyechakaa ambaye yawezekana kamwe

hakustahili tena kuokolewa kwa vyovyote vile na juhudi zozote za kumwokoa zisingekuwa na faida yoyote.

Ni watu wengi miongoni mwetu hatujafanya jambo kama hilo la kuokoa nafsi tulipokuwa tunaelekea kanisani siku ya Jumapili, tulifikiri kwamba tutatimiza jukumu letu kwa kujifanya watu wa dini, wakati wote tuliupuuza wito wa Agizo Kuu la Yesu wa kuwaokoa waliopotea walio jirani na sisi walio katika kufa na dhambi?

Lakini baadaye Msamaria alipita njia ile. Wasamaria walichukuliwa kuwa ni watu wa chini sana katika jamii ya Uyahudi. Siyo tu kwamba Msamaria alisimama, bali pia alimpaka aliyeanguka njiani divai na mafuta kwenye vidonda vyake. Hapa divai inawakilisha Roho wa Mungu na mafuta yanawakilisha mafuta ya Roho Mtakatifu. Huyu mtu alimwombea mwenye dhambi mara hiyo akiwa katika hali yake ya uchafu! Kisha akamchukua mpaka katika nyumba ya wageni (kanisa) ambamo alimsihi mhudumu wa nyumba ile kuhakikisha huyo mtu anatunzwa mpaka Msamaria atakaporudi.

Sasa basi, swali la kwanza lilikuwa ni lipi? Lilikuwa linataka tuwe Wakristo au tufanye matendo mema? Hapana! Swali lilikuwa ni kama hivi, nifanye nini ili niikwepe kuzimu? Jinsi gani naweza kuikwepa hukumu/jehanamu? Hatima yako ya milele haitegemei nafasi yako kanisani wala jinsi gani unaonekana kuwa

msafi katika kuvaa na kutembea kwako kama Mkristo. Hii inahusiana na kuwa mwenye huruma kwa waliopotea na wanaotaka kufa. Hilo ndilo jibu Yesu alilitoa, na yeye ndiye pekee utakayesimama mbele zake. Unaweza kuchagua kile ukipendacho, lakini kama ilivyo kwangu, sitaki kuishia mahali fulani kama kuhani na Mlawi walivyofanya. Walichagua kumpuuza aliyepotea akiwa katika hali ya kufa kadiri walivyotembea katika njia yao ya uzima, wakifikiri kwamba haki yao itatosha kuwaokoa. Neno la Mungu linatupatia onyo kali kuhusu kuwapuuza waliopotea.

> *Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe. Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye? Je! Hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake? (Mithali 24:11-12).*

## Kipofu Bartimayo

Ninapokuwa nahubiri kanisani huwa natumia aya nyingi za Maandiko kuhusu uamsho, lakini mara nyingi hupenda kuhitimisha na ujumbe mmoja: habari ya kipofu Bartimayo (Marko 10:46-52).

Kwenye habari ambayo Yesu alikuwa akipita katikati ya Yeriko, kuelekea Yerusalemu kuuwawa, kadiri alivyokuwa akipita, ndivyo mji wote walivyokuja kukutana naye. Hii ilitokea mwishoni mwa huduma

yake, hivyo kila mtu alikuwa tayari anamfahamu yeye ni nani na alikwishasikia kuhusu miujiza yote Yesu aliyofanya. Kila mtu alikuwa pale: liwali, wanasiasa, maaskofu na wachungaji, watu wote wa kanisa. Kila mmoja alitaka kufurahia kuwa karibu na Mtu huyu ambaye wengi walimwamini kama Masihi.

Akiwa njiani, mwombaji kipofu alikuwa akikaa pembeni mwa njia. Kwa sababu alikuwa kipofu, alitengwa na jamii na kuchukuliwa kuwa mchafu. Hakuna hata mmoja aliyetaka hata kumgusa la sivyo wangenajisika. Hapakuwa na masuala ya kumsaidia, hata nyumba yake ilimkataa. Alichofanyiwa tu ni kuachwa pembeni mwa njia katika hali ya uchafu, akiombaomba, akidondokewa na kinyesi na mkojo wa wanyama waliopita mahali hapo. Akiwa na njaa kali, aliombaomba tu riziki kutwa nzima. Lakini hiyo haikuwa nafasi mbaya sana. Nafasi mbaya sana ilikuwa, hakuwa na tumaini. Kwake kesho ilikuwa ni kama leo, na hata mbaya zaidi. Siku zote alikuwa kipofu, aliyekataliwa, mwenye kudhofika kwa njaa na kuombaomba.

Lakini baadaye alisikia kwamba Yesu alikuwa anapita katika njia hiyo! Huyu Yesu alikuwa ni Mtu aliyekuwa ameshaponya vipofu wengi. Alikuwa ameshawatakasa wenye ukoma, kufufua wafu, na kunena kwa mamlaka ya nguvu za Mungu! Hii ndio ilikuwa nafasi yake ya mwisho, nafasi maishani mwake!

Na Yesu alikuwa akipita karibu naye. Alihitaji kukutana na Yesu!

Hivyo, alianza kupaza sauti, "Mwana wa Daudi, Yesu, unirehemu" (msitari wa 47). Lakini watu wa kanisa walimfanyia nini? Walimwambia anyamaze. Walichomwambia ni kama kusema, "Usimchoshe Bwana. Wewe ni mwobaji tu aliyelaaniwa, mchafu aliyechakaa! Inawezekanaje upaze sauti kwake namna hiyo!"

Lakini Bartimayo aliendelea kupaza sauti, "Mwana wa Daudi, unirehemu" (msitari wa 48).

Ndipo Yesu akasimama. Akawaamuru wanafunzi wake kumleta Bartimayo kwake na akamwuliza, "Wataka nikufanyie nini?" (msitari wa 51).

Bartimayo akajibu, "Mwalimu wangu, nataka nipate kuona" (msitari wa 51). Aliishi gizani na hakuona. Kwa huzuni alitaka nuru ya Yesu Kristo, alihitaji kuokolewa na kufunguliwa asife akiwa mwenye dhambi. Alimhitaji Yesu kuiokoa nafsi yake!

Wakati fulani niliposoma habari hii, Bwana alinifunuliwa kwamba kwa sababu kulikuwa na watu wengi wakimzunguka Bwana, isingewezekana kwake kumsikia Bartimayo kwa kutumia masikio yake ya kimwili katikati ya makelele ya watu. Haikuwa sauti yake ambayo Yesu aliisikia. Alisikia kilio cha moyo wa mtu kipofu. Hiki ndicho kilichomfanya Yesu asimame njiani. Aliusikia moyo wa kipofu ukimlilia.

Rafiki, unaweza kuisikia sauti ya watu kama huyo kipofu? Sauti hiyo haitoki ndani ya kanisa lako; inatoka nje kwenye mitaa ya watu maskini, vipofu, wagonjwa, viwete na vilema—kutoka kwa wale wasiokuja kanisani. Ni sauti ya moyo wa mtu kipofu. Au sisi ni kama watu waliomzunguka Yesu wakiwa na mwonekano wao wa kidini lakini wakiwaambia wagonjwa na vilema wa kiroho kunyamaza? Je tumefikia kiwango cha kutosheka hata tusisikie kilio cha waliopotea?

Ee Mungu mpendwa, naomba utusamehe. Utusamehe kwa "kuwa na kanisa." Tumesahau ulituokoa kwa ajili ya nini.

## Habari Moja ya Mwisho

Uniruhusu nikwambie habari moja ya mwisho katika sura hii inayoonyesha hii kanuni. Miaka michache iliyopita, nilikuwa kwenye mkutano wa maombi ya uamsho wakati wa jioni (angalau hicho ndicho walichoitisha), na nikagundua kwamba watu waliokuwa hapo walikuwa wakiombea makanisa yao, wachungaji wao, wagonjwa, vyombo vya muziki—kila kitu na kila mtu, isipokuwa nafsi zilizopotea! Nilishangaa kwa nini walikuwa hawaombei jambo la maana sana ambalo ndilo linahusu uamsho?

Nilipokuwa nimekaa pale, Bwana akanionyesha maono: niliona gati ikiwa imechomoza baharini. Ilikuwa na upana mara mbili ya gati ya kawaida na ilikuwa

imejaa watu. Ilikuwa ni siku nzuri wakati wa mchana, na watu waliokuwa kwenye gati walivaa nguo za kupendeza zenye rangi za kuvutia. Kila mmoja alionekana kuwa mwenye furaha, na nikaweza kuiona furaha ya Bwana kwenye nyuso zao. Watu hawa kwa kweli walikuwa wameokoka wakimsifu Yesu. Kila mmoja alikuwa akimtembelea mwenzake ili kumbariki. Wengi wao waliweka mikono yao juu ya watu na kutabiri juu yao kuhusu mambo yote yaliyo ya ajabu. Yalikuwa ni maono ya ajabu jinsi gani!

Na kisha maono yangu yalipanuka hadi kwenye bahari iliyokuwa ikiwazunguka. Kwa utofauti mkubwa na rangi nilizoziona zikimeremeta kwenye gati, bahari ilionekana nyeusi na baridi katika rangi ya shaba na bluu nyeusi, karibu yote ilikuwa kama nyeusi na nyeupe. Maji yalikuwa hayajatulia yenye mawimbi yaliyoenea kila mahali. Kutoka juu ya maji nikaona mamia ya watu wakitapatapa kwa kuzama, na kupunga mikono yao hewani na kulia wakiomba msaada kadiri mawimbi ya bahari yalivyokuwa yakiwasukuma huku na kule. Nikajaribu kuwaita watu waliokuwa juu ya gati ili waende kuwasaidia hao watu waliokuwa wakizama, wawatupie maboya yatakayookoa maisha yao. Au kama haikutosha sana, kuogelea majini na kuwavuta mpaka mahali salama. Lakini hakuna yeyote aliyenisikia. Waliendelea tu kubarikiana, kutabasamu na kuwa na wakati mzuri.

Ndipo nikagundua, haikuwa kwamba watu waliokuwa kwenye gati hawakujali kuhusu watu waliokuwa wakizama pembeni mwao. Oho, walijali, sawa sawa. Ila hawakuweza kuwasikia. Masikio yao yalijawa na masuala ya kanisa hata wasiweze kuzisikia sauti za vilio vya watu waliopotea.

> *Azibaye masikio yake asisikie kilio cha maskini, Yeye naye atalia, lakini hatasikiwa. (Mithali 21:13).*

# Sura ya 9

# Nenda Kaokoe Nafsi!

Uamsho hauhusiani na kutafuta kujisikia vizuri, kuwa na huduma nzuri, wala kuhusu miujiza. Uamsho unahusiana na kuokoa nafsi. Ili kufanya hilo, tunatakiwa kuwashirikisha injili nafsi za watu waliopotea. Hii siyo mbadala wala jambo unaloweza kuachana nalo. Ni kiini cha wazo lote la injili.

Yesu alipotoa Agizo Kuu, alisema, "Enendeni," siyo "Kaeni." Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio Injili, siyo wakaao nyuma ya mabenchi kanisani! Unapaswa kwenda mahali walipo waliopotea. Hawatakuja kanisani kwa kufikiria tu.

Kwenye makanisa mengi huwa nayaita kama Makanisa yenye Viti vya Plastiki. Hata hivyo hakuna hata mmoja ambaye huelewa namaanisha nini. Katika makanisa mengi Afrika, hayana mabenchi wala viti vizuri. Yana viti vya plastiki vya bei nafuu kama vile unavyoviona katika soko la Walmart. Mimi huchukua kiti na kukiweka katikati ya chumba na kuendelea kujinyosha juu yake. Hupiga miayo na kujikunyata kama vile ninasinzia, kisha huinua kichwa changu na kumwagiza mhudumu wa mlangoni kutazama nje barabarani ili aniambie kama kuna watu wamekuja. Hapana? Vema, naomba mtu mmoja aniamshe mara mtakapowaona wanakuja.

Wote hucheka wanaposikia hivyo. Wote hufahamu nini ninachomaanisha. Na kisha, huwatazama moja kwa moja na kuwaambia kwamba, hapana, hawatakuja. Kwa nini watu hawatakuja? Na unajua kwa nini wasije? Kwa sababu wanaogopa kwamba wao pia watakuwa kama wewe, kukaa tu kwenye kiti cha plastiki kanisani, kufahamu ukweli kuhusu Wokovu na Hukumu, lakini bila kwenda nje kuwaambia wengine.

Unafikiri nimenena vibaya? Hufikirii kwamba hilo ni kweli? Hebu nenda kawaulize [hasa waokoao nafsi] kwa nini hawaji. Watakwambia. Kama kwa uaminifu watu wanafikiri kwamba nguvu za Mungu zipo katika kanisa lako ili kuwaponya, basi waponye, na uwaokoe, unadhani kwamba hawatakuja? Lakini hawaji, hii ni kwa sababu hakuna moto wa kutosha katika kanisa lenu kwa ajili yako kukuwezesha kwenda kuwaalika. Ukumbuke mfano wa kondoo na mbuzi. Yesu alisema kwamba alipokuwa huko nje, watu walio mbuzi hawakumkaribisha nyumbani mwao. Kwa maneno mengine, hawakumwalika kuingia katika Nyumba ya Mungu, ni hicho ndicho kilichowahukumu mbuzi kwenda katika jehanamu.

Mimi ninapokuwa ninahubiri kwenye kongamano la uamsho, mara nyingi hutumia muda wote wa huduma kwenye hili jambo moja tu. Nikitumia aya hadi aya nyingine, kama nilivyofanya kwenye kitabu hiki, ili kuthibitisha, kulingana na Neno la Mungu, kama utakosa rehema kwa waliopotea, basi kuna siku

utajikuta mwenyewe ukikabili kiti cha Rehema cha Kristo bila kuonewa rehema ya kutosha kukiendea. Kama unataka uamsho, hiki ndicho uamsho unamaanisha: "Bwana, nipe nafsi, la sivyo, nitakufa mimi!"

## Jinsi ya Kufanya Jambo Hili

Lazima ieleweke kwamba lazima uwepo moto ukiwaka katika kanisa kabla hujaanza kuleta/kuingiza nafsi mpya; vinginevyo, nafsi zitakazoingia zitarudi nyuma na kutoka nje. Nafsi hizi zinahitaji kitu halisi, siyo vitu vilivyoigwa kirahisi rahisi tu. Hata hivyo, mara baada ya moto kuwaka, ndipo huwa rahisi kuokoa nafsi, kwa sababu wewe mwenyewe [na kanisa] mtakuwa mmehamasika na kile kinachoendelea kanisani kwenu! Waliopotea hawasikilizi maneno yanayohubiriwa wala kusoma vipeperushi vya Injili utakavyowapatia kadiri wasivyomwona Kristo ndani yako. Unapohamasika, ndipo watauona moto ndani ya macho yako. Ni roho yako ndiyo huzungumza na wao kuliko kitu kinginecho.

Usifanye kosa la kushuhudia kitu ambacho ni kigumu kukifanya. Huna haja ya kuwa na shauku kuhusu kuwa mhubiri, kujua Maandiko mengi, kuwa na majibu ya maswali ya waliopotea, au hata kumshawishi mtu yeyote ili aokolewe. Jambo kubwa unalotakiwa kufanya ni kuwaalika kuja kanisani. Hivyo ndivyo ilivyo! Waalike kuingia kanisani. Rahisi sana.

Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kwamba ufanyapo karamu wawaite maskini, vilema, viwete, vipofu (Luka 14:13). Waambie tu kuja kanisani na watakutana na Yesu. Kama watakuja, vema! Wasipokuja, angalau utakuwa umetimiza wajibu wako wa kuwaalika.

Huna haja ya kutegemea kutumia Injili yenye gharama za vipeperushi vilivyo ghali. Kanisa nililokuwa nikihusika miaka ya sabini liliokoa nafsi 100,000 katika miaka 10, na yote tuliyokuwa nayo ni vipande vya karatasi za mraba tulivyovigonga muhuri na kuvigawa mitaani. Huna pesa? Hata sisi hatukuwa nazo. Vinginevyo labda utakuwa bora usipojali kushika mambo ya kidini.

Unaweza kufanya jambo hili. Kama kile ulichonacho ni muhuri wenye anuani ya kanisa lako, ratiba za ibada, na namba za simu, hiyo itafaulu. Gonga muhuri huo kwenye karatasi za mialiko kisha zipeleke mitaani. Kama utafanikiwa kuwa na kadi za huduma (business cards) utakazoambatanisha na mwaliko, hii itafaulu vizuri zaidi. Tumia upande wa mbele wa kadi yako ya huduma kuonyesha jina la huduma/kanisa lako, wapi na wakati gani ibada hufanyika, na namba za simu na barua pepe [na mtandao wa kijamii] ili watu waweze kukutafuta na kukupata. Utashangazwa utakapoona watu wakikupigia simu kukuuliza ili kuwaombea.

Upande wa nyuma wa kadi ya huduma ni silaha ambayo ni siri yako. Hapo ndipo unapoweza kuweka Mpango wa Wokovu. Hapa nimeorodhesha dondoo 6

za mpango ninaoutumia mimi. Unaweza kuzitumia kwa vyovyote zitakavyokufaa. Hivi ndivyo nilivyoweka nyuma ya kadi yangu:

**Mpango wa Wokovu**

1. *Mshahara wa dhambi ni mauti na jehanamu ipo.*
2. *Wote tumefanya dhambi na sote tunahitaji Mwokozi.*
3. *Yesu alikufa Msalabani kulipa deni la dhambi zetu na kutuokoa kutoka jehanamu.*
4. *Yesu alisema kwamba tusipozaliwa mara ya pili kwa Roho, hatuwezi kwenda mbinguni.*
5. *Kama tutamkiri Yesu kama Bwana na kumwomba atuokoe, atajibu na kuziokoa nafsi zetu.*
6. *Tutakapozaliwa mara ya pili kwa Roho, Mungu atatupatia nguvu za kuzishinda dhambi zote na kuweza kuishi maisha ya ushindi katika Kristo.*

Kile unachotakiwa kufanya ni kuwapelekea kadi na mwaliko na kuendelea kwenda. Kama kuna mtu anakuzuia ili kukuuliza swali, ni sawa! Kama sivyo, endelea. Hiyo mialiko midogo midogo itapeleka uzima, na Mungu itaitumia kushughulika na kuzishawishi nafsi alizoziweka mbele zako. Unachotakiwa tu kufanya ni kuwaalika. Mungu atafanya kazi itakayobaki, kama utampa nafasi.

Piga picha jambo hili, kama utataka. Charles amechukua moja ya kadi zako, hata hafikirii kuhusu kadi hiyo, na ameiweka kwenye mfuko wake. Jioni

hiyo, alipokuwa akitaka kwenda kulala, akaitoa kadi mfukoni. Mmmmh. Akairudisha tena mfukoni. Asubuhi iliyofuata, akaiona hiyo kadi tena alipokuwa akivaa nguo. Mmmmh. Akaiweka mfukoni tena. Baadaye jioni, akaitazama tena, na tena. Wakati huu wote, Bwana alikuwa anamshughulisha ili kumshawishi. Anajua Charles ni mwenye dhambi; anajua anahitaji kuwa sawa na Mungu, na anajua Mungu anaivuta nafsi yake kumwendea. Huhitaji kufanya kitu chochote! Mungu anamshughulisha Charles na kama Charles atakuwa tayari kuokoka, atakuja kanisani. Mungu atamleta! Huna haja ya kufanya kitu chochote. Mwache Mungu afanye kazi yake. Basi Mungu anakutaka umpe kadi Charles.

Luka 14:23 inatwambia tutoke nje katika njia kuu na vichochoro tukawashurutishe kuingia katika nyumba yake. Kushurutisha ni neno zuri imara. Lina maana ya kujali, kumlazimisha mtu. Zinaweza kuwepo nyakati za wewe kufanya hivyo, lakini wakati huo huo, kama utawaalika kuja kanisani na wakawa na njaa ya kuitafuta Kweli, watakuja.

Kuna njia zingine nyingi za kuwasilisha Injili, lakini siyo zote zitafanya kazi kwako. Mikutano ya hadharani, ambapo makutano hufika kwenye eneo lililo wazi lenye vyombo vya sauti ili waweze kusikia Injili ikihubiriwa, hii hufanya kazi sana barani Afrika kuliko Amerika. Nyakati zimebadilika, na ndivyo ilivyo kwa mbinu za uinjilisti pia. Kama mikutano ya hadhara itafaa kwako,

basi fanya kwa namna yoyote ile. Kama haitafaa, fanya kitu kingine kinachofanya kazi kwako. Weka kituo mahali fulani, peleka chakula cha bure kwenye jamii [mfano kwenye nyumba za wazee wasiojiweza, wagonjwa n.k.], saidia kufanya usafi kwenye mitaa inayozunguka kanisa na kisha waalike wakazi kuja kanisani. Hii pia haifanyi kazi yoyote kwako? Basi mwombe Mungu. Hii ni kampeni yake siyo yako, hivyo mwombe yeye akuongoze.

Usishangazwe kwa vile Bwana atakavyokuongoza kufanya. Na usimpe ibilisi nafasi ya kukwambia kufanya kile unachokiweza kumbe hukiwezi. Mimi nimeshawahi kusimama nje ya jengo la FBI mjini Washington DC, Marekani, kugawa vipeperushi. Hawakutuacha tuingie ndani ya jengo kugawa vipeperushi, hivyo tuliwaombea watoke nje waje mahali tulipokuwa. Fikiria nini kilitokea? Ulikuwa ni wakati wa gwaride la ushindi wa Super Bowl kwa ajili ya Washington Redskins, na kwa wakati muafaka tuliokuwa tunasimama mahali hapo tukishangaa shangaa nini cha kufanya, waliwaruhusu wafanya kazi wote watoke nje kutazama gwaride. Kwa ghafla, mamia ya wafanyakazi wa FBI wakatoka na kusongamana nje ya jengo, wote wakipitia njia yetu! Na hapo ndipo tulipokuwa, kuwapatia Injili mkononi. Usikishushe hadhi kile Mungu atafanya kwa ajili yako katika kukusaidia kuziokoa nafsi.

Haijalishi utazifikia kwa jinsi gani. Chochote ufanyacho, hata hivyo kifanye, kwa namna yoyote inayojitokeza, shuhudia. Uzima wako na wa wengine unategemea kwenye Injili. Hii ni siri ya uamsho.

Mara tu nafsi zitakapoanza kuja kanisani, zitachochea moto ambao utasambaa kwenye jamii nzima. Wanajamii watanusa harufu ya moshi wake. Na watakuja. Na hivyo ndivyo uamsho huanza.

# Sura ya 10

# Hatua za Utekelezaji

Hapa kuna hatua za kutekeleza ili kukufanya uanze uamsho katika mwelekeo sahihi:

## 1. Soma Biblia Kila Siku

Hatua ya kwanza ya kivitendo ili kulisaidia kanisa na waamini kujiweka sawa sawa kwa uamsho ni wewe mwenyewe kujijengea nidhamu ya kusoma Biblia. Dhana muhimu sana ambayo Mungu ametupatia ni Neno lake. Kusoma Neno la Mungu ndio mahali ambapo uamsho huanzia. Kwenye Neno ndimo tunamopata nguvu zetu. Bila Neno, hatuwezi kuwa na nguvu hata za kuomba, hatutajali kufahamu tunachokiomba.

Mungu atashughulika nawe kupitia Neno lake kuhusu mambo ya muhimu sana utakayokutana nayo katika siku. Siku yako itakuwa nyepesi na rahisi unapoanza siku na Neno. Usipofanya hivyo, utagundua kwamba, siyo tu kila kitu kitaonekana kuwa cha kuchanganyikiwa na kigumu zaidi, bali pia muda mwingi utapotea kwenye mambo yasiyo ya muhimu.

Hapa kuna hatua mbili za kivitendo kwa ajili ya kuharakisha kuanza kujisomea Biblia.

Anza kujisomea kila siku sura nzima ya kitabu cha Mithali. Kuna siku thelathini na moja katika miezi ya kalenda iliyo mingi na kuna sura thelathini na moja

katika Mithali. Soma sura inayoendana na tarehe ya siku hiyo. Mithali zitakupatia hekima na zitazungumza nawe unapokuwa kwenye hali ngumu.

Jiwekee nidhamu ya kufanya hivyo kama jambo la kwanza kila siku asubuhi. Mara tu baada ya tabia hii kuzoeleka, utaona kuna tofauti ndani yako.

Muhimu sana, mara baada ya kuifungua Biblia, ni rahisi sana kumwomba Bwana nini kingine anachotaka usome na kuendelea kusoma. Sehemu iliyo ngumu itakwisha pale utakapoketi chini na kuifungua Biblia. Ni rahisi sana kuendelea kusoma baada ya kuanza tayari. Hivi ndivyo unavyoanza kuwasha moto ndani ya moyo wako.

Kitakachofuatia, unda vikundi vya kujifunza Biblia. Utafurahia sana jambo hili na kwa wakati huo huo ukiwaimarisha kila mmoja na kanisa zima. Kuna njia mbili za kufanya jambo hili.

Tenga wakati wa jioni kanisani kwa ajili ya mchungaji au mtu mwingine aliye kiongozi ili aendeshe darasa la kujifunza Biblia. Nzuri zaidi itakuwa pale utakapofanya lifanyike darasa moja kila siku jioni. Hii itafanya wanafunzi katika uhalisia wake. Utahitaji kiongozi anayelijua Neno la Mungu vema na ana kiwango fulani cha mamlaka, ili kutaniko lisiwe kama kikao cha wakati wa mazungumzo au kama mahali pa watu wasiojifunza wanaoleta mambo yao tu mengine na kuchoshana bure katika ubatili wa mashindano ya maneno na midahalo.

Njia nyingine ya kivitendo iliyo na ufanisi ni kuunda vikundi vidogo vidogo vitakavyokutana majumbani mwao kula na kusoma Biblia. Kila mmoja wao ataleta kitu kwa ajili ya chakula. Ni fursa nzuri ya ushirika kama nini! Mtamega mkate wewe na makaka na madada, mtakula chakula kizuri, na kuketi mkizunguka meza moja na kusoma sura moja ya Biblia. Baadaye kidogo utahitaji kuiona hii sherehe ikiendelea kila juma. Utaongeza uelewa wako wa Neno, kuimarisha sumaku ya ushirika katika kanisa, kupata msaada kutoka kwa makaka na madada, na kuwa na mahali pa ajabu pa kuwaalika wengine kujiunga nawe. Nafsi zisizookoka pia zitakuja kwenye chakula na kuishia kuokoka, na Wakristo wachanga watajiona kumezwa ndani ya familia mpya yenye upendo. Hii hufanya kazi kwenye madaraja mbalimbali!

## 2. Jiwekee Muda wa Kuomba Kila Siku

Ule usemi wa zamani ni kweli, "Kama hauombi, hautakaa ukatulia." Bila kuwa na nidhamu ya muda wa maombi ambayo utakuwa umejipangia mwenyewe, mara nyingi utajikuta ukichanganyikiwa na mambo au kujichosha kwa kufanya kitu kisicho sahihi. Kamwe ibilisi hatakuruhusu upate muda wa kuomba! Karibu watu wote wanaume na wanawake wa Mungu wenye nguvu katika historia waliamka asubuhi na mapema kuutafuta uso wa Mungu. Nawe pia, amka asubuhi na mapema uombe! Mithali 8:17 inatwambia, "…wale

wanitafutao kwa bidii wataniona." Kama utasubiri mpaka ufike wakati ukufaao, utaishia bila kufanya maombi na bila kuwa na wakati kama huo na Mungu.

Tenga muda maalumu. Inuka mwenyewe na kuanza kuomba mara ufikapo muda huo. Kama una shida, basi mtafute ndugu atakayefanya agano nawe la kukutana kanisani au mahali pengine pa faragha ili kuomba wote kila siku. Utagundua pia kwamba kuna watu wengine wengi ambao pia wanahitaji nidhamu ya maombi ya kushirikiana kwa kukutana pamoja. Unaweza kuanzisha kikundi cha maombi ambacho kitaanza na kuvunja/kuangusha kuta za zamani za kimwili na uvivu ambazo daima zilikuwa zinazuia maombi yenu yasifanyike hapo kwanza. Kisha utaona nguvu za mbinguni zikianza kuwajilia/kutembea kwa jinsi ambayo hukutegemea. Huu ni wito ambao Mungu anatuita katika sura ya 2 ya Yoeli. Maombi ni muhimu kwa uamsho wowote ambao haujawahi kutokea.

Mara tu nguvu ya msukumo wa maombi kuanza kutembea, anza kutafuta fursa ya kuungana na waamini wa makanisa mengine katika jamii yako ili kujenga mnyororo wa maombi ya masaa 24 siku 7 kwa juma. Hii itayaunganisha makanisa pamoja katika jamii yako na itawasilisha umoja katika kuziangusha nguvu za giza.

Ni ushuhuda wenye nguvu namna gani huu! Siyo tu itaimarisha jamii yako nzima bali pia itazuia majaribio ya Shetani ya kusababisha migawanyiko katika mwili wa Kristo. Nabii Yoeli alisema kuhusu

jeshi la Wakristo katika siku za mwisho kwamba hapana hata mmoja amsukumaye mwenzake; huendelea mbele kila mmoja katika njia yake…wala hawaachi kuifuata njia yao (Joeli 2:8). Kwa maneno mengine, kutakuwa na nguvu ya usumaku kati ya viungo vya mwili na kwamba lazima tuutunze umoja. Maombi ni dhana isiyoepukika ya kutuleta kwenye umoja wa roho.

Miaka mingi iliyopita, nilihudumu kwenye makanisa mawili katika mji mdogo nchini Kenya ambapo nililitambulisha hili wazo la kutengeneza mnyororo wa maombi pamoja na makanisa mengine mjini hapo. Hakuna hata kanisa moja miongoni mwao lililokuwa na waumini wa kuyagawana masaa 24 ili kutengeneza mnyororo, hivyo nilipendekeza waungane pamoja kuunda mnyororo mkubwa mmoja wa maombi. Walishangazwa sana na wazo ambalo wote waliungana. Kulikuwa na makanisa saba mjini, kila moja kwenye moja ya njia saba zinazoingia mjini. Kila kanisa lilitumia muda wa mchana kwa kufunga <u>na</u> kuomba kwa ajili ya nafsi kuokoka. Baada ya mwaka, mchungaji aliwasiliana nami ili kunifahamisha kwamba tangu wakati ule walibeba huo mzigo, nafsi zilikuwa zikiokoka kila siku. Katika kila kanisa. Kwenye kila njia.

Wakati wa huduma ya Jesus Movement mwaka 1969, tulianzisha mnyororo kama huo wa maombi katika kanisa letu dogo nililokuwa sehemu yake mjini Hollywood, California nchini Marekani. Kila mmoja

alipata muda wa mombi waliyopangiwa ambayo waliwajibika. Tuliomba masaa yote kwa miaka kama kumi kwa ajili ya Mungu kuzileta nafsi kuokolewa. Na alizileta. Wakati wote wa hiyo miaka kumi, tuliona nafsi 100,000 zilizokuja madhabahuni na kumpa Yesu maisha yao. Daima mimi huamini kwamba chumba chetu cha maombi yasiyokoma kilikuwa ni tanuru lililowasha huo uamsho ambao hatimaye ulikwenda kwa ulimwengu na kuokoa nafsi nyingi mnamo miaka ya sabini.

Kuna kitu chenye nguvu kuhusiana na mnyororo wa maombi ya masaa 24/siku 7 ambayo humfanya Mungu atembee. Lazima anapendezwa na mtindo huo wa harufu ya uvumba usiozimika daima kutoka kwenye maombi ya watoto wake. Vyovyote itakavyokuwa, naweza kutoa ushuhuda kwamba hii humfanya Mungu atembee, na itafanya magurudumu ya uamsho yaanze kuzunguka.

## 3. Kuosha Miguu na Ushirika Mtakatifu

Kuna kitu chenye nguvu sana kuhusu kutaniko lililoungana katika Roho. Siku ya kwanza ya Pentekoste ilikuja pale waumini walipokuwa wote pamoja (Matendo ya Mitume 2). Naamini kwamba Siku ya pili ya Pentekoste itakuja ambapo kanisa litaungana tena kwa namna hiyo hiyo. Moja ya njia bora za kuwa na umoja ni kwa kutumia mtindo wa zamani wa kuosha miguu. Yesu mwenyewe alituachia kielelezo na

kutuagiza kuoshana sisi kwa sisi miguu yetu (Yohana 13:1-14).

Biblia hutufundisha kwamba wakati wowote tunapokuwa na kwazo na ndugu, tunatakiwa kumwendea huyo mtu na kujishusha na kupatana naye. Haijalishi ni nani aliye sababu ya kwazo au aliye sahihi au aliyekosea. Dhambi ya kujivuna kiroho haitambui huo utofauti. Hivi ndivyo Shetani husababisha migogoro na migawanyiko katika kanisa na, kwa kufanya hivyo, huharibu tumaini lolote la uamsho.

Mwendee mtu huyo uliyetofautiana naye, mwombe akusamehe kama umetenda au kunena jambo ovu ambalo lilimkwaza, na umwombe kumwosha miguu yake. Hii itaondoa roho yako ya majivuno kuliko ambavyo kitu kingine kingeweza kukuondolea. Mara baada ya kufanya jambo hilo, utofauti au mashitaka yoyote au yote yatapata suluhu na sumaku itatokea kati yenu ambayo itaharibu chochote Shetani amejaribu kukifanya kati yenu. Sasa fikiria hii itakuwaje kama itafanyika kwa kanisa lote. Tafuta wakati, likusanye kanisa lote pamoja, andaa maji, mabeseni na taulo za kuogea, kisha osha miguu ya kila mtu na kuifuta. Utajionea hali ya kanisa lote kusafishwa na uhuru kutokea ndani ya roho zenu ambayo itaruhusu imani yako kukua. Itatoa uhuru kwa Roho wa Mungu kuanza kutiririka.

Ushirika Mtakatifu [Meza ya Bwana] una kazi hiyo hiyo. Kumbuka, Maandiko hutwambia kwamba

yatupasa kufanya ushirika siyo tu kwa damu bali pia kwa mwili, ndugu zako katika Kristo. Kabla ya kushiriki Ushirika Mtakatifu, toa muda kwa kila mmoja kuwa na nafasi ya kwenda kwa mtu yeyote aliye na kwazo naye na kumwomba amsamehe/kumsamehe. Tena, ni muhimu kukumbuka kwamba siyo kuhusu nani amekosa na nani hajamkosa mwenzake; lengo ni kuponya majeraha yaliyomo katika mwili na kutia muhuri kwenye migawanyiko ambayo mshitaki wa watakatifu alijaribu kuitengeneza. Paulo alituonya kwamba kushiriki meza ya Bwana pamoja na dhambi nafsini mwetu hutusababisha tuwe dhaifu na wagonjwa (1 Wakorintho 11:30). Chuki na kutofautiana sisi kwa sisi ni dhambi ya mauti mbele za macho ya Mungu kwa sababu alisema tutajulikana kwamba sisi tu wanafunzi wake kutokana na upendo tulionao baina yetu na kwa wengine.

Tumeonywa mara ngapi katika vitabu vya Injili na 1 Yohana kuwapenda ndugu? Pia tumeambiwa kwamba upendo wetu kwa Mungu unategemea upendo wetu kwa ndugu (1 Yohana 4:20). Hili ni jambo kubwa la kujishughulisha na Mungu, na kama unataka kumwona Mungu akitembea kanisani mwenu, lazima ukate kamba zote za uchungu na kuanzisha upendano wa ndugu baina yenu.

## 4. Waangalizi

Mchungaji wa kanisa lolote hawezi na asitegemewe kufanya kila kitu yeye peke yake katika kundi. Lazima wawepo waangalizi katika nyumba ya Mungu watakaoliangalia kanisa, wanaume na wanawake walio tayari wenye uwezo wa kupambanua roho ili kutofautisha mema na mabaya. Mambo yanapokuwa mengi sana husababisha kitu chochote kujiingiza bila kujua au kutopata suluhu. Hii ni pamoja na kuliendeleza kanisa, kutoa mahitaji kwa watu, na kuangalia madhaifu yanayoweza kujipenyeza katika kundi, hasa kwa vijana na walio dhaifu. Hakikisha viongozi wameteuliwa ili kusaidia kanisa kuwa na afya.

## 5. Weka Wakristo Waliokomaa Kwa Kila Mkristo Mchanga Anayeokoka

Nafsi zote mpya zilizookoka kwa mara ya kwanza zinatakiwa kupewa Mkristo aliyekomaa ili kuzisaidia kumtumikia Bwana. Mkristo aliyekomaa atakuwa ni rafiki aliyekomaa, aliyejitoa kusoma Biblia pamoja na waamini wapya, kuomba pamoja nao, kutoka nao nje kushuhudia, na kuwaangalia. Haina haja ya shemasi wala mzee kufanya kazi hii bali mtu yeyote ambaye ameshaokoka zamani kutosha kuyafahamu mambo ya msingi katika kumtumikia Bwana. Moja ya baraka kubwa sana nilizoziona mimi kama Mkristo niliyekomaa ni kuwaangalia Wakristo wachanga ili kukua katika Mungu.

Yesu alisema kwamba nia yake ni kwamba tukazae matunda mengi na matunda yetu yakae (Yohana 15:16). Kuna uzuri gani kuokoa nafsi na kisha kuziacha kuanguka tena njiani kwa sababu hakuna mtu katika kanisa anayejali kuzitunza? Yatupasa kujitoa kuwatunza walio wachanga katika Bwana kadiri tuwezavyo kama tufanyavyo kwa watoto wetu wenyewe. Sehemu ya maagizo katika Agizo Kuu ni kuwafanya waamini wapya kuwa wanafunzi wa kila kitu alichotuagiza sisi (Mathayo 28:19).

Kama hatuwajali watoto wetu wachanga, kwa nini tutegemee Mungu kuzileta nafsi zaidi za watu wake kuja kwetu? Haya ni mapigo ya moyo wa uamsho: kuokoa na kulea nafsi mpya.

## 6. Uwe na Maono

Biblia inasema kwamba pasipo maono, taifa huangamia (Mithali 29:18). Lazima uwe na maono ili kufahamu wapi unaelekea ambayo yatakusaidia kuvishinda vikwazo vitakavyoingia njiani mwako. Maono ni zaidi ya ufunuo kutoka kwa Mungu au lengo la kufikia. Maono yana mada iliyozaliwa kutokana na nia. Hiyo hukuendesha kuushinda mwili, kuushinda woga, na kuyashinda mashaka. Maono huleta ushindi.

Lazima uwe na uwezo wa siyo tu kuona zaidi ya upeo wako bali pia kuushika ukweli wake kwa imani inayozalisha shauku ndani yako itakayokutaka kumwamini Mungu vya kutosha hata kusema NDIYO!

kwenye yasiyowezekana. Maono yako lazima yawe makubwa kuliko uwezo wako, makubwa kuliko idadi ya mahudhurio ya Jumapili ya kanisa lako, na makubwa kuliko mwonekano wa kidini unaouona. Maono yako yanapaswa kuhusiana na uamsho utakaolichochea kanisa na kuwaokoa waliopotea kwa ajili ya Kristo. Chochote pungufu ya hicho ni kanisa linalofanya mizaha.

Yesu alitwambia tujikane wenyewe, tuchukue msalaba wetu tumfuate (Mathayo 16:24). Maono yake yalikuwa ni msalaba na ushindi ambao ulipatikana kwa ajili ya nafsi za wanadamu wote. Jinsi gani tutamfuata kama hatuna maono tuliyonayo ya kuvumilia? Tunahitaji maono, la sivyo tutapotelea katika kuwa duni tu.

Maisha yetu daima yana upeo ulio na kikomo tunachoweza kukiona kikituzunguka. Kama unataka uamsho wa kweli wa Roho Mtakatifu, lazima uweke maono yako yaone zaidi ya upeo unaoweza kuuona kwa macho yako na kuona kwa imani yako. Uwe hodari katika kumwamini Mungu na kumbeba kwenye Neno lake. Ni baada tu ya hapo ndipo njia itatokea inayokuongoza kwenye ushindi.

Bwana anatuamuru "kuiandika njonzi [maono] tukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji." (Habakuki 2:2). Yaandike maono yako! Mpaka yatakapokaa kwenye karatasi, bila hivyo hayatakuwepo. Kisha yaweke mahali ambapo

yanaweza kushuhudia uso wako kutwa nzima. Sasa unajua unakoelekea na kwa nini. Sasa unayo dira ya kukuongoza kwenye mwelekeo utakaokusaidia kutimiza wito wako katika Mungu.

Hii ni sawa pia kwa kanisa. Kanisa lako linapaswa kuwa na maono yanayofafanua lengo kuu unalotaka kulifikia. Yaweke ukutani kanisani ili kila mtu aweze kuyaona. Sasa kanisa lako litakuwa na malengo, mwelekeo, na shauku iliyowekwa mbele zako ili kwamba ujue kile unachofanya na kwa nini.

Gharama ya uamsho ni kubwa, na bila kuwa na maono, hautakuwa na shauku ya kulipa hiyo gharama.

## 7. Umezaliwa Mara ya Pili?

Kitabu hiki hakitakuwa kamili bila wito wa kuokoka. Unaweza kuwa Mkristo aliye moto na uliyeokoka tangu miaka mingi iliyopita, au unaweza tu kuwa umechukua kitabu hiki kwa udadisi lakini bado hujampa Yesu maisha yako yote. Yawezekana kwamba umekaa kanisani maisha yako yote, lakini kamwe hujawahi kufanya huo uamuzi wa mwisho wa kumwomba Yesu aokoe nafsi yako kwa kuzaliwa mara ya pili.

Vyovyote itakavyokuwa, kama hujazaliwa mara ya pili, Biblia iko wazi kwamba hutaingia katika ufalme wa mbinguni. Hakuna njia nyingine karibu na hilo. Yesu alisema kwamba kama utajaribu kukwea kwa kupitia

njia/mlango mwingine kuingia mbinguni, utakuwa ni mwizi na mnyang'anyi (Yohana 10:1).

Paulo ameweka muhtasari wa Sala ya Toba kwa ajili yetu:

> *Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. (Warumi 10:9-10).*

Nami nitaweka wazi. Kutamka maneno mengi hayatakuokoa. Ifanye sala aliyoandika mwingine kuwa kilio kutoka moyoni mwako kinachotoka kupitia kinywa chako, ukimlilia Mungu kwamba atakusikia.

Vipengele vya wokovu ni rahisi:

**Tubu dhambi zako.** Zote, kwa uaminifu, na uwe tayari kuziacha milele. Yesu alishakulipia deni la dhambi zako, na lazima uelewe kwamba deni/gharama aliyolipa kwa ajili yako haikuwa ndogo wala rahisi kwa wewe kuilipa. Usifanye huzuni za dhambi zako kuwa ndogo na rahisi. Lazima upondeke kwa dhambi zako. Kama unafikiri unaweza kutamka maombi na kuokoka tu kama kwa muujiza, utaona hayo maneno yako kuwa ni tupu na yanayozaa matokeo hewa. Lazima uje chini ya msalaba katika moyo uliopondeka, ukilia kwa ajili ya

rehema za Mungu. Ni baada tu ya kufanya hivyo ndipo atakusikia.

Kama hautafikia hali hiyo ya moyo uliopondeka na kutokuwa tayari kuziacha dhambi zako, basi mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu akushawishi ili ufikie hatua hiyo ambapo utakuwa tayari kuacha kila kitu na kwenda mwenyewe chini ya msalaba wake. Niamini, Bwana atakujibu.

**Mkiri Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako.** Kubali kwamba ni yeye peke yake ndiye atakayekuokoa, na kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

**Mwombe Yesu akuokoe na kukusafisha ndani ya Damu yake.** Ni damu yake ndiyo iliyo ukombozi (malipo) wa dhambi zako, na ni damu yake ambayo huvunja mgongo wa nguvu za dhambi katika maisha yako. Hakuna matendo mema unayoweza kuyaleta katika madhabahu ambayo yatalipa gharama ya dhambi zako—ni damu ya Yesu pekee.

**Amini.** Imani inahusika zaidi kuliko kutambua tu. Ni kujikabidhi kikamilifu kwenye hii kweli ambayo umeigundua. Mungu husikia kilio cha moyo wako na yuko tayari sana kuliko ulivyowahi kufahamu katika kuiokoa nafsi yako. Anaweza kukusikia, na ameahidi katika Neno lake kwamba atakujibu. [Mwalike na kumwamini Bwana Yesu.] Atakuokoa.

**Mshukuru Mungu.** Kwenye sifa na shukurani zetu, imani huachiliwa na milango ya mbinguni hufunguka.

Inua mikono yako na umsifu Mungu kwa ajili ya wokovu wako.

Maombi hapa chini yanamaanisha tu kama mfano kwako. Kama utatamka haya maombi au yafananayo na haya kama utakavyochagua kutoka moyoni, hakikisha unatamka kutoka ndani ya moyo wako. Usitafute kurudiarudia (kupayukapayuka) ili kufuata desturi za kidini bali kupokea wokovu wa Uzima usio wa kawaida. Omba hivi:

*Bwana wangu na Mungu wangu, uionee huruma nafsi yangu, iliyokutenda dhambi.*

*Naamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai na kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ili nisamehewe dhambi zangu.*

*Naamini Yesu alifufuka tena kutoka kwa wafu kwa nguvu za Roho Mtakatifu na ameketi mkono wa kuume wa Mungu.*

*Bwana Yesu, njoo moyoni mwangu na unioshe dhambi zangu zote kwa damu yako. Nakualika maishani mwangu uje uwe Mwokozi na Bwana wangu na nitakufuata maishani mwangu mwote.*

*Neno lako lasema kamwe hutamtupa mtu nje, nikiwemo na mimi. Kwa hiyo, natambua umenisikia, na ninatambua umenijibu, na ninatambua nimeokoka.*

*Asante Bwana Yesu kwa kuniokoa maisha yangu. [Kwa jina la Yesu nimeomba.] Amina.*

Sasa inua mikono yako na umshukuru na kumsifu Bwana kwa kuiokoa nafsi yako. Fungua moyo wako na umpokee Roho wa Uzima kutoka kwa Mungu.

Sasa umemwomba Yesu kuja moyoni na maishani mwako, unahitaji kutafuta Wakristo wengine waliozaliwa mara ya pili ili kuwa na ushirika nao ambao pia watakusaidia kukua katika Bwana na kukusaidia pia upate Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Mwombe Mungu akuonyeshe kanisa utakalolelewa. Usijitenge na kundi hili. Mungu ana mahali salama kwa ajili yako. Mwombe akuonyeshe wapi anapotaka uhudhurie kanisani, na yeye atakuongoza jinsi ya kufika hapo.

## Hitimisho

Mambo yote niliyokushirikisha katika kitabu hiki yameandikwa katika Neno la Mungu, na yatatimia. Kumekuwepo na uamsho mkubwa sehemu mbalimbali nyakati za nyuma, lakini uamsho mkubwa zaidi ulioahidiwa katika Yoeli 2:23 na Isaya 32 bado haujatimia. Nabii Yoeli ametaja mara sita wakati wa uamsho huu ambao utatokea kabla ya Siku ya Bwana.

Matukio ya wakati huu yanatupatia maana halisi, kwa sababu hali ya kiroho kabla ya siku ya kurudi kwake Bwana mara ya pili inafanana na ile iliyokuwepo kabla ya kuja kwake mara ya kwanza. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu alikuwa ni kama mzizi katika

nchi kavu (Isaya 53:2). Ukame wa kiroho uliwaacha Waisraeli wote wakifa kwa kiu ya kumwona Mungu kwa upya kabla tu ya kuja kwa Yesu mara ya kwanza. Kulikuwa na masinagogi na Mafarisayo katika kila mji, lakini maneno ya huyu nabii aliyetokea katika Israeli yalisababisha maelfu ya wakulima wa kawaida kuacha majembe yao na kutembea umbali mrefu kwenda katika Mto Yordani ili kumsikia Bwana akinena. Kutakuwa na ukame mkubwa zaidi wa kiroho kabla hajarudi, mwanzo halisi wa uamsho. Sijui ukame huo utaisha kwa muda gani au lini utaanza, lakini najua unakuja.

Lakini hautakuja kwenye ulimwengu wa kanisa tunaoufahamu leo hii. Mungu atayapa makanisa muda fulani wa kutubu, na hayatatubu. Kwa nini yasitubu? Hawajioni kama wanatakiwa kutubu. Uamsho ndio utafaa, lakini hawatakuwa na huzuni ya kuhitaji uamsho wowote kwa gharama yoyote. Jambo la kusikitisha kuhusu ukengeufu/kurudi nyuma kiroho ni kwamba blanketi zile zile za starehe na kawaida ambazo kanisa linajifunika ni blanketi zile zile zinazofunika uwezo wa kanisa kuona. Kanisa litakuwa la mwisho katika kugundua jinsi gani limekufa, ingawa hali hii itakuwa wazi kwa kila mtu anayelizunguka.

Kanisa lililokuwa Laodikia, kama Yesu alivyofafanua katika kitabu cha Ufunuo, liko hai katika makanisa yetu sasa. Lilidhani li tajiri na lenye baraka nyingi za Mungu, bali lilikuwa limepofushwa na starehe zake na halikuona mbali jinsi gani lilikuwa limeanguka

kutoka pale lilipokuwa. Madhehebu yaliyokuwa yameanzisha moto wa bandia wa uamsho sasa yamekuwa taasisi za kijamii—zinazonawili, matajiri, zenye mpangilio, sahihi katika elimu ya Mungu ya duniani, na zenye kujivunia urithi ambao sasa haziumiliki tena. Kujivuna kwake hakutawaruhusu kutubu, na kwa hiyo nuru ya kinara chao cha taa ilianza kuzimika pale walipoanza kubweteka katika vivuli vya giza vilivyoongezeka kati yao. Moto wao ambao uliwaka sana hapo mwanzo sasa unaonekana kugeuka kuwa makaa na majivu ambayo sasa ni vuguvugu (Ufunuo 3:16).

Mungu atainua mawe kwenye nafasi zao. Kinachoenea sasa duniani ni kizazi cha Gideoni ambacho kinataka kitu kingine zaidi ya "kanisani kama kawaida." Hawa ni watu Mungu atawaita kutoka kwenye taasisi za kidini zilizokufa ili kuunda jeshi alilolitabiri Joeli katika wakati huu wa vita vya mwisho kati ya Mungu na Shetani kwa ajili ya wokovu wa nafsi za wanadamu.

Hakuna swali kwamba uamsho huu wa mwisho utakuja. Unakuja. Roho Mtakatifu anapiga sauti ya tarumbeta. Swali ni kwamba, wewe utaitikia kwenye wito huo? Kama hautaitikia, basi utaishia kwenye kusimama pembeni kuona jinsi moto wa Mungu utakavyokuwa ukishuka kwa makanisa mengine yaliyokuwa tayari kufanya kile wewe hukutaka. Uchaguzi ni wako.

Rafiki, tunaishi katika wakati wa kushangaza zaidi katika historia yote. Vita vibaya sana vya kiroho vinakuja, na ni kwa ajili ya wakati kama huu kwamba tumeitwa kusimama katika vita hivi vya mwisho. Huu ni mwisho wa mrundikano wa mgogoro ambao umeendelea tangu mwanzo wa wakati huu wa mwisho. Mashujaa wataandaliwa wakati wa vita hivi vya mwisho ambao watang'aa milele na milele. Nakuombea uwe mmoja wao.

Itikia wito, inuka uikabili changamoto, na uwe hodari kumwamini Mungu na kujiandaa kwa uamsho mkubwa kuliko siku zote.

# Kuhusu Mwandishi



Dalen Garris amekuwemo kwenye huduma tangu mwaka 1970 wakati wa huduma ya Jesus Movement huko California Marekani. Mwaka 1997 alianzisha kipindi cha matangazo ya redio ambacho hatimaye kilienea katika makumi ya nchi, tangu Israeli na Saudi Arabia mpaka Afrika na Ufilipino. Kipindi chake cha *Moto Shimoni*, kilichaguliwa kutangazwa katika bara la Amerika ya Kaskazini kwenye mtandao wa Sky Angel kama Sauti ya Yerusalemu.

Baadaye ilifuatiwa na uandishi wa makala zilizochapishwa magazetini, ambapo ameandika zaidi ya makala 700. Pia ameandika makuni ya vitabu na vitini mbalimbali.

Tangu mwaka 2004, amekuwa akiuwasha moto wa uamsho katika makanisa yanayoenea katika ukanda wa jangwa la Sahara barani Afrika. Kwa kipindi cha miaka 17, amehubiri katika makanisa zaidi ya 1,000 na kujionea mamia ya makanisa hayo yakianzisha moto na kukua kwa mlipuko, na mamia ya makanisa mapya yamepandwa barani Afrika. Mamia ya watu wameponywa kwa nguvu zisizo za kawaida wakati wa

kupanga misitari ya uponyaji ambayo mara nyingi imekuwa ukitokea katika hii mikutano ya uamsho, na makumi ya maelfu ya watu wameokolewa. Na bado moto unaendelea kuwaka.

Kwa sababu ya kazi yake barani Afrika, Dalen Garris alitunukiwa Shahada ya tatu ya Udaktari ya heshima mwaka 2017 na Chuo Kikuu cha Kikristo cha Northwestern cha Florida, nchini Marekani. Pia alitunukiwa tunu ya Brevet de Merite kutoka muungano wa makanisa ya Vision Barza Grands Lacs.

Dk. Garris kwa sasa anaishi pamoja na Cindy, mkewe mwenye umri wa miaka 44, mjini Waxahachie Marekani na bado wanajishughulisha sana na makanisa barani Afrika. Tumaini lake kubwa liko katika kuona mtembeo huu wa Mungu wenye nguvu katika Afrika unawachochea na Marekani pia. Garris anaamini kwamba kizazi hiki kinachokuja kitakuwa ni Kizazi cha Gideoni ambacho kitaleta, katika wakati huu wa mwisho, uamsho mkubwa ambao ameuhubiri kwa miaka mingi.

## Vitabu vya Dalen Garris

*Vinapatikana kwenye tovuti ya: www.revivalfire.org/books/*

Hatua Nne za Uamsho / Four Steps to Revival.

Kusimamia Nafasi Wazi / Standing in the Gap.

Maagano Mawili / Two Covenants.

Moto Shimoni / Fire in the Hole.

## Kampeni za Uamsho

Kumbukumbu za Kenya / The Kenya Diaries.

Tarumbeta Nigeria / A Trumpet in Nigeria.

Harufu ya Mvua / A Scent of Rain.

Moyoni mwa Giza / Into the Heart of Darkness.

Moto na Mvua / Fire and Rain.

Kampeni za Uamsho Afrika 2019 / Revival Campaigns in Afrika 2019.

Vita kwa Ajili ya Nigeria / A Battle for Nigeria.

Mapambano katika Nyasi Kavu / A Match in Dry Grass.

Nuru Porini / A Light in the Bush.

## Mfululizo wa Sauti ya Nyikani

Toleo la 1: Safari Imeanza / vol. 1, the Journey Begins.

Toleo la 2: Miaka ya Mwanzoni / vol. 2, the Early Years.

Toleo la 3: Nabii Anatokea / vol. 3, Prophet Rising.

Toleo la 4: Uamsho katika Mbawa / vol. 4, Revival in the Wings

Toleo la 5: Sauti ya Mvua Kubwa / vol. 5, Sound of an Abundance of Rain.

Toleo la 6: Mlinzi, Nini Kimetokea Usiku? / vol. 6, Watchman, What of the Night?

Toleo la 7: Tope na Majemedari / vol. 7, Mud and Heroes

Toleo la 8: Majivu ya Asubuhi / vol. 8, Ashes in the Morning

Toleo la 9: Kuutikisa Mti wa Mzeituni / vol. 9, Shaking the Olive Tree

## Vitini vya Dalen Garris

*Vinapatikana kwenye tovuti ya: www.revivalfire.org/booklets/*

Volkano Mjini Cape Verde / *A Volcano in Cape Verde.*

Tanzania, 2011.

Nigeria, 2012.

Kupanda Mbegu Liberia / Planting a Seed in Liberia.

Filimbi kwenye Upepo / A Whisper in the Wind.

Kukamilisha Kile Tumekianzisha / Finishing What We Started.

Maagano Mawili / Two Covenants.

Ukalvari Umekosolewa / Calvinism Critiqued.

Kama utapenda Dk. Dalen Garris awe mnenaji katika kanisa lenu au taasisi yenu, tafadhali wasiliana nasi kwa ajili ya kupata muda na ratiba. Hatutozi fedha, wala kamwe hatutatoza, ili kuihubiri Injili kila mahali ulimwenguni.

**RevivalFire Ministries**

Dr. Dalen Garris
PO Box 822, Waxahachie, TX
Barua pepe: dale@revivalfire.org
Tovuti: www.RevivalFire.org